Published on *Books on Islam and Muslims | Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)



# Ukweli Uliopotea - Sehemu ya Nne

Madhehebu Nne chini ya Darubini


### Author(s):

Sheikh Mu'tasim Sayyid Ahmad [3]



### Publisher(s):

Al Itrah Foundation [4]


Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kiitwacho al-Haqiqatu 'dh-Dha'i'ah kilichoandikwa na Sheikh Mu'tasim Sayyid Ahmad. Sisi tumekiita, Ukweli Uliopotea. Kwa vile kitabu hiki ni kikubwa, sisi tumekigawa katika juzuu tano ili kiwe chepesi kusomwa na wasomaji wetu wa Kiswahili. Hiki ulichonacho mkononi mwako ni juzuu ya tano.

Kitabu hiki ni utafiti uliofanywa na mwanachuoni huyo wa Kiislamu kuhusu madhehebu za Kiislamu. Utafiti wake huu ulihusisha pia mahojiano na mijadala baina yake na na masheikh wa Kiwahabi na maustadh wake katika chuo alikosoma.


### Translator(s):

Sheikh Harun Pingili [5]

### Category:

General [6]

**Topic Tags:**

Historia [7]

Dini [8]

Madhehebu [9]

**Person Tags:**

Imam Ahmad bin Hanbal [10]
Imam Jaffar Sadiq (as) [11]
Imam Malik Bin Anas [12]
Imam Abu Hanifa [13]

# Neno La Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kiitwacho *al-Haqiqatu 'dh-Dha'i'ah* kilichoandikwa na Sheikh Mu'tasim Sayyid Ahmad. Sisi tumekiita, *Ukweli Uliopotea*. Kwa vile kitabu hiki ni kikubwa, sisi tumekigawa katika juzuu tano ili kiwe chepesi kusomwa na wasomaji wetu wa Kiswahili. Hiki ulichonacho mkononi mwako ni juzuu ya nne.

Kitabu hiki ni utafiti uliofanywa na mwanachuoni huyo wa Kiislamu kuhusu madhehebu za Kiislamu. Utafiti wake huu ulihusisha pia mahojiano na mijadala baina yake na na masheikh wa Kiwahabi na maustadh wake katika chuo alikosoma.

Kama kawaida katika utafiti wake, ametumia sana vitabu vya historia ya Kiislamu na vya hadithi vilivyoondikwa na wanavyuoni wa Sunni na Shia, kisha akahitimisha kwa Qur'ani Tukufu na Sunna. Baadhi ya vitabu hivyo ameviorodhesha ndani ya kitabu hiki ili msomaji aweze kuvirejelea. Lakini bahati mbaya sana mengi ya matoleo mapya ya vitabu hivyo yamefanyiwa mabadiliko na baadhi ya sehemu kuondolewa, hususan zile zinazounga mkono madai ya Shia. Ufuatao hapa chini ni mfano mdogo tu wa yanay- ofanywa katika vitabu hivyo:

Katika ukurasa wa 301 wa juzuu ya 3 ya *Tafsir al-Kashshaaf* iliyokusany- wa chini ya maelekezo ya Sheikh Mustafa al-Halabi (toleo la pili, 1319 A.H. liliochapishwa na Main Government Printing House ya Amiriah Bulaq ya Misri), beti zinazojitokeza ambazo kwazo Jarallah Zamakhshari, mfasiri wa *al-Kashshaaf,* alitangaza wazi imani yake katika uhalali wa Ushia. Lakini katika toleo la mwaka wa 1373 A.H. kutoka Printing House Istiqamah bi 'l-Qahara, shairi lililotajwa halionekani tena.

Marehemu Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi katika kitabu chake kiitwa- cho, *Uimamu,* ukurasa wa 37, anaandika kushangazwa kwake kutokana na maneno yaliyoondolewa katika kitabu cha *at-Tarikhat-Tabari,* chapa ya Leiden (ya mwaka 1879 Miladia).

Chapa hii ya Leiden imeyanakili maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w.) aliyoyatumia wakati wa karamu mashuhuri ya ndugu wa karibu aliyoitayarisha ambapo katika khutba yake alisema: "Enyi watu wangu!

Huyu Ali ni ndugu yangu, Wasii wangu na Khalifa wangu miongoni mwenu; msikilizeni na mtiini." Lakini katika chapa ya Misri ya mwaka 1963, (chapa inayodaiwa kuwa imechekiwa na ile ya Leiden) maneno haya muhimu: "Wasii wangu na Khalifa wangu" yamebadilishwa na kuandikwa "kadha wa kadha" na kusomeka hivi: "Huyu Ali ni ndugu yangu na kadha wa kadha." Huu ni msiba mkubwa.

Huu ni mchezo umefanywa na unaendelea kufanywa mpaka leo. Na lengo ni kuficha ukweli. Lakini hata hivyo, 'ukweli siku zote unaelea'; matoleo ya zamani yapo mengi na yamehifadhiwa kwenye maktaba zetu.

Ni muhimu kufikia kila aina ya maoni katika kujaribu kuamua ukweli. Uislamu kimsingi uko dhidi ya kufuata kibubusa. Utafiti huu umefanywa ili kuwaelemisha Waislamu kwa ujumla juu ya madhehebu za Kiislamu ili kujenga maoni yao kuhusu mtazamo mzuri wa mtu mwenyewe, na ni muhimu mtu kuelewa hoja za wale ambao hakubaliani nao. Inawezekana kusemwa kwamba wale ambao hawaelewi kabisa mtazamo wa maoni tofauti, hawaelewi kwa ukamilifu (mtazamo) wa kwao wenyewe.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni mambo ambayo hayana nafasi tena katika akili za watu.

Kutokana na ukweli huo, taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu, Sheikh Harun Pingili kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

**Mchapishaji:**
**Al-Itrah Foundation**
**S. L. P. 19701**
**Dar-es-Salaam, Tanzania**.

# Hadiya

Kwa aliyezaliwa kwenye ngome ya umaasumu na uchamungu, na mashukio ya wahyi na uongofu, na mrithishwa wa fadhila tukufu na ukarimu.

Imwendee mwanamke mwema, na mpambanaji mtoa nasaha, aliye huru mkataaji, na ni muujiza Muhammadiyah, na ni hazina Haydaria, na ni amana Fatmiyah.

Imwendee aliyekuwa mtii wa Mwenyezi Mungu, katika hali ya siri na ya wazi, na aliyetoa changamoto kwa msimamo wake dhidi ya wanafiki na wafitini.

Imwendee aliyewatia hofu masultani wakorofi kwa msimamo wake thabiti, na alizishangaza akili kwa umadhubuti wa moyo wake, na alifanana na baba yake Ali kwa ushujaa wake, na alishabihiana na mama yake Zahra'a kwa utukufu wake na balagha yake.

Imwendee aliyenasibika na ukoo wa kinabii na uimamu, aliyetunukiwa shani ya cheo, utukufu na karama.

Imwendee shujaa wa Karbalaa bibi wa kibani Hashim.

*Sayyidatiy wa Maulatiy Zaynab* (*a.s.*).

# Mlango Wa Nane

## Madhehebu Manne Chini Ya Darubini

Kwa kweli athari za Saqifa na kuugeuza ukhalifa kutoka kwa Ahlul-Bayt zimekuwa kinyume katika kila nyanja zikiathiri kinyume katika historia na elimu ya Hadithi, na elimu nyingine zisizokuwa hizo. Na athari zake za wazi zimejitokeza katika fiqhi ya kiislamu, kwa mujibu huo madarasa za kifiqhi zimekithiri na kujitenga mbali na zingine.

Historia imenakili kuwa kila jamaa yapendelea fikra za chuo chake cha kifiqhi na yaliyotokea kati yao, kama vile ilivyoweka wazi sauti zilizopanda na mzozo hadi kufikia daraja ya kukufurishana, pia imetuwekea wazi mchango wa utawala unaohukumu jinsi ulivyokuwa ukiichezea dini ya waislamu, kwa hiyo mwanachuoni anayeafikiana nayo kulingana na utashi wake yeye huwa ndio imamu wa waislamu na dola huwalazimisha watu kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja kumfuata na kumtii.

Rejea za kifiqhi zimetia nanga baada ya hali nyingi tofauti zilizojiri juu ya wanne miongoni mwa mamia ya mujtahidina na hao ni: Malik, Abu Hanifa, Shafii na Ahmad bin Hanbali. Halafu ijtihadi ilipigwa marufuku baada ya hawa na watu wote walipopewa amri ya kuwafuata hawa wanne. N

a hilo larejea katika historia ya mwaka 645 A.H. pale mamlaka iliyokuwa inatawala ilipoona kuwa masilahi yake yapo katika kuiwekea wigo ijtihadi kwa hawa masheikh wanne.

Na kundi miongoni mwa wanavyuoni lilipendelea fikra hii na walitangaza kuliunga mkono kwao. Na kundi lingine lilizingatia kitendo hiki kuwa ni kuukandamiza uhuru na kupokonya uwezo wa mtu. Ibnu Al-Qayim ametunga mlango mrefu katika kitabu *Iilamul-Muwaqiina*, humo amefuatilia dalili za wasemao wajibu wa

kuufunga mlango wa ijtihadi na kuusimamisha, kwa dalili zenye nguvu.

Japokuwa rai isemayo ni wajibu kusimama kwenye ijtihadi za maimamu wanne zipo kinyume na dini na akili iliyo salama, ila ni kwamba ilikuwa ndio yenye ushindi kwa sababu ya kuungwa mkono rai hii na dola ambayo inadhamini maslahi yake.

Ustadh Abdul-Mutaali Swaiidiy anasema: "Kwa hakika mimi naweza kuhukumu baada ya hivi kuwa kuzuia ijtihadi kulifanyika kwa njia za kidhalimu, na kwa nyenzo za kulazimisha na kuvutwa kwa kupewa mali, na hapana shaka nyenzo hizi lau zingepatikana kwenye madhehebu yasiyokuwa haya manne - ambazo tunazifuata hii leo – jamhuri ingebaki inazifuata pia na zingekuwa zakubalika hivi sasa kwa wanaozikataa.

Basi sisi tuko huru hatulazimiki kujifunga na madhehebu hizi nne ambazo tumelazimishwa nazo kwa njia hizo mbaya, na tuko huru kurejea kufanya ijtihadi katika hukumu za dini yetu, kwa kuwa kuizuia kwake hakukufanyika ila kwa njia ya mabavu, na uislamu hauridhii ila lipatikanalo kwa njia ya ridhaa na ushauri kati ya waislamu. Kama alivyosema (s.w.t.): **"Na mwenendo wao ni kushauriana wao kwa wao"** (***Surat Shura***: **38**)"[1]

Huu ni ukweli mchungu aufikiao mtafiti mwenye insafu katika historia ya madhehebu manne, kwa haki gani wamewajibishiwa waislamu kufanya ibada kupitia mmoja wao, na kwa dalili gani wanavyuoni wamezuiliwa ijtihadi, na kwa nini wamechaguliwa hawa wanne na si wengine?! Hali wakiwepo wanavyuoni wenye elimu zaidi na bora kuliko wao. Kwa mfano:

### Sufian Thauriy:

Alizaliwa mwaka 65 A. H. Alikuwa na madhehebu mahsusi lakini hakuyafanyia kazi kwa muda mrefu kwa uchache wa wafuasi, na kutokuungwa mkono na utawala. Naye ni mmoja wa wanafunzi wa Imam Sadiq (a.s.) na mhitimu wa madrasa yake, na azingatiwa kuwa miongoni mwa wanavyuoni ambao hufanyiwa safari mtu kwenda kwake kutafuta elimu, na kutoka kwake wameelezea (wasimulizi wa hadithi) ishirini elfu. Mansur alitaka amuue hakufanikiwa na alikimbia akijificha mbali naye mpaka alipokufa mwaka 161 A.H. Madhehebu yake yalibaki yakitendewa kazi mpaka karne ya nne.

### Sufian Bin Uyayna:

Mwanachuoni na mwanafiqhi thabiti aliichukuwa elimu kutoka kwa Sadiq (a.s.), Zuhriy na Ibnu Diynar na wengine. Shafii amesema kumhusu: "Sijapata kumuona mwenye kutosheleza kuliko yeye katika kutoa fatwa." Na ana madhehebu yalikuwa yakitendewa kazi yametoweka katika karne ya nne.

### Al-Awzaiy:

Al'Awzaiy alikuwa miongoni mwa wanazuoni, madhehebu yake yalienea Sham - Syiria – na watu wa Sham walifanya ibada kwa mujibu wa madhehebu yake kwa muda, na Al-Awzaiy alikuwa akiheshimiwa

na kuwa mtu wa karibu na dola. Alikuwa miongoni mwa wanaoiunga mkono na kwa minajili hiyo dola ilimfanya nembo ya kidini.

Na walipoingia watawala wa Bani Abbas walimsogeza karibu kwa sababu ya nafasi yake kwa watu wa Sham. Hivyo Mansur alikuwa anamtukuza na kumtumia alipomtambua kuwa amepotoka mbali na ali Muhammad swalawatullahi alayhim.

Lakini pamoja na hayo madhehebu ya Al-Awzaiy yalitoweka alipoainishwa Muhammad bin Uthman, mfuasi wa Shafii kuwa Kadhi wa Damascus, hapo basi hukumu ikawa kwa mujibu wa madhehebu ya Shafii na aliyalazimisha katika Sham, kiasi kwamba watu wa Sham waligeuka na kuwa mashafi mwaka 302 A.H.

Na wengine miongoni mwa makumi ya mamujtahidi mfano wa Ibnu Jarir Tabariy, Daudi Ibnu Ali Dhwahiriy, Al-Liyth Ibnu Said, A'amash, Shaabiy na wengine.

Kwa nini zilibaki madhehebu haya manne na yakaenea na si mengine?! Je maimamu wake walikuwa watu wenye elimu zaidi kuliko wengine katika zama zao?! Au ridhaa za watu zilijikusanya na kuwafanya wao ndio maimamu wao?

Haya yote hayakuwa kwa madhehebu haya manne. Yakutosha historia ambayo yathibitisha kuwepo kwa wanavyuoni ambao walikuwa na elimu zaidi kuliko wao. Kwani akili peke yake inahukumu kutokuwepo kwa sharti hili, kwa sababu kuuwekea mpaka ujuzi ni jambo gumu. Kama ambavyo kuenea kwa madhehebu haya na maimamu wake kuwa mashuhuri haikuwa katika hali na mazingira yenye uhuru na usafi wa kielimu, bali yadhihiri kwa mwenye kufuatilia hali yake kihistoria kuwa haya madhehebu yalilazimishwa juu ya waislamu katika wakati ambao waislamu hawakuwa makini katika jambo lao.

Ama watu kuafikiana na kuwaridhia ni jambo halikuwa na athari katika historia ya kiislam, bali lilikuwa kinyume kabisa. Kila watu waliipendelea madhehebu yao na walikebehi zile itikadi za wenzao, mpaka ulifikia kuwa mzozo wa kumwaga damu, maelfu ya waislamu wamekwenda muhanga, kwa minajili hiyo walikuwa maadui wanaohasmiana na waliwatendea baadhi yao utendewaji wa waliotoka nje ya dini, kiasi kwamba Muhammad bin Musa al-Hanafii ambaye alikuwa Qadhi wa Damascus, aliyefariki dunia mwaka 506 A. H. akasema: ''Lau ningekuwa na kauli ningechukua Jizya[2] kutoka kwa mashafii."

Na Abu Hamidi Tusiy aliyefariki mwaka 567 A.H. anasema: "Lau ningekuwa na amri ningewawekea mahambali kodi."

Hivyo matukio kati ya mahanafii na mahanbali na kati ya mahanbali na mashafii yalikithiri. Wakawa makhatibu wa kihanafii wanawalaani mahanbali na mashafii juu ya mimbari. Na mahambali wanaunguza msikiti wa mashafii huko Muruwu. Moto wa fitna na upendeleo kati ya mahanbali na mashafii ulilipuka huko Nisabur hivyo soko na madrasa zilichomwa moto, walikithiri waliouwawa upande wa mashafii. Halafu mashafii wanavuka kiwango katika kulipa kisasi kwao na hilo lilitokea mwaka 554 A.H. Na mfano kama huo ulitokea kati ya mashafii na mahanbali, mpaka dola ililazimika kumaliza mzozo kwa nguvu, na

hilo lilitokea mwaka 716 A.H.[3]

Mahanbali walikuwa wanaacha kazi zao kwa amani na wanafanya fujo Baghdad, na walikuwa wanajihami kwa vipofu dhidi ya mashafii ambao waliokuwa wanakimbilia msikitini, ikiwa mtu wa madhehebu ya Shafii atawapitia, hatimaye watampiga.[4]

Na madhehebu mengine yanajikusanya dhidi ya Hanbali kughadhibika dhidi ya vitendo vya Ibnu Taymiyyah. Palinadiwa huko Damascus na mahali pengine kuwa: Mwenye kuwa katika dini ya Ibnu Taymiyyah mali yake na damu yake ni halali. Kwa maana ya kuwa wao hutendewa watendewavyo makafiri wapiganaji. Na kwa kulikabili hilo twamkuta Sheikh Ibnu Hatim ambaye ni Hanbali anasema: "Asiyekuwa Hanbali si mwislamu."[5] Hivyo yeye anawakufurisha waislamu wote isipokuwa

Hanbali, na kinyume chake ni Sheikh Abu Bakr al-Maghribiy, yeye ni mhutubu katika vyuo vikuu vya Baghdad, yeye anawakufurisha Hanbali wote.[6]

Na mengine miongoni mwa matukio ambayo yanaliza nyoyo. Baadhi ya upendeleo binafsi umefikia kuwaua wanavyuoni na wanafiqhi kwa hila, kwa kutumia sumu. Na mwanachuoni huyu Abu Mansur aliyefariki mwaka 567 A.H. mahanbali wamemuuwa kwa sumu kwa msukumo wa chuki dhidi yake. Ibnu Al-Jawzi amesema: "Kwa kweli Hanbali walimtuma mwanamke kwa hila alikuja kwake na sahani ya haluwa, na akasema: 'Ewe bwana wangu hii ni katika ufumaji wangu.' Alikula yeye, mkewe, mtoto wake na mtoto wake mdogo, na hatimaye wakawa maiti, alikuwa miongoni mwa wanavyuoni wa kishafiiy waliojitokeza."[7] Na wengi walio mfano wao miongoni mwa wanavyuoni waliouliwa na upanga wa chuki binafsi.

Ni kama hivi kila kundi lilikuwa linafanya upendeleo kwa ajili ya maimamu wao kiasi kwamba wao waliweka Hadithi za ubora wao na walizinasibisha kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kwa uwongo na uzushi, kwa hiyo zikawatoa nje ya mipaka ikubaliwayo kiakili iwezayo kupimika. Na mfano wa Hadithi walizomnasibishia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): "Kwa hakika Adam alijionea fahari kwa mimi, na mimi najionea fahari kwa mtu miongoni mwa umma wangu jina lake ni Nuuman." Kwa sura nyingine imekuja: ''Manabii wanajionea fahari kwa mimi, na mimi najionea fahari kwa Abu Hanifa, mwenye kumpenda amenipenda mimi na mwenye kumchukia amenichukia mimi."[8]

Kwa hakika walikumbwa na uvukaji mpaka kumhusu Abu Hanifa mpaka wakasema katika fadhila zake: Mwenyezi Mungu amemfanya awe mahsusi kwa sheria na kwa karama, na katika jumla ya karama zake ni kuwa al-Hidhru alikuwa akija kwake kila siku wakati wa asubuhi na alikuwa akijifundisha kwake hukumu za sheria muda wa miaka mitano, na alipokufa al-Hidhru alimuomba Mola wake akasema: "Ewe Rabi, ikiwa mimi nina daraja kwako mpe idhini Abu Hanifa anifundishe kutokea kaburini kama kawaida yake ili niwafundishe watu sheria za Muhammad kwa ukamilifu, ili nipate *tarika*."
Mola wake akamkubalia ombi hilo. Hidhru darasa lake lilitimia kwa Abu Hanifa hali akiwa kaburini mwake. Mpaka mwisho wa hadithi hii ambayo husomwa kwenye majlisi za kihanafi misikitini mwao huko uhindini."[9]

Na watu wa madhehebu ya Malik wamejigamba mambo mengi kumhusu imamu wao, miongoni mwayo ni kuwa: Imeandikwa pajani kwake kwa kalamu ya Kudura: ''Malik ni hoja wa Mwenyezi Mungu katika ardhi yake.'' Na kuwa yeye anahudhuria kwa maiti miongoni mwa swahiba zake kaburini mwao na kuwaondoa malaika wawili mbali na maiti, wala hawaachi wamuhesabu amali zake.10

Na imeelezwa kuwa kitabu chake *al-Muwatau* kilitupwa majini wala hakikulowa.

Wanahambali wamesema kumhusu imamu wao: ''Ahmad bin Hambali ni imamu wetu na asiyeridhia ni mtu wa bidaa. Hivyo basi kulingana na kanuni hii waislamu wote wasioukubali uimamu wa Ahmad ni watu wa bida.''

Na wanasema kuwa hajafanya jambo la uislamu yeyote baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kama alivyofanya Ahmad bin Hanbali, wala Abu Bakr Swiddiq hakufanya mfano wake. Na kuwa Allah alikuwa akilizuru kaburi lake. Kama alivyoeleza Ibnu al-Jawziy katika *Manaqib Ahmad* Uk. 454, amesema:

"Amenihadithia Abu Bakr bin Makarim Ibn Abi Ya'aliy al-Harbiy – alikuwa Sheikh mwema – Amesema: 'Ilikuja mvua nyingi mno katika baadhi ya miaka kabla mwezi wa Ramadhani haujaingia kwa siku chache, usiku mmoja nililala katika mwezi wa Ramadhan niliona usingizini kana kwamba nimekuja kwenye kaburi la imamu Ahmad bin Hanbali namzuru kama kawaida yangu. Nikaona kaburi lake limeambatana na ardhi kadiri ya safu – yaani safu ya mchanga au tofali - au safu mbili, nikasema: Hakika haya yamelifika kaburi la Imam Ahmad kwa sababu ya wingi wa mvua. Ghafla nikamsikia akisema toka kaburini:

"'Hapana hiyo ni haiba ya al-Haqi Azza Wajalla, alinizuru nikamuuliza siri ya ziara yake kwangu kila mwaka, Azza Wajalla akasema: Ewe Ahmad ni kwa sababu wewe umeyanusuru maneno yangu kwa hiyo yanaenezwa na yanasomwa katika mihrabu.' Niliuendea mwana ndani wake na kuibusu halafu nilisema: Ewe Bwana wangu nini siri ya kuwa halibusiwi kaburi la yeyote ila kaburi lako? Aliniambia: Ewe mwanangu hii sio karama kwangu lakini hii ni karama ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kwa sababu mimi nina vijinywele kutoka kwenye nywele zake swalallahu Alayhi Wasalam, mwenye kunipenda mimi ananizuru katika mwezi wa Ramadhani. Alisema hivyo mara mbili."

Na mengine miongoni mwa sifa njema ambazo zajulisha upendeleo wao na uvukaji wao mipaka uliyo mbaya mno, na umejitokeza upendeleo huu waziwazi kabisa katika mashairi yao.

Mshairi wa kihanafii akasema: *Madhehebu ya Nuuman madhehebu bora, mwezi ung'arao na ni sayari bora.*

Na mshairi wa kishafii anasema: *Mfano wa Shafii kati ya wanavyuoni ni mfano wa Badru katika nyota za mbingu.*

*Mwambie alinganishwaye na Nuuman kwa ujinga. Je giza hulinganishwa na nuru!*

Na mshairi wa Malik asema: *Wakisema vitabu vya elimu ni hai, je kitabu al'**Muwatau** ni utunzi wa Malik!*

Hali ni kama hiyo kila mmoja avutia moto kwenye mkate wake, na anamshabikia imamu wake, na kujionea fahari madhehebu yake na anajiepusha mbali na madhehebu nyingine mpaka ilisemwa: ''Kwa kweli mwenye kuingia uhanafii huvuliwa, na mwenye kuingia ushafii huadhibiwa."[11]
Na Bw. Sabakiy ameeleza katika kitabu *Tabaqatus-Shafiiyyah* kwa kauli yake: "Hivyo huyu Abu Said aliyefariki mwaka 562 A.H. alikuwa madhehebu yake ni Hanafiya na aligeuka na kuwa Shafiiya, ndipo alipata taabu na kutihaniwa kwa ajili hiyo.

Na huyu Samaniy alipohama madhehebu ya Hanafi alipata mtihani na taabu, na zilifanyika vita, na moto wa fitna ulikolezwa kati ya makundi mawili, ilikuwa unajazwa kati ya Khurasani na Iraqi, na kwa ajili hiyo watu wa Muruu waliyumba myumbo wa kufadhaisha, mlango wa matatizo ulifunguliwa.

Na watu wa rai walijiambatanisha na watu wa hadithi, na walikweda mlangoni kwa Sultani..."[12] Mpaka mwisho wa aliyosimulia.

Matukio kama haya ni mengi hayahesabiki. Na tuliyotaja yanatosha kama mfano wa harakati wa tofauti na upendeleo kati ya madhehebu manne, mpaka ikawa kuficha madhehebu ni lazima.

Abu Bakr Muhammad bin Abdil-Baaqi aliyefariki mwaka 535 A.H., alikuwa Hambalia, anaelezea hali ya kuficha kwa kauli yake: "Hifadhi ulimi wako usihalalishe vitatu: Jino, mali uwezavyo na madhehebu."

Zamakhshariy amebainisha tofauti na ukali wa kulumbana kati ya madhehebu kwa kauli yake:

"*Wakiuliza madhehebu yangu siyadhihirishi.*
*Nitayaficha ufichaji wa kusalimika kwangu.*

"*Ukisema ni Hanafiya, watasema kuwa:*
*mimi nahalalisha Talaa, nacho ni kinywaji haramu.*

"*Ukisema ni Shafiiya, watasema kuwa:*
*mimi nahalalisha ndoa ya binti hali binti ni haramu.*

"*Ukisema ni Malikiya, watasema kuwa:*
*mimi nawahalalishia kula mbwa nao ni wao.*

"*Ukisema ni Ahlilhadithi na kundi lake,*
*watasema beberu hajui wala hafahamu*."[13]

## Kisimamo Pamoja Na Maimamu Wa Madhehebu Manne

Kwa hakika kufanya utafiti kuhusu historia ya mimamu wa madhehebu manne kuna ugumu. Kwa kuwa kuzipata habari zao ni ima iwe kwa kuzinakili kutoka kwa wenye kuwapendelea walio na uvukaji mipaka

kuwahusu wao, au iwe kupitia maadui zao wanaowasingizia, na kati ya safu mbili hizi zinazopingana ni vigumu kutoka na mtizamo wa pekee ulio safi.

Ahmad Amin anasema: "Kama ambavyo upendeleo wa kimadhehebu umewafanya baadhi ya wafuasi wa kila madhehebu wazushe habari ili kuinua hadhi ya imamu wao, kutokana na mlango huu ni Hadithi walizoeleza kuwa Nabii (s.a.w.w) alibashiri kumhusu kila imamu, mfano wa ilivyoelezwa kuwa Nabii (s.a.w.) alisema kuhusu watu wa Iraqi:

'Mwenyezi Mungu ameweka hazina ya elimu yake katika wao.' Na mfano:
'Katika umma atakuja kuwepo mtu ataitwa Nuuman bin Thabiti, kuniya yake itakuwa ni Abu Hanifa, mkononi mwake Mwenyezi Mungu atahuisha Sunna yangu katika Uislamu.' Mpaka mwisho imefikia kudhania kuwa Taurati imembashiri Abu Hanifa. Ni kama hivyo wamefanya baadhi ya mashafii kumhusu Shafii na mamaliki kumhusu Malik, na halikuwatosha hilo. Kwa minajili hiyo imekuwa vigumu kwa mtafiti kuelewa historia sahihi ya kila imamu. Ilikuwa kila kikija kizazi kinazidisha fadhila za imamu wake."14

Ni Abu Hanifa peke yake amepata bahati ya fadhila hizi kwa kuwekewa kundi la vitabu. Tunataja miongoni mwavyo kwa mfano tu: *Uqudul- Marjani Fii Manaqibi Abi Hanifan-Nuuman* cha Abu Ja'far at-Tahawiy, *Manaqibu Abihanifa* cha al-Khawarzamiy, *al-Bustanu Fii Manaqib Ibni Nuumani* cha Sheikh Muhiyudin Abdul-Qaadir bin Abil-Wafaa.

Na *Shaqaiqun-Nuumani Fii Manaqib Ibni Nuumani* cha Zamakhshariy. Na vingine. Na hii ikijulisha lolote itakuwa yajulisha daraja ya uvukaji mipaka na upendeleo kwa ajili ya Abu Hanifa, mzozo na kupaza sauti kuzihusu madhehebu na maimamu wa madhehebu hizo, vinginevyo kuna haja gani ya kuandika vitabu hivi vyote, ambavyo hawakuipata hadhi kama hii Khulafau Rashidun (Abubakr, Umar na Uthman)?!

Na kati ya safu mbili hizi zinazopingana ambazo ni uvukaji mipaka na kusingizia, tutajaribu kufichua mtazamo wa pekee wa historia ya madhehebu na kiwingu kilicho tanda juu ya wazo hili.

# Imamu Abu Hanifa

## Makuzi Ya Abu Hanifa:

Yeye ni Nuuman bin Thabit, alizaliwa mwaka 80 A.H, zama za ukhalifa wa Abdul Malik bin Marwani. Na amefariki huko Baghdad mwaka 150 A.H. Ameinukia katika mji wa Kufa, wakati wa al-Hujjaj. Na Kufa ulikuwa ni mojawapo ya miji mikubwa ya Iraqi ambayo duru za elimu zilikomaa. Shauku zenye kupingana, na rai katika mapambano ya kisiasa, elimu, na misingi ya itikadi vilionesha mduwazo wakati ule. Katika hali hii Abu Hanifa alijitokeza na ubingwa wa theolojia (*scholastical*) na mjadala, alifanya majadiliano humo mjini. Halafu alihamia kwenye duru za fiq'hi mpaka zikawa mahsusi kwake. Na alisoma kwa Hamad bin Abi Sulayman aliyefariki dunia mwaka 120 A.H.

Na alikuwa miongoni mwa wanafunzi wake wenye kujitokeza mno, na Abu Hanifa alikuwa wa pekee baada ya kufa Hamad, hivyo basi sauti yake ilisikika na jina lake likawa mashuhuri, pia alikuwa

amesoma kwa masheikh wa zama zake, na alihudhuria kwa Atai bin Rabbahi huko Makka, na kwa Naafiu huria wa Ibnu Umar huko Madina, na kwa wengine. Na alikuwa anabaki sana na Hammad bin Sulayman, na alichukuwa riwaya kutoka kwa Ahlul-Bayt, kwa mfano kutoka kwa Imam Muhammad al-Baqir na mwanawe As-Swadiq (a.s.).

## Fiqhi Ya Abu Hanifa:

Abu Hanifa hakujulikana kuwa na Fiqhi makhsusi isipokuwa kwa njia ya wanafunzi wake. Hivyo yeye mwenyewe hakuandika fiqhi wala hapakusajiliwa kitu kutoka katika rai zake. Na Abu Hanifa alikuwa na wanafunzi wengi, lakini walioyachukua madhehebu yake na kuyaeneza ni wanne, nao ni: Abu Yusuf, Zufar, Muhammad bin al-Hasan al-Shiibaniy na al-Hasan bin Ziyad al-Luuluiy.

Abu Yusuf ambaye ni Yaaqubu Bin Ibrahim ametoa mchango mkubwa kuieneza madhehebu ya Hanafii. Alipata bahati ya kukubaliwa na makhalifa wa kibani Abbas, naye alishikilia uraisi wa ukadhi katika zama za al-Mahdiy na al-Hadiy na Rashid, na alipata kwa Rashid hadhi makini.

Hivyo Abu Yusuf alifurahia cheo hiki akakitumia kueneza madhehebu ya Hanafii katika nchi nyingi mikononi mwa makadhi aliokuwa akiwaainisha katika swahiba zake, ikawa kupita kwa sauti ya madhehebu ya Hanafii kwategemea nguvu yake.

Ibnu Abdil-Bari amesema kuhusu hilo: “Abu Yusuf alikuwa Kadhi wa makadhi, alikuwa Kadhi wa makhalifa watatu, alitawalia ukadhi baadhi ya siku za al-Mahdiy kisha akawa Kadhi wa al-Haadiy halafu wa ar-Rashid. Na ar-Rashid alikuwa anamheshimu na kumtukuza, na alikuwa kwake mwenye hadhi makini. Kwa ajili hiyo yeye alikuwa na mkono mrefu katika kueneza utajo wa Abu Hanifa na kuinua daraja yake kwa sababu ya nguvu ya usulutani na usulutani wenye nguvu.”[15]

Mwanafunzi wa Abu Hanifa, Muhammad bin al-Hasan al-Shiiban ameshiriki kuitangaza madhehebu ya Abu Hanifa kwa tunzi zake ambazo ziligeuka kuwa ndio rejea ya kwanza ya fiqhi ya Abu Hanifa, japo kuwa yeye ni mwanafunzi pia wa Thauriy, al-Awzaiy na Malik. Na aliingiza Hadithi katika fiqhi ya wafuasi wa rai.

Ama Zufar Ibnu Hudhaili naye ni miongoni mwa swahiba wa mwanzo wa Abu Hanifa. Aliyaeneza madhehebu ya Abu Hanifa kwa ulimi wake, na alitawalia ukadhi katika zama za Abu Hanifa huko Basra. Alikuwa mfanya ulinganishi sana, kiasi kwamba Ahmad bin al-Maadil al-Maliky alimdhihaki kwa kauli yake: “Ukiwa muongo uliyonihadithia ni juu yako dhambi za Abu Hanifa au Zuffar, wafanyao ulinganishi makusudi, wasiopenda kushikamana na habari.”

Abu Hanifa na swahiba zake walikuwa wanaaibishwa sana kwa kufanya ulinganishi. Na imeelezwa katika kitabu *Iqdul-Farid*, Uk. 408 kuwa: “Musawiru akasema kumuhusu Abu Hanifa: ‘Tulikuwa na wasaa kabla ya hii leo katika dini, mpaka tulipopatwa na balaa la watu wa ulinganishi. Wametoka sokoni mapato yao yaliposimama, wakatumia rai baada ya juhudi na umasikini.”’

Abu Hanifa alikutana naye akamwambia: ‘’Umetudhihaki ewe Musawiru, sisi tutakuridhisha.’’ Akampa Dirham - (pesa za huko).

Listaajabishalo ni kuwa wanavyuoni walioasisi madhehebu ya Hanafii na kuyaandika, hawakuwa wenye kumfuata Abu Hanifa katika rai zake, bali walikuwa ni wanavyuoni wanaojitegemea, pengine wanaafikiana na ustadhi wao na kuwa tofauti naye mahali pengine. Kwa ajili hiyo tunavikuta vitabu vya kihanafi vina kauli nne katika mas’ala moja. Abu Hanifa ana kauli yake, Abu Yusuf ana kauli yake, Muhammad ana kauli yake, na Zuffar ana kauli yake.

Allama al-Khudhwiriy anasema: ‘’Baadhi ya mahanafii wamejaribu wazifanye kauli zao zilizotofautiana kuwa ni kauli za Imam alizoziacha. Lakini huu ni mghafala mkubwa wa historia ya maimamu hawa, bali wa yaliyosemwa katika vitabu vyao. Kwani Abu Yusuf anasema rai ya Abu Hanifa katika kitabu *al-Kharaju* halafu anataja rai yake akieleza bayana kuwa yuko kinyume naye, na anabainisha sababu ya tofauti.

Na kama hivyo anafanya katika kitabu *Abu Hanifa* na *Ibn Abi Layla*. Kwani yeye mahala pengine huisema rai ya Ibnu Abi Layla baada ya kutaja rai mbili. Na Muhammad, Mungu amrehemu anaeleza katika kitabu chake kauli za imamu, kauli za Abu Yusuf na kauli zake, na anaeleza wazi tofauti iliyopo kati ya kauli hizo. Kwa kuwa lau (Abu Hanifa) angekuwa kama walivyosema, basi rai walizoziepuka zisingekuwa ndio madhehebu!

“Na, ni miongoni mwa yaliyothibiti kuwa Abu Yusuf na Muhmmad waliziacha rai alizokuwa nazo Imam, walipoona Hadithi walizonazo watu wa Hijazi. Lililo hakikiwa kihistoria ni kuwa maimamu wa kihanafi ambao tumewataja baada ya Abu Hanifa, rahimahu llahu, hawamfuati yeye.”16

Muhtasari ni kuwa: Madhehebu ya Hanafii yalipanuka na kuenea kwa juhudi za watu wake. Na walisaidiwa na nguvu za dola alizokuwa nazo Abu Yusuf.
Hivyo madhehebu ya Hanafii ni taasisi ya kundi la wanafaqihi, ambao kila mmoja akijitegemea mwenyewe wala haikutokana na imamu mmoja ambaye ni Abu Hanifa. Na hili jaribio la mahanafii, la kuyarejesha yote kwake ni jambo lisilo sawa.

## Kashfa Kwa Abu Hanifa:

Kulikuwa na wasiomshabikia ambao ni upande mwingine miongoni mwa wanachuoni waadilifu wa zama zake ambao walimsingizia Uzandiki, na kutokuwa makini, na walisema kuwa ni mtu aliyeharibikiwa kiitikadi na ana utovu wa nidhamu wa kidini, na yuko kinyume na Kitabu na Sunna, walimrarua katika dini yake, na kumvua imani.17

Walikusanyika Sufiyan At-Thauri, Shariiku, Hasan bin Swalihu na Ibnu Abi Layla, walituma kwa Abu Hanifa na wakasema: “Wasema nini kuhusu mtu aliyemuua baba yake na kumuingilia mama yake na akanywea pombe kichwa cha baba yake?”

Akasema: “Ni muumini.” Ibn Abi Layla akasema: “Sitokukubalia ushahidi abadan.” Na Sufianu At-Thauri alimwambia: “Sitosema na wewe abadan.”[18]

Na Ibrahimu bin Bishar alihadithia kutoka kwa Sufian bin Uyayna kuwa amesema: “Sijapata kumuona yeyote mwenye kuthubutu mno juu ya Mwenyezi Mungu kuliko Abu Hanifa.” Na pia kutoka kwake:

“Abu Hanifa alikuwa anaipigia mfano Hadithi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na kuiepusha kwa elimu yake.”[19]

Na imeelezwa kutoka kwa Abu Yusuf, aliulizwa: “Je Abu Hanifa alikuwa Marjaiy?” Alijibu: “Ndio.” Aliulzwa: “Alikuwa Jahamiy?” Alisema: “Ndio.” Aliulizwa: “Ukonaye vipi?” Akasema: “Abu Hanifa alikuwa mwalimu tu, hivyo basi endapo kauli yake itakuwa nzuri tutaikubali na endapo itakuwa mbaya tutamuachia.”[20]

Hii ndio rai ya waliokuwa karibu mno na yeye, mwanafunzi wake na muenezaji wa madhehebu yake, je itakuwaje rai ya watu wengine!

Na kutoka kwa al-Walid bin Muslim amesema: “Malik bin Anasi aliniambia: ‘Je Abu Hanifa hutajwa nchini kwenu?’ Nilimwambia: Ndio. Alisema: ‘Haipaswi nchi yenu kuwa makazi ya kuishi.”’[21]

Al-Awzaiy akasema: “Kwa hakika sisi hatumkemei Abu Hanifa kuwa na rai, kila mmoja wetu anayo rai, lakini sisi tunamkemea kwa sababu yeye humjia Hadithi kutoka kwa Nabii (s.a.w.w) anaigeuza vingine.”[22]

Amesema Ibn Abdil-Bari: “Na miongoni mwa waliomkashifu na kumuumbua ni, Muhammad bin Isma’il al-Bukhariy. Amesema katika kitabu chake *Ad-Dhuafaau Wal-Matrukuuna*: “Ni Abu Hanifa an- Nuuman bin Thabit al-Kufiy. Naim bin Hamad amesema: Alituhadithia Yahya bin Said na Muadhi bin Muadhi kuwa, tulimsikia Sufiani At- Thauriy anasema: Abu Hanifa alitakiwa afanye toba ya kuachana na ukafiri mara mbili. Na Naimu al-Fuzariy amesema: Nilikuwa kwa Sufiani Bin Uyayna, likaja tangazo la kifo cha Abu Hanifa, alisema….Alikuwa anaubomoa Uislamu tanzi moja baada ya lingine, hajazaliwa katika uislamu mtoto wa shari kuliko yeye. Haya ndio aliyoyasema al- Bukhariy.”[23]
Ibn al-Jaarud amesema katika kitabu chake *ad-Dhuafau Wal-Matrukuuna*: “Ni al-Nuuman bin Thabit, hadithi zake zote ni mawazo. Na imepokewa kutoka kwa Wakii bin al-Jarahi kuwa yeye amesema: ‘Nimemkuta Abu Hanifa amekhalifu Hadithi mia mbili kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu.’ Na aliambiwa Ibnu Mubaraka: ‘Watu walikuwa wanasema kuwa wewe unakwenda na kauli ya Abu Hanifa.’ Akasema: ‘Sio kila wasemalo watu ni kweli. Tulikuwa tukimwendea muda hali tukiwa hatumjui, lakini tulipomjua…..”[24]

Ni wazi kuwa kauli hizi zimetambulika kuwa ni za malengo, hivyo hazikuwa tusi au kebehi au kutoka nje ya mpaka wa kiakili bali hizo ni shaka za kielimu dhidi ya Abu Hanifa. Na hapa tumefumbia macho kero za maadui zake na kukithirisha kwa wafuasi wake, na tumetosheka na rai za wanavyuoni katika hilo, nayo yatosha kuutia dosari utu wake, vipi ilimfalia awe imamu, hali ikiwa katika umma kuna anayestahiki

zaidi yake yeye, kifiqhi, kielimu na kiuadilifu?! Lakini ni siasa, waijuaje siasa!

## Abu Hanifa Na Imam Ja'far As-Sadiq (A.S):

Alikuwa mfanya mjadala sana, mshindani hodari hivyo Mansur alitaka kumtumia kumpiga kumbo Imam as-Sadiq (a.s.) ambaye alikuwa anatajika kila mahali na umaarufu wake ukiwa umenyanyuka, na ilikuwa inamuia vigumu Mansur kuona Kufa, Makka, Madina na Qum duru za kielimu zinazoshabihiana na matawi ya madrasa ya Imam Ja'far bin Muhammad as-Sadiq (a.s.), kwa ajili hiyo Mansur alilazimika kumleta Imam (a.s.) kutoka Madina mpaka Kufa na alimtaka Abu Hanifa aandae mas'ala zilizo muhimu amuulize Imam (a.s.) katika kikao cha jumla ili amdhiki Imam Sadiq (a.s.) na kumpunguzia daraja yake.

Alisema: "Sijapata kumwona faqihi zaidi ya Ja'far bin Muhammad as- Sadiq. Mansur alipomleta alinitumia na akasema: 'Ewe kwa kweli watu wamefitiniwa na Ja'far bin Muhammad basi hebu muandaliye mas'ala magumu.' Nilimuandalia mas'ala arobaini.

"Halafu Abu Ja'far alinitumia mjumbe hali akiwa huko Hayra, nilimjia nikaingia kwake, na Ja'far bin Muhammad akiwa ameketi kuliani kwake, nilipomtia machoni, haiba ya Ja'far bin Muhammad as-Sadiq iliniingia kiasi ambacho haikuniingia haiba ya Abu Ja'far al-Mansur. Nilimtolea salamu, alinifanyia ishara nilikaa, halafu alimgeukia na akasema: 'Ewe Abu Abdillahi huyu ni Abu Hanifa.' Akasema: 'Naam, ametujia.' Kana kwamba amechukia ambayo husemwa na kaumu yake kumhusu kuwa yeye amuonapo mtu humjua.

"Halafu Mansur aligeukia kwangu na akasema: 'Ewe muulize Abu Abdillahi maswali yako.' Nikawa namuuliza naye ananijibu, anasema:

'Ninyi mnasema hivi na watu wa Madina wanasema hivi na sisi tunasema hivi, huenda tukafuata na huenda wakawafuata na huenda tukawakhalifu wote.' Mpaka nikaleta maswali arobaini. Kisha Abu Hanifa akasema: 'Si tumeeleza kuwa mwenye elimu zaidi ni mjuzi zaidi wa tofauti za watu."[25]

Imam as-Sadiq (a.s.) alikuwa anamkataza asikisie na alikuwa mkali kumkataza. Na alikuwa anasema: "Zimenifikia kuwa wewe unakisia dini kwa rai yako, usifanye hivyo kwa kuwa wa kwanza kukisia ni Ibilisi."[26]

Na alimwambia: "Ewe wasemaje kwa aliye katika hali ya ihramu aliyevunja *rubaiyyah*[27] ya mnyama swala?!" Akasema: "Ewe mwana wa Mtume wa Mwenyezi Mungu sijui hilo." Akasema: "Wewe unachanganyikiwa hujui kuwa swala hana rubaiyyah bali ni meno tu ya kawaida abadan."[28]
Abu Naim alituhadithia kuwa: "Abdullahi bin Ubayy Shibrima na Ibnu Abilayla waliingia kwa Ja'far bin Muhammad as-Sadiq, alimuuliza Ibnu Abilayla: 'Ni nani huyu aliye pamoja nawe?' Alisema: 'Huyu ni mtu ana uoni na sauti katika dini.' Akasema: 'Huenda anakisia jambo la dini kwa rai yake.' Akasema: 'Ndio.' Ja'far alimuuliza Abu Hanifa: 'Jina lako ni nani?' Akasema: 'Nuuman.' Akasema: 'Sioni kama unafanya vizuri kitu chochote.' Halafu akawa anamuuliza maswali ikawa jibu la Abu Hanifa ni kutokuwa na majibu yake. Ndipo Imam alipoyajibu.

“Halafu akasema: ‘Ewe Nuuman baba yangu alinihadithia kutoka kwa babu yangu kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema: Wa kwanza kukisia jambo la dini kwa rai yake ni Ibilisi. Mwenyezi Mungu (s.w.t.) alimwambia: Sujudu kwa ajili ya Adam. Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye, umeniumba mimi kutokana na moto na umemuumba yeye kutokana na udongo. Hivyo mwenye kukisia dini kwa rai yake Mwenyezi Mungu atamuunganisha na Ibilisi Siku ya Kiyama, kwa kuwa yeye ni miongoni mwa wafuasi wake katika kukisia.”’

Fakhru Raziy anasema: “La ajabu ni kuwa tegemeo lake lilikuwa kukisia na hali mahasimu wake wanamlaumu kwa sababu ya kukithiri kukisia. Wala haijanakiliwa kutoka kwake wala kwa mmoja miongoni mwa swahiba zake kuwa alitunga lau karatasi kuthibitisha ukisiaji. Wala hakuwahi kutaja katika mojawapo ya maandishi yake shubha yoyote, achia mbali hoja, wala hakujibu dalili za mahasimu wake katika kukanusha ukisiaji, bali wa kwanza aliyesema katika mas’ala hii na kuitolea dalili ni Shafii.”29

Kwa ajili hiyo tunamkuta Imamu as-Sadiq (a.s.) anauelekeza umma njia zilizo sahihi katika kuopoa hukumu za kisheria hasa baada ya kutapakaa ukisiaji na kuufanyia kazi kama chimbuko miongoni mwa chimbuko za uwekaji sheria.

Hivyo basi walihitimu kutoka madrasa yake maelfu ya wanavyuoni na mujtahidu. Miongoni mwao alikuwa ni Abu Hanifa ambaye alibakia naye muda wote wa miaka miwili aliyoishi Madina. Na kuhusu hilo husema: “Lau si miaka miwili angeangamia Nuuman.”

Na alikuwa hamsemeshi mwenye kikao ila kwa kauli: “Nimefanywa fidia yako ewe mwana wa binti ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).”30

Na Abdul Halim al-Jundiy anatoa maoni yake kuhusu Abu Hanifa kusoma kwa Imam as-Swadiq (a.s.): “Ikiwa utukufu wa Malik ni kuwa kwake miongoni mwa masheikh wakubwa wa Shafii au utukufu wa Shafii ni kuwa kwake mkubwa mno miongoni mwa maustadhi wa Ibnu Hanbali, au ni utukufu kwa wawili hao kusoma kwa masheikhe wao hawa. Basi kwa kweli uwanafunzi kwa Imam Swadiq umeivalisha utukufu fiqhi ya madhehebu manne ya Ahlus Sunna. Ama Imam as-Sadiq utukufu wake haukubali ziada au nuksani. Kwa kuwa Imam ni mubalighi kwa watu wote wa elimu ya babu yake alayhi swalatu wassalamu. Na Uimamu ni daraja yake, na maimamu wa kisunni kujifunza kwake ni utukufu kwao kwa kumkurubia mwenye daraja.”31

Ni kweli kabisa kuwa kuketi na Imam as-Swadiq (a.s.) ni utukufu wa kujifaharisha nao. Yeye ni mwanachuo wa Ahlul-Bayt, chimbuko la hekima. Ubora wake maadui wameutambua. Mansur amesema: “Huu mwiba – yaani Ja’far Sadiq – uliokwama shingoni kwangu ni mjuzi mno katika watu wa zama zake. Na yeye ni miongoni mwa wanaoiwania akhera sio dunia.”

Na suala hapa sio kuutambua ubora alionao, au kupata heshima ya kuketi pammoja naye basi, bali litakiwalo ni kumfuata na kutii amri yake kwa kuwa kumtii yeye ni faradhi kutoka kwa Mwenyezi Mungu juu ya kila mwislamu, kama ilivyothibiti kwa Hadithi ya Vizito Viwili: “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu,” na yasikitisha kuwa Abu Hanifa hakuwa miongoni mwa wanaosalimu amri yake, bali

alijitenga pekeyake anatoa fatwa kwa rai yake na kukisia katika dini, kwa ajili hiyo akienda kinyume na Hadithi za Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) ambazo hakuzikubali ila Hadithi kumi na saba...! Ninahitimisha maongezi haya kwa mjadala uliojiri kati ya Imam as-Sadiq (a.s.) na Abu Hanifa, pindi alipokuja kwake:

*As-Sadiq (a.s.)*: Wewe ni nani?
*Abu Hanifa*: Abu Hanifa.

*As-Sadiq (a.s.)*: Ni mufti wa watu wa Iraqi?
*Abu Hanifa*: Ndio.
*As-Sadiq (a.s.)*: Kwa kitu gani unawatolea fatwa?
*Abu Hanifa*: Kwa kitabu cha Mwenyezi Mungu.

As-Sadiq (a.s.): Hivi wewe ni mjuzi wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu? Waijua *nasikhu* na *mansukhu* zake? Aya Muhkamu na *mutashabihu* zake?
Abu Hanifa: Ndio.

*As-Sadiq (a.s.)*: Nipe habari kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu “**Na tukapima humo safari, nendeni usiku na mchana kwa amani.**” (***Surat Sabaa*: 18**) ni mahali gani hapo?

*Abu Hanifa*: Hapo ni kati ya Makka na Madina.

Imam aligeuka kulia kushoto: “Namuapa Mwenyezi Mungu, je mnakwenda kati ya Makka na Madina na hampo katika amani ya damu zenu kwa kuuwawa? Na kuibiwa mali zenu?” Kwa sauti moja waliohudhuria wakasema: “Ewe Mungu wangu, ndio.”

Mara hii Imam (a.s.) aligeuka kumuelekea Abu Hanifa: “Ole wako ewe Abu Hanifa! Kwa kweli Mwenyezi Mungu hasemi ila ukweli.”

Alinyamaza dakika kadhaa, halafu alibadilisha kauli yake ya mwanzo, akasema: “Sina elimu ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu.” Hapo alileta epusho jipya: “Mimi ni mtu wa ukisiaji tu.”

Imam (a.s.) akasema: Angalia katika ukisiaji wako, ikiwa ni mkisiaji. Ni ipi mbaya zaidi kwa Mwenyezi Mungu: Kuuwa au kuzini?

*Abu Hanifa*: Ni kuuwa.
*As-Sadiq*: Vipi ameridhia katika kuuwa mashahidi wawili wala hakuridhika katika kuzini ila wanne? Lafanyiwa ukisiaji hili kwako?
*Abu Hanifa*: Hapana.
*As-Sadiq*: Vyema. Je swala ndiyo bora au Swaumu?
*Abu Hanifa*: Swala ndio bora.
*As-Sadiq*: Hivyo basi kulingana na kauli yako itakuwa wajibu juu ya mwenye hedhi alipe Swala zilizomfutu katika siku zake za hedhi. Si Swaumu. Na hali Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amewajibisha juu

yake alipe Swaumu sio Swala.

*As-Sadiq*: Je mkojo ndio mchafu zaidi au manii?
*Abu Hanifa*: Mkojo mchafu zaidi.
*As-Sadiq*: Hivyo kulingana na ukisiaji wako itakuwa wajibu kuoga, kwa sababu ya mkojo, na si manii, na hali Mwenyezi Mungu Mtukufu amewajibisha kuoga kwa kutokwa na manii wala si mkojo. Je hili lafanyiwa ukisiaji kwako?

Alinyamaza, na akasema: "Mimi ni mtu wa rai tu." Haraka sana Imam alimuuliza: "Nini rai yako kuhusu mtu ambaye alikuwa na mtumwa, alioa na akamuolea mtumwa wake mke usiku mmoja. Na wakawaingilia wake zao usiku mmoja, wakawaweka wake zao katika chumba kimoja kisha wakasafiri, na wale wanawake wakazaa watoto wawili wa kiume. Halafu kile chumba kikawabomokea wale wanawake wawili, wao wakafariki lakini watoto wakabaki hai. Ni yupi kulingana na rai yako atakuwa mmiliki na yupi atakuwa mmilikiwa? Na yupi kati ya wawili hao mrithi na yupi mrithiwa?"

Kwa mara ya tatu, alibadili msimamo wa kauli yake kuwa ni mtu wa rai, na alitangaza baada ya muda wa ukimya, kufikiri, kuduwaa, na aibu: "Mimi ni mtu wa hadi za kisheria." Imam (a.s.) akasema: "Waonaje kuhusu kipofu amepofoa jicho la mtu aliyekuwa mzima, na aliyekatika mikono amekikata kipande cha mkono wa mtu. Vipi itatekelezwa hadi ya kisheria juu ya wawili hawa?"

Alijaribu kujibu maswali ya Imam ili apate kuhalalisha uandikaji nne wake juu ya kiti cha enzi cha fatwa huko Iraq, lakini alishindwa kisha kwa masikitiko akasema: "Sina elimu…sina elimu…... Lau sio watu kusema kwamba ameingia kwa mwana wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na wala hakumuuliza kitu, mimi nisingekuuliza kitu.

*As-Sadiq*: Hivyo basi fanya ukisiaji ikiwa ni mkisiaji.
*Abu Hanifa*: La, sitoongea kwa rai na ukisiaji katika dini ya Mwenyezi Mungu baada ya kikao hiki.

Lakini Imam (a.s.) alitabasamu akisema: "Hapana… hapana, kwa kusema kweli kupenda ukubwa hakutokuacha wewe kama hakujawaacha waliokuwa kabla yako."

## Imam Malik Bin Anas

Yeye ni Abu Abdillahi, Malik bin Anas. Alizaliwa Madina mwaka 93 A.H. kulingana na baadhi ya kauli, na alifariki mwaka 179 A.H. kulingana na kauli mojawapo. Wakati wa Malik uling'ara kwa elimu, na Madina siku hizo ilijaa wanafunzi kutoka nchi tofauti za kiislam, na madrasa ya Madina ilijulikana kwa kushikamana na Hadithi na kuipiga vita madrasa ya rai ya huko Kufa iliyokuwa chini ya uongozi wa Abu Hanifa, ni miongoni mwa yaliyozua mfarakano kati ya madrasa mbili hizo na mabishano yaliyotoka nje ya mpaka wa kielimu.

Na changamoto ya madrasa hii ilikuwa ni madrasa ya Imam as-Sadiq (a.s.) ambayo ilikuwa imejaa wanachuoni na mikusanyiko ya misafara kutoka pande mbalimbali za dunia ya kiislamu, ambao

walikuwa wanagawana fursa ya kukutana na maimamu wa Ahlul-Bayt (a.s.), na Imam as-Sadiq (a.s.) alikuwa na nafuu kidogo ya ukandamizaji wa watawala, ukimlinganisha na maimamu wengine wa Ahlul-Bayt. Na Malik alijiunga na madrasa yake muda mrefu na alichukua Hadithi kutoka kwake. Na anazingatiwa kuwa ni miongoni mwa masheikh wakubwa wa Malik.

Halafu Malik alisoma kwa idadi kadhaa ya masheikh. Mfano wa Amiru bin Abdillah bin Zubair bin al-Awwam, na Zayd bin Aslam na Said al-Maqbariy na Abu Hazim, na Swafwan bin Salim na wengine. Na Malik alikuwa makhsusi kwa kujiambatanisha na kuchukua kutoka kwa Wahbi bin Hurmuz, na Nafiu huria wa Ibnu Umar, na Ibnu Shihabi az-Zuhriy, na Rabiatu ar-Raayi, na Abu Zanad.

Malik aliendelea mpaka alichukua ukuu wa madrasa ya Hadithi, lakini haraka sana siasa ilijiingiza, ili iinusuru madrasa ya rai, na wakasirishwe watu wa Hadithi, na kwa ajili hiyo Malik bin Anas alikuwa lengo la ukandamizaji wa dola mpaka walifikia kumzuia kuelezea Hadithi, na alipigwa mjeledi kwa sababu ya fatwa aliyoitoa isiyokubaliana na utashi wa dola, na hilo lilikuwa zama za uliwali wa Ja'far bin Sulayman, mwaka wa 146A.H. Kwa kweli yeye alimvua Malik na kumnyoosha na kumcharaza kwa mijeledi mpaka mabega yake yaling'oka.

Ibrahim bin Hammad akasema: "Nilikuwa namwangalia Malik aliposimamishwa kutoka kikazi chake, mkono wake wa kulia au wa kushoto ulibebeshwa juu ya mwingine."

Na ni miongoni mwa ajabu na lenye kusisimua sana ni kuwa baada ya zama kidogo, Malik alikuwa anawekwa mbele katika dola, mwenye kutiliwa maanani, na alifikia daraja ambayo kwayo watawala walikuwa wanamwogopa. Swali ambalo lenyewe linakuja, ni kitu gani kimepatikana kwa Malik mpaka dola imridhiye na imnyanyue mpaka daraja hii? Hivi ni kuwa dola ilikuwa yamchukia kwa rai maalumu ambayo sasa Malik ameachana nayo? Au alibakia thabiti katika rai yake na dola ikaichukua na kuacha msimamo wake kwa ajili ya Malik? Au kuna kitu kingine?

Swali hili linaloduaza, na ulizo linalojitokeza mbele ya anayeidurusu historia ya imamu Malik, ataona kubadilika kwa uhusiano kati yake na dola, kutoka hali ya kukandamizwa na ghadhabu mpaka kufikia Malik na Mansur wanapendana na kusifiana. Hivyo basi Mansur anamwambia Malik: "Wallahi wewe ni kati ya watu wachache na umjuzi mno, ukipenda nitaiandika kauli yako kama misahafu inavyoandikwa, na nitaituma pande mbali mbali za nchi na nitawalazimsha nayo."

Kutokea hapo madhehebu ya Imam Malik ilianza kuenea alipokuwa aridhiwa na Sulutani. Vinginevyo kwa kweli mas'ala sio elimu na kutokuwa na elimu bali ni ya ufalme na usulutani, kujigamba, na kujitangaza. Na watu kuchukuliwa wakiwa wanaridhia au kwa kahari kuifuata madhehebu. Na hili ndilo ambalo limemfanya Rabiatu ar-Raayi -Ustadhi wa Malik na mwenye elimu nyingi kuliko yeye - aseme: "Hamjui kuwa uzito wa dola ni bora kuliko mzigo wa elimu."32

Na Malik alipopata ridhaa hii kutoka kwa Sulutani akawa anasema: "Nimemkuta Mansur mjuzi mno wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake na athari za waliotangulia."

Subhanallah! Ni elimu gani aliyonayo Mansur kiasi awe ni mjuzi mno katika watu wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake (s.a.w.w)?! Si chochote bali ni kujikurubisha na kujisogeza kwa mfalme na Sultani.

Ama dalili ya kuwa Malik alikuwa amejitenga mbali na Sultani, hiyo historia haijatuhadithia kuwa alithubutu kusimama mbele ya Mansur, akimpinga jambo au kuipinga njia yake, kama alivyofanya Abdullahi bin Marzuq alipokutana na Abu Ja'far katika tawafu, hali watu wamejitenga kumpisha. Abdullahi akasema kumhusu: "Ni nani amekufanya uwe na haki zaidi ya nyumba hii kuliko watu, unawazuia kati ya nyumba na wao, na unawaweka kando nayo?!" Abu Ja'far alimwangalia usoni kwake na alimtambua, na akasema: "Ewe Abdullah bin Marzuq, nani amekufanya uthubutu kufanya hili, na nani amekutanguliza mbele ya hili"?

Abdullah akasema: "Utanifanya nini? Je mkononi mwako muna madhara au manufaa? Wallahi siogopi madhara yako wala sitarajii manufaa kwako, mpaka Mwenyezi Mungu awe amekuidhinisha kwangu."

Mansur akasema: "Kwa hakika wewe umeihalalishia nafsi yako na umeiangamiza." Abdullahi akasema: "Allahuma ikiwa mkononi mwa Abu Ja'far kuna la kunidhuru, usiache chochote katika madhara ila kiteremshe juu yangu, na ikiwa mkononi mwake kuna manufaa yangu, yakate manufaa yote kutoka kwake, wewe ewe Mola wangu mkononi mwako mna kila kitu na wewe ni mmiliki wa kila kitu." Hapo Abu Ja'far alitoa amri kumhusu, alimchukua mpaka Baghdad alimuweka jela huko halafu alimfungua.33

Kwa minajili hiyo twamwona Malik yuko mbali na Imam Ja'far as-Sadiq (a.s.) kwa kuwa yeye haafikiani na rai zake za kujiepusha mbali na Sultani na kuwa mbali naye.

Mimi kwa mtazamo wangu ni kuwa sababu ya msingi ya utawala kumghadhibikia Malik hapo mwanzo ni kuwa uliona upendo kwa Imam as-Sadiq (a.s.), na tuhuma iliyokuwa yazunguka wakati ule ni kuwa Waarabu wanataka kufanya mageuzi kwa ajili ya Ahlul-Bayt, ndio maana tunaona utawala uliwasogeza karibu vipenzi vyao na ulimnusuru Abu Hanifa huko Kufa. Na jambo hili lilipotoweka, utawala haukupata njia ila kuing'arisha shakhsia ya Malik na kumweka kama mfano wa kidini kwa dola, ili ithibiti kwa watu jina la dola ya kiislamu, na hasa ukizingatia kuwa Abasiyina waliwaasi Amawiyina kwa hoja ya kuwa wao wako mbali na dini.

Kwa ajili hii tunakuta amri ya mfalme ilinena waziwazi uaminifu wa Malik usiozoeleka kwa mwanachuoni yoyote hapo kabla: "Ikikuingia shaka kutoka kwa liwali wa Madina au liwali wa Makka au kutoka kwa yeyote miongoni mwa maliwali wa Hijazi, aidha kuhusu dhati yako au ya mtu mwingine, au uovu au shari kwa raia yoyote, niandikie nitawashushia wanayoyastahiki."

Kutokana na hali hiyo daraja ya Malik ilitukuka, wakawa maliwali wanamwogopa sawa sawa na kama wamwogopavyo Mansur. Kama alivyohadithia Shafii alipofika Madina akiwa na barua ya liwali wa Madina kutoka kwa liwali wa Makka, na alikuwa ataka aifikishe kwa Malik.

Liwali akasema: "Ewe kijana kwa hakika kutembea kwa mguu kutoka ndani ya mji wa Madina mpaka

ndani ya Makka bila viatu, ni rahisi mno kwangu kuliko kwenda kwenye mlango wa Malik, sioni udhalili ila nisimamapo mbele ya mlango wa nyumba yake."34

Na alipokuja al-Mahdi baada ya Mansur nafasi ya Malik ilizidi kutukuka na alizidi kuusogelea utawala, al-Mahdi alikuwa anamtukuza na kumheshimu na kumpa zawadi kubwa kubwa na kumpa mengi na kuwadhihirishia watu hali yake na daraja yake ya juu.

Na alipokuja ar-Rashid hakubadilisha akamhifadhia Malik nafasi na alimtukuza upeo wa kumtukuza, hivyo haiba ya Malik iliingia nyoyoni. Ndivyo siasa ilivyo, wamuinua umpendae kumwinua, na unaisahaulisha kumbukumbu ya umtakiaye hivyo. Baada ya hivyo ni pingamizi gani itazuia kuenea kwa madhehebu ya Malik baada ya kuwa aridhiwa na dola?!

Wako ni Mwenyezi Mungu ewe bwana wangu Ja'far bin Muhammad as- Sadiq (a.s.), wanatambua kuwa haki ni yako na ipo kwako, wala uimamu hauwi jaizi kwa asiyekuwa wewe.

Je Malik hakusema: "Jicho langu halijapata kuona wala sikio kusikia, wala kuingia katika moyo wa mwanadamu aliye bora kuliko Ja'far as-Sadiq, kiubora kielimu, kiibada na kiuchaji Mungu."35

Pamoja na kudhihiri fadhila zake, hakupata (a.s.) na Shia wake ila kukandamizwa, kutishwa, mauaji na kufurushwa, na linalotoa ushahidi wa hayo ni historia ya Shia, tokea kutawafu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) na muda wote wa historia yao.

Lakini mimi najiuliza kama anavyojiuliza mwandishi wa kitabu *al-Imam Sadiq Mualimul-Insani* aliposema: "Kwa hakika mimi sijiulizi kwa nini waislamu wameendelea kuchanika na kuwa Sunni na Shia? Hapana. Isipokuwa najiuliza na kuduwazwa: Vipi Shia wameweza kubaki imara mpaka hii leo! Japokuwa kulikuwa na hali ya mambo yenye kukandamiza, na hali ngumu walioipita katika kivuli cha vitisho vya kifikra na vya kimwili?!. na japokuwa kulikuwa na majaribio mengi ya kufutilia mbali ishara za ukweli na kuurarua uislam?!"36

Kama sivyo, je! Sio miongoni mwa dhuluma kuitanguliza kila madhehebu mbele ya madhehebu ya Ja'far bin Muhammad as-Sadiq?! Bali yasikitisha mno kuwa si mashuhuri mpaka hii leo hata kati ya wasomi miongoni mwa tabaka za jamii.

Nakumbuka siku moja, mwalimu wetu huko chuo kikuu alikuwa anatusomesha fiqhi ya Malik, hivyo kundi la wanafunzi lilimpinga wakisema: Kwa nini hautusomeshi fiqhi ya madhehebu manne?! Alisema: "Mimi ni Mmaliki, na Wasudani wote ni Mamaliki, na ambaye si Mmaliki miongoni mwenu mimi nipo tayari kumsomesha madhehebu yake kwa sura mahsusi."

Nilimwambia: Mimi sio Mmaliki je utanisomesha madhehebu yangu? Alisema: "Ndio, madhehebu yako ni madhhebu gani? Je wewe ni Shafii?" Nilimwambia: Hapana. Akasema: "Je wewe ni Hanafi?" Nikamwambia: Hapana. Akauliza: "Je wewe ni Hanbali?" Nilimwambia: La. Hapo mshangao na kuchanganyikiwa kulijitokeza usoni kwake, na akasema: "Hivyo basi wamfuata nani?!" Nikasema: Ja'far

bin Muhammad as-Sadiq (a.s.). Akasema: "Ja'far ni nani?!"

Nilisema: Ni Ustadhi wa Malik na yeye ni miongoni mwa dhuria wa Ahlul-Bayt, madhehebu yake yalikuwa mashuhuri kwa jina la madhehebu ya Ja'fariyah. "Alisema sijapata kusikia madhehebu hii hapo kabla." Nilisema: Sisi ni Shia. Alisema: "Najikinga kwa Mwenyezi Mungu dhidi ya Shia." Na alitoka....!

Hivyo basi mwenye kuwa na hadhi, kujitangaza na mamlaka atafika kilele cha juu zaidi. Kwani Malik mwenyewe hakuwa na tamaa ya daraja hii kwa kuwa yeye alikuwa anajua kuna wengi wanaofaa zaidi kwa ajili ya nafasi hii kuliko yeye, lakini utawala wamtaka yeye awe marejeo ya watu wote katika fatwa. Mansur alimwamuru aweke kitabu awalazimishe watu kwacho kwa kahari, Malik alikataa, ndipo Mansur akasema: "Weka – yaani kitabu – hakuna yeyote hii leo mjuzi zaidi kuliko wewe."[37] Akaweka kitabu *al-Muwatau*, na mpiga mbiu wa Sultani alinadi siku za Hijja kuwa: "Yeyote asitoe fatwa isipokuwa Malik."

## Kuenea Kwa Madhehebu Ya Malik:

Madhehebu ya Malik ilienea kwa njia ya makadhi na wafalme, hivyo basi katika nchi ya Hispania mfalme wake aliwalazimisha watu kuyafuata madhehebu ya Malik, hiyo ni pindi yalipomfika maneno ya kumsifu kutoka kwa Malik alipoulizwa kuhusu sera ya mfalme katika Uhispania, alitaja sifa zilizompendeza kumhusu, akasema: "Tunamuomba Mwenyezi Mungu (s.w.t.) alipambe eneo letu takatifu kwa mfalme wenu." Kauli yake ilipofika kwa mfalme aliwabebesha watu madhehebu yake, na aliyatupilia mbali madhehebu ya Al-Awzaiy, na watu walimfuata kutii mamlaka yake, kwani watu wako pamoja na dini za wafalme wao.

Na pia madhehebu ya Malik yalienea Afrika kwa njia ya Kadhi Sahnoun. Miqriziy anasema: "Na al-Maaziy bin Baadiys aliposhika uliwali aliwalazimisha watu wa Afrika kushikamana na madhehebu ya Malik na kuacha yasiyokuwa yake. Kwa hiyo watu wa Uhispania na wa Afrika wote walifanya rejea kwenye madhehebu yake, wakitaka kilicho kwa Sultani na pupa ya kuitaka dunia, kwa sababu ukadhi na utoaji fatwa katika miji yote hiyo hauwezi kuwa ila kwa anayejiita madhehebu ya Malik.

Hivyo basi watu wa kawaida wakadharurika kupata hukumu zao na fatwa zao. Hivyo ikatapakaa madhehebu hii huko, na ikapata hadhi ya kukubaliwa, si kwa sababu ya kustahiki kwake na unyofu wake kiroho. Bali yalienda tu kulingana na nidhamu ya mabavu ambayo watu walilazimika kuitii bila ya uangalifu."[38]

Hivyo hivyo ilienea huko Moroko alipotawala Ali bin Yusuf bin Tashifayni, katika dola ya Bani Tashifayni, aliwatukuza wanachuoni na kuwasogeza karibu. Na ilikuwa hamsogezi karibu ila mwanachuoni wa madhehebu ya Malik, hivyo watu walishindana kuyapata madhehebu ya Malik, vitabu vya madhehebu ya Malik vilipata soko na watu walivitendea kazi na kuviacha visivyokuwa vya madhehebu ya Malik, mpaka hima ya watu kukielekea kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Nabii wake ilipungua.

Ni kama hivyo, siasa iliichezea dini ya waislamu ikawa siasa ndiyo yenye kauli katika itikadi zao na kuziendesha ibada zao. Hivyo basi watu walirithi madhehebu zilizolazimishwa na waliyapokea bila ya

mjadala au kuhoji. Na ilikuwa yapendeza kila kizazi kiwe huru kulijua hilo na kisifanye ufuasi, yaani kisiige na kutii utii wa kipofu kumtii mwenye uoni.

Ibnu Hazmi amenena: “Madhehebu mbili zimeenea mwanzoni mwa suala lao kwa utawala na mamlaka: Madhehebu ya Abu Hanifa, kwa kuwa Abu Yusufu alipotawalia ukadhi alikuwa hamtawalishi Kadhi isipokuwa kutoka swahiba zake wenye kujiunga na yeye na madhehebu yake.

“Pili: Madhehebu ya Malik tuliyonayo Uhispania, kwa kuwa Yahya bin Yahya alikuwa na sauti kwa Sultani mwenye kukubaliwa katika ukadhi. Alikuwa hamtawalishi Kadhi katika miji ya Uhispania ila kwa ushauri wake na uchaguzi wake, wala haendi ila na maswahiba wake, na watu ni wenye haraka kuielekea dunia, wakaelekea wanakotarajia kufikia malengo yao.”[39]

## Kebehi Kwa Maliki

### Kashfa Juu Ya Malik:

Hapa zimekithiri kauli za wenye kumpendelea, na nimeacha fadhila walizonazo, ambazo Mwenyezi Mungu hajateremsha ufalme wowote juu yake, kwa kuwa zenyewe sio kipimo halisi cha kujua shakhsia ya Malik, na miongoni mwa mifano hiyo yakujia: Kwa hakika al-Qaysiy alimuona Nabii (s.a.w.w) akitembea njiani na Abu Bakr nyuma yake, na Umar nyuma ya Abu Bakr na Malik bin Anas nyuma ya Umar na Sahnoun[40] nyuma ya Malik.[41]

Na mamia mfano wake, nayo ni mambo yasiyo na maana na ni fadhila za kutengenezwa hazifai kujadiliwa.

Na hapa nimetosheka na maneno ya wanachuoni na ya baadhi waliokuwa katika zama moja na Malik, nazo ni rai huru si zaidi ya vile achukuliwavyo mtu kielimu.

Shafii amesema: “Liithu ni mtaalamu zaidi kuliko Malik, ila tu swahiba zake hawakutendea kazi taaluma yake. Na Said bin Ayyub amesema: Lau Liithu na Malik wangekutana Malik angekuwa bubu mbele ya Liithu na Liithu angemuuza Malik kwa amtakaye.”[42]

Ali bin Madiiniy alimuliza Yahya bin Said: “Ni rai ya yupi mmojawapo yakupendeza mno, ya Malik au rai ya Sufyan?” Akasema: “Rai ya Sufyani haina shaka katika hili.” Na akasema: “Sufyan ni zaidi ya Malik katika kila kitu.”

Na Yahya bin Muiin akasema: “Nimemsikia Yahya bin Said akisema: Sufyan anipendeza mno kuliko Malik katika kila kitu.”[43]

Na Sufyani Thauriy akasema: “Hana uwezo wa kuhifadhi - yaani Malik.” Na amesema Ibnu Abdul-Bari: “Ibnu Dhuaibi alinena kumhusu Malik bin Anas maneno makavu yenye kukwaruza, nimeona vibaya kuyataja.”[44]

Na alinena kumhusu Malik, Ibrahim bin Sa'ad na alikuwa akimwombea dua mbaya, na pia alinena kumhusu Malik Abdur Rahman bin Zayd bin Aslam, Ibnu Abu Yahya, Muhammad bin Is'haqa al-Waqidiy, na Ibnu Abu Zinad, na walikebehi vitu katika madhehebu yake. Na Salmatu bin Sulayman alimwambia Ibnu Mubarak: "Umeweka kitu katika rai ya Abu Hanifa na kwa nini haujaweka katika rai ya Malik?" Alisema: "Sikumuona yu mwanachuoni."45

Na amesema Ibnu Abdil-Bar kumuhusu Malik: "Kwa kweli wao wamevitia dosari vitu katika madhehebu yake. Na kutoka kwa Abdillahi bin Idrisa amesema: 'Alikuja kwetu Muhammad bin Is'haq tulimwambia kitu kuhusu Malik, na akasema: Leteni elimu yake. Na Yahya bin Swalih akasema: Ibnu Akthum aliniambia: Umemuona Malik na umesikia kutoka kwake na umekuwa pamoja na Muhammad bin al-Hasan ni yupi alikuwa na elimu zaidi? Nilisema: Muhammad bin al-Hasan anavyojichukua binafsi ni mwanachuoni zaidi kuliko Malik."46

Na Abu Muhammad bin Abu Hatmi alikuwa akisema: "Kutoka kwa Abu Zar'a kutoka kwa Yahya bin Bakir kuwa yeye alisema: 'Liithu ni mwanachuo zaidi kuliko Malik ila tu hadhi ilikuwa ni ya Malik."47
Na Amesema Ahmad bin Hanbal: "Ibnu Abu Dhuaybi anashabihiana na Said bin Al-Musayab, na alikuwa bora kuliko Malik, ila Malik watu wanamtakasa zaidi kuliko yeye."48

Kutokana na maneno yote haya tunaweza kusema kuwa: Malik hana ubora zaidi ya mwingine miongoni mwa wanachuoni, na wala hana kinachompambanua na kumfanya awe anastahiki kuwa marejeo ya kifiqhi, lakini siasa haiangalii mahali stahiki, yenyewe ina kipimo chake mahsusi inakitumia kwa misingi ya vipimo vyake vya kisiasa na maslahi yake. Hivyo basi mwanafiqhi ambaye hapingani na siasa yake ndiye faqihi ambaye wajibu juu ya waislamu kumfanya kigezo na kufuata mfano wake.

## Imamu Shafii

Yeye ni Abu Abdillahi Muhammad bin Idrisa bin Al-Abbas bin Uthman bin Shafii. Alizaliwa mwaka 150 A.H. Na kuna kauli isemayo kuwa ni siku ambayo alikufa. Na kuna tofauti kuhusu mahali alipozaliwa kati ya Ghaza, Asqalani na Yemen, na kauli isiyo ya kawaida iliyotupiliwa mbali ni Makka. Na alikufa Misri mwaka 204 A.H.

Alihama akiwa na mama yake naye akiwa mdogo kwenda Makka. Na humo alijiunga na chuo cha Qur'ani na alihifadhi Qur'ani tukufu, na alijifundisha kuandika na baada yake alitoka kwenda Badiyah na aliambatana na Hudhaylu akiwa na miaka ishirini kulingana na alivyohadithia Ibnu Kathiir katika *al-Bidaya Wan-Nihayah,* na miaka kumi na saba kama alivyohadithia yeye mwenyewe katika *Muujamul-Buldaan*. Hivyo aliupata ufasaha wa Hudhaylu, na katika muda huu wote Shafii hakuwa na mwelekeo wa kielimu na kifiqhi kwa kuwa hakuelekewa ila katika kumi la tatu la umri wake. Na ikiwa kubakia kwake Badiyah ni miaka ishirini basi utafutaji wake wa fiqhi ni katika kumi la nne, yaani baada ya kuivuka kwake miaka thelathini.

Shafii amejifunza kwa masheikh wa Makka, Madina, Yemen na Baghdad, na wa kwanza ambaye kutoka

kwake Shafii amepata elimu ni Muslim bin Khalid al-Makhzumiy aliyekuwa maarufu kwa jina la az-Zanjiy, na alikuwa sio miongoni mwa wanaotegemewa katika Hadithi. Wamemzingatia kuwa ni dhaifu na wamemkebehi mahafidhu wengi kama Abu Daudi na Abu Hatim na Nasaiy.49

Halafu alisoma kwa Said bin Salum al-Qudahi, na alituhumiwa kuwa ni miongoni mwa *Murjiah*. Na alichukua kutoka kwa Sufyani bin Uyaina, mwanafunzi wa Imam as-Sadiq (a.s.), naye ni moja miongoni mwa madhehebu zilizotoweka. Kama ambapo amechukua elimu kutoka kwa Malik bin Anas huko Madina. Na kutoka kwa wengine, Ibnu Hajar amewataja themanini miongoni mwao, na humo kuna aina ya kutia chumvi. Na Raziy kwa chuki binafsi amekanusha madai ya kuwa Shafii amechukua elimu kutoka kwa Muhammad bin al-Hasan Shiibaniy, aliyekuwa Kadhi na mwanafunzi wa Abu Hanifa, lakini utashi wake binafsi hauna nafasi, kwani Shafii mwenyewe amekiri kuchukuwa elimu kutoka kwake.

Ama wanafunzi wa Shafii miongoni mwao kuna ambaye ni Mwiraki na miongoni mwao kuna ambaye ni Mmisri. Na hapo baadaye walitengeneza sababu ya misingi ya kusambaa kwa madhehebu yake. Katika Wairaki ni Khalidu al-Yamaniy al-Kalbiy Abu Thauri al-Baghdady ambaye anahesabika kuwa ni mwenye madhehebu ya pekee, alikuwa na watu wanaomfuata mpaka karne ya pili. Na amefariki mwaka 240 A.H.

Wengine ni al-Hasan bin Muhammad bin Swabah az-Zaafaraniy, al-Hasan bin Ali al-Karabisiy, Ahmad bin Abdul-Azizi al-Baghdady, na Abu Abdur Rahman Ahmad bin Muhammad al-Ash'ariy. Huyu alikuwa anashabihiana na Shafii na anasifika naye, kwa sababu yeye ni nusra ya madhehebu na aliwahami swahiba zake kwa sababu ya nafasi aliyokuwa nayo kwa Sultani na daraja yake kuwa juu katika dola, kwa hiyo yeye alikuwa na jaha kubwa mno.

Na miongoni mwa wanafunzi wake ni Ahmad bin Hanbal, japo mahanbali wajigambe kuwa Shafii alikuwa anasema Hadithi kutoka kwa Ahmad na kuwa alisoma kwake kama ilivyokuja katika *Tabaqatul-Hanabila*.
Ama wanafunzi wake Misri, walikuwa na taathira zaidi ya kusambaza madhehebu yake, na kutunga vitabu na aliye mashuhuri miongoni mwao ni, Yusuf bin Ya'aqub al-Buwaytiy, naye ni khalifa wa Shafii katika darasa na ni miongoni mwa walinganiaji wake wakubwa. Alikuwa anawaleta karibu wageni na kuwatambulisha fadhila za Shafii mpaka walikithiri wafuasi wake na kusambaa madhehebu yake, kwa minajili hiyo Ibnu Abu Liith al-Hanafiy alimhusudu na alimtoa Misri, kwa hiyo alifariki akiwa jela huko Baghdad.

Na miongoni mwa wanafunzi wake ni Ismail bin Yahya al-Mazniy, Abu Ibrahim al-Misriy, na anazo tunzi kuihusu madhehebu ya Shafii zilizosaidia kuisambaza madhehebu, mfano wa hizo ni *Al-Jamiul-Kabiir, Al-Jamius-Swaghir*, na *Al-Manthuur....*

Na mwenye kuisoma historia ya Shafii atakuta wanafunzi wake na swahiba zake ndio ambao walimuunga mkono kumtilia nguvu na kuyasambaza madhehebu yake.

Na kuna tofauti kati ya madrasa ya Shafii huko Irak na madrasa yake huko Misri, yahitaji kuzingatia.

Imejulikana kutoka kwa Shafii kuwa alibadilisha fatwa zake za Irak, na ilitambulika kuwa ni madhehebu ya zamani, nayo ndiyo waliyoichukua wanafunzi wake huko Irak. Na miongoni mwa vitabu vya madhehebu ya zamani ni *al-Aamaliy* na *Majmaul-Kaafiy*. Alipohama kwenda Misri aliharamisha kuyatendea kazi madhehebu yake ya zamani baada ya kusambaa kwa watu wa kawaida na wao kuyatendea kazi. Je aliyaacha kwa kuwa yalikuwa batili?! Au ni kuwa ijitihadi yake ilikuwa pungufu huko Baghdad na ilikamilika Misri?!

Kisha kuna uthibitisho gani wa kusihi kwa madhehebu yake mapya Misri?! Na je lau umri ukimuwia mrefu atayaacha?! Kwa minajili hiyo tunakuta kauli mbili katika mas'ala moja katika fiqhi ya Shafii, kama ilivyokuja katika kitabu *al-Ummu*. Na huenda kukazingatiwa kutaradadi huku na tofauti kwatokana na kutokuwa na uamuzi wa kukata shauri, nao ni upungufu katika ijtihadi na elimu.

Maana hii imetiliwa nguvu na kauli ya al-Bazzazu: "Huko Irak Shafii alikuwa anatunga vitabu huku swahiba wa Muhammad – yaani As- Shiibaniy – wakikithirisha kauli zake (As-Shaiibaniy) kwa hoja na wanazidhaifisha kauli zake (Shafii), kwa kweli walimfanya dhaifu, na wanahadithi hawazitilii maanani kauli zake. Na wanamtuhumu kwa kuwa *Muutazila*, na lilipokosekana soko huko Irak kwa ajili yake, alitoka na kwenda Misri.

Na huko hakukuwa na faqihi maalumu kwa hiyo kwake ikawa huko ni soko."[50]

Hali hii ilikuwa tofauti alipohamia Misri, kwa kuwa Shafii alijulikana kuwa ni mwanafunzi wa Malik na ni mnusuru wa madhehebu yake na mlizi wake. Na hili ndilo jambo ambalo lililomuandalia ufanisi Misri, hiyo ni kwa sababu hali ya mambo kwa jumla ilikuwa ni ya kimalik, kuongezea kuwa yeye alifika Misri kwa usia wa Khalifa wa wakati ule kwa amiri wa Misri, kwa hiyo alikuta utiliwaji maanani wa kutosha katika Misri, khususan kutoka kwa swahiba wa Malik, baada ya hapo alianza kueneza madhehebu yake mapya.

Lakini Shafii hakuchukua muda mwingi mara alianza kutunga vitabu vya kumjibu Malik na kuzipinga kauli zake. Na kuhusu hilo Rabiu anasema: "Nimemsikia Shafii akisema: 'Nilifika Misri na nilikuwa sijui kuwa Malik anapingana na baadhi ya hadithi ila Hadithi kumi na sita tu, nikaangalia, kumbe huwa anasema asili na ana acha tawi, na pengine anasema tawi na kuacha asili.' Na Abu Umar amesema: 'Na wamemsema Malik pia kulingana na aliyoyataja Saajii ndani ya kitabu *al-Ilalu,* Abdul-Azizi bin Abi Salma, na Abdur Rahman bin Zayd, walivitia dosari vitu katika madhehebu yake.' Mpaka anasema: 'Na Shafii na baadhi ya swahiba wa Abu Hanifa walimshambulia kuhusu kitu katika rai yake kwa ajili ya wivu wa mahali pake pa uimamu."[51]

Wana madhehebu ya Malik walidhikika naye, hivyo walimuwinda mpaka wakamuua. Na Ibnu Hajar amebainisha kuwa walimpiga kwa ufunguo wa chuma na akafa.[52]

Na aliitaja kaswida ya Abu Hayyan katika kumsifu Shafii: "*Walimchana paji la usowe, ufunguo wa chuma kutumia. Katoweka ameuawa mwishowe, bila wa kumlilia wala kumhabarishia.*"

Hivyo Shafii alikwenda akiwa mhanga wa chuki binafsi ya kimadhehebu kutoka kwa wanamadhehebu wa Malik. Pamoja na yote hayo Misri ilikuwa mbegu ya kwanza ambayo kutokea humo yamesambaa madhehebu ya Shafii, kwa fadhila za swahiba zake na wanafunzi wake, kama si wao hali yake ingekuwa hali ya madhehebu zilizotoweka.

Kama yalivyosambaa huko Sham, nchi ambayo madhehebu ya Awzaiy ilikuwa ndiyo ya walio wengi. Na baada ya Muhammad bin Uthman ad-Damashqiy as-Shafiiy kushikilia ukadhi humo alifanya kazi ya kueneza madhehebu ya Shafii huko Sham – Syria ya leo - na baada ya hapo madhehebu ya Awzaiy yalitoweka na kukatimia kufuatwa kwa madhehebu ya Shafii zama za dola ya al-Ayubiya, kwani wafalme wao walikuwa mashafi, jambo ambalo ni miongoni mwa yaliyosaidia kuimarika kwa madhehebu.

Na baada yao ilipokuja dola ya mamaliki huko Misri, hadhi ya madhehebu ya Shafii haikupungua, kwani walikuwa wafalme wake wote ni mashafi isipokuwa Saifu Diyn ndiye aliyekuwa Hanafii, lakini yeye hakuathiri kitu katika kuenea madhehebu ya Shafii. Kwa njia hii jina la Shafii lilipanda kupitia wafalme na masultani, lau si hivyo madhehebu yake yangekuwa yenye kusahaulika.

## Kashfa Juu Ya Shafii:

Kila imamu alikuwa na mistari miwili inayopingana. Mstari wa wanaovuka kipimo cha mambo, na mstari wa wale wanaochukia, kama ilivyotangulia kutajwa. Kwa mujibu huo haiwezekani kutathmini kwa kina zaidi hali ya Shafii. Na wanaovuka mipaka ya mambo wamemuelezea sifa kadhaa, wakamfanyia daraja ya ukamilifu, ambayo haiwezekani kiumbe yeyote kuifikia, na kinyume chake wanaomchukia wamemfanyia hadithi ambazo kwazo wamemteremsha chini kwenye daraja za Ibilisi.

Ameeleza Muhammad bin Abdillah al-Juwaybariy kutoka kwa Abdu bin Maadan kutoka kwa Anas kutoka kwa Nabii (s.a.w.w) kuwa amesema: "Katika umma wangu atakuja mtu atakayeitwa Muhammad bin Idrisa, atakuwa na madhara mno kwa umma wangu kuliko Ibilisi, na atakuja mtu katika umma wangu atakayeitwa Abu Hanifa, yeye ni taa ya umma wangu."[53] Na Hadith hii ni miongoni mwa ambazo watu wawili hawatofautiani kuwa ni ya kuwekwa.

Na kinyume chake Ibnu Abdil-Bar anaeleza kwa sanad yake kutoka kwa Suwaid bin Said amesema: "Tulikuwa kwa Sufyani bin Uyayna huko Makka, akaja mtu analeta habari ya kifo cha Shafii na anasema: 'Kwa kweli yeye amekufa.' Sufyani akasema: 'Ikiwa amekufa Muhammad bin Idrisa atakuwa amekufa mtu aliye bora mno katika watu wa zama zake."[54]

Habari hizi pia ni za uwongo, kwa kuwa kufa kwa Sufyan kulitokea mwaka 198 A.H. yaani kabla ya kufa kwa Shafii kwa miaka sita. Lakini pamoja na yote hayo kebehi zilimuelekea Shafii, walimsingizia kuwa ni Muutazila, na mara nyingine kuwa yeye ni Shia, na kuwa yeye anahadithia riwaya kutoka kwa waongo na kuwa yeye ni mwenye uchache wa Hadith.

Na aliulizwa Yahya bin Muiyn: "Je Shafii alikuwa anasema uwongo?" Alisema: "Sipendi Hadithi zake

wala simtaji.” Al-Khatib ameeleza kutoka kwa Yahya bin Muiyn kuwa yeye akasema: “Shafii sio mwaminifu.”

Na kuna kebehi zisizo na maana, siko katika nafasi ya kuzipa uzito na kutathmini, lililonichochea ni kumtuhumu Shafii tu kuwa ni Shia, na tuhuma kama hii ilikuwa inahesabika kuwa ni tuhuma hatari mno zama zile, zama ambazo Alawiyuna na Shia walikuwa wanajengewa kwenye nguzo na walikuwa wanauawa vibaya, hali ilifikia kujidhihirisha uadui dhidi ya Ali (a.s.) watoto wake na Shia wake ni jambo lenye kuenea.
Na ili kupata zaidi, rejea vitabu vya historia mfano wa *Maqatilut- Taalibiyna* cha Abul Faraji al-Asfahaniy, ili utambue aina kidogo miongoni mwa aina za adhabu walizofanyiwa Ahlul-Bayt na Shia wao. Kwa ajili hiyo watu waligawanyika makundi mawili, kikundi kilivuta subira na kujitoa muhanga na kushikamana na upendo wao kwa Ahlul-Bayt, na watu kama hawa ni wachache, na kundi, nalo ndilo la walio wengi wametii na kuiuza dini yao kwa dunia ya masultani. Imam Husein (a.s.) amekuwa mkweli aliposema:

“Watu ni watumwa wa dunia, na dini inarambwa tu juu ya ndimi zao, wanaiweka mahali ambapo pana mzunguko wa maisha yao, endapo watachujwa kwa balaa wanadini huwa wachache.”

Katika hali hii iliotanda giza, Imam Shafii alidhihirisha upendo wake kwa Ahlul-Bayt, na ilikuwa kuwapenda tu ni tuhuma ya kuwa yeye ni Shia. Ukweli ni kwamba Shafii hakuwa Shia, yaani hakuwa mwenye kuwatawalisha maimamu wa Ahlul-Bayt na mfuasi wa mwenendo wao, lakini ni upendo tu ambao huangikwa kwenye umbile la kila mwanadamu, na kwa ajili hiyo Shafii akasema:

“Eenyi Ahlul-Bayti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kuwapenda ni faradhi kutoka kwa Mwenyezi Mungu ameishusha ndani ya Qur’ani.

Wakutosheni utajo adhimu kuwa: Asiye kuswaliyeni hana swala.” Akiegemeza usemi huo kwenye kauli yake (s.w.t.):

قُلْ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَىٰ ۗ{23}

***“Sema: Kwa haya siombi malipo yoyote kwenu isipokuwa mapenzi katika karaba wangu.”*** (***Sura Shuura: 23***).

Na hiyo ni Aya inayoeleza wazi wajibu wa kuwapenda Ahlul-Bayt (a.s.). Na nilikuwa nastaajabishwa vipi Mwenyezi Mungu anaweka ujira wa risala yake katika kuwapenda Ahlul-Bayt?! Jambo hili halikuniwia wazi ila baada ya nilipojua kiwango cha mtihani wa kuwapenda Ahlul-Bayt na kushikamana nao. Na huyu Shafii ni mfano mbele yako, yalipodhihiri tu mapenzi yake kwa Ahlul-Bayt hapo hapo walimtuhumu kuwa ni Rafidhu, Shafii amesema:

**“Wakasema: Umekuwa rafidhu. Nilisema: La hasha, rafidhu sio dini yangu wala sio itikadi yangu. Lakini nimempenda bila shaka Imam aliye bora na mwongozi aliye bora. Ikiwa kumpenda wasii ni urafidhu, kwa hakika mimi ni mja rafidhu mno.”**

Na ulipodhihiri upendo wake kwa Ali (a.s.) baadhi ya wa shairi walimdhihaki: “Shafii anakufa wala hatambui: Mola wake ni Ali au Mola wake ni Allah.”

Na Shafii katika hali hii iliojaa msimamo wa chuki dhidi ya Ahlul-Bayt na Shia wao, hakusikia unyonge kuonyesha upendo wake kwao, mpaka alifikia kuimba shairi akisema:

**“Ewe msafiri simama changaraweni Mina, na mtangazie mwenye kuketi kwenye maporomoko yake na aliyesimama. Mahujaji watakapomiminika Mina usiku, mmiminiko wa mto wenye mawimbi yenye kumiminika: Ikiwa kuwapenda Ali Muhammad ni urafidhu, basi Vizito Viwili na vishuhudiye kuwa mimi ni Rafidhi.”**

Kama ambavyo Shafii alikuwa anawaita waliotoka dhidi ya Ali (a.s.) na kupigana naye kuwa ni waovu, tuhuma ya kuwa yeye ni Shia ni miongoni mwa yaliyothibitisha dhidi yake, tuhuma ambayo ilikuwa jinamizi vifuani mwa watawala. Lakini baada ya darasa na kutathmini inatudhihirikia kuwa ushia wa Shafii ulikuwa ushia kulingana na hali ya jamii ile aliyokuwa akiishi nayo, iliyokuwa imezama katika uadui dhidi ya Ahlul-Bayt (a.s.), wakiwafuata wafalme wao, kwa ajili hiyo alituhumiwa kwa Ushia. Na endapo tutaivua jamii ile ufuasi wake kwa utawala na siasa yake, hatumpati yeyote anayewachukia Ahlul-Bayt isipokuwa *Khawarij* na waliokwenda mwendo wao.

Kwa kuwa upendo wa Ahlul-Bayti hauachani na moyo wa mwislamu, hivyo kwa hilo Shafii anakuwa mpenzi wa Ahlul-Bayti na wala sio Shia.
Na tofauti ni kubwa kwa sababu kila anayependa unyofu na dini anawapenda Ahlul-Bayti ambao kwao dini hii imekuwa kielelezo, hata akiwa si mwislam, na shuhuda za hayo ni nyingi. Zitatutosha miongoni mwazo kuwa mwandishi mkristo George Jordaq, ametunga kitabu kikubwa chenye jalada tano kumhusu Imam Ali (a.s.), humo anamsifu kwa sifa tukufu mno ambazo aweza kusifiwa.

Na mwingine anatunga kitabu kingine kumhusu Sayyida Tahira Fatima Zahrau (a.s.) anakiita *Fatmatu Wataru Fii Ghumd*, naye ni Sulayman Kitaniy mwandishi wa kitabu *al- Imam Ali Nibrasu Wa Mitrasu*. Kama ambavyo kaswida ndefu mno duniani ambayo ina beti elfu tano ameitunga mkristo, ikimhusu Imam Ali bin Abu Talib (a.s.). Na kaswida ya pili yenye beti elfu tatu pia ni ya mkristo ikihusu ubora wa Imam Ali bin AbuTalib (a.s.).

Na yote hayo hayatoshi kuwafanya wawe Shia, upendo peke yake hautoshi kuwafanya Shia, kwa kuwa upendo wa kweli hasa ni kuwazingatia kuwa wao Ahlul-Bayt ndio mawalii, huku wakiwafuata na wakijikata kikamilifu mbali na wengine, na kuwaelekea wao Ahlul-Bayti ili kuichukua dini na maalumati ya kiislamu kama mshairi anavyosema:

**“Lau upendo wako ungekuwa wa kweli ungemtii. Kwa kuwa mpenda ni mtii kwa ampendaye.”**

## Imam Ahmad Bin Hanbal

Yeye ni Ahmad bin Muhammad bin Hanbal bin Hilal. Alizaliwa 164 A.H. huko Baghdad kama ilivyo mashuhuri, na kulingana na habari dhaifu ni kuwa amezaliwa huko Murruu. Ahmad amekuwa katika hali ya uyatima mkononi mwa mama yake na alielekea kwenye elimu akiwa na miaka kumi na tano, yaani hapo mwaka 179 A.H. Alisoma elimu ya Hadith baada ya kujifunza kusoma Qur'ani na Lugha. Sheikh wa kwanza ambaye kwake alipata elimu ni Hisham bin Bashir al-Silmiy, aliyefariki mwaka 183 A.H. Ahmad amekuwa naye miaka mitatu au zaidi.

Na alisafiri kwenda kusoma elimu ya Hadith huko Makka, Kufa, Basra, Madina, Yemen, Sham. Amesoma katika nchi hizo kwa kundi la wanazuoni, hapana haja ya kuwataja, bali aliye muhimu miongoni mwao ni Shafii, na wanastaajabisha mahanbali kumfanya Shafii mwanafunzi wa Ahmad!

Na yeye ana wanafunzi wengi, aliye mashuhuri ni Ahmad bin Muhammad bin Haniy, maarufu kwa jina la Al-Athrum aliyefariki mwaka 261 A.H. Na Swalih bin Ahmad bin Hanbal naye ni mkubwa katika watoto wake, na Abdullah bin Ahmad bin Hanbal, aliyefariki mwaka 290 A.H. alielezea Hadithi kutoka kwa baba yake.

### Miongoni Mwa Vitabu Vya Ahmad Na Athari Zake:

Ahmad hakutunga kitabu cha fiqhi kihesabiwacho kuwa ni asili, ambacho kutoka humo huopolewa madhehebu yake ya kifiqhi, ila tu yeye ana vitabu vimehesabika kuwa miongoni mwa maudhui za kifiqhi, mfano wa *al- Manasikul-Kabiir* na *al-Manasikus-Swaghiir* na *Risalatus-Swaghiiratu Fiis-Swalati*, lakini hivyo havivuki zaidi ya kuwa ni vitabu vya Hadith, japokuwa katika maudhui zake zimegusia kwa kuzikunjua na kuzisherehesha.55

Na ni maarufu kutoka kwake kuwa yeye alikuwa anachukia kuweka vitabu vinavyoingiza uwekaji matawi na rai. Siku moja alimwambia Uthman bin Said: "Usiangalie yaliyomo kwenye vitabu vya Abu Ubaid wala aliyoyaweka Is'haqa, wala aliyoyaweka Sufyan wala Shafii wala Malik, bali ni juu yako kushikamana na asili."

Na miongoni mwa tunzi zake zilizo mashuhuri katika Hadith ni *Musnad* yake. Ina Hadithi arobaini elfu, miongoni mwa zilizokaririwa ni kumi elfu, na Ahmad ameithibitisha *Musnad* yake. Na Alipoulizwa kuhusu Hadith akasema: "Angalia ikiwa ipo ndani ya *Musnad* vinginevyo sio hoja."

Hata hivyo Mahufadhi wengi wamezitia dosari wala hawakuamini kila kilichomo humo, bali wamesema wazi kuwepo kwa riwaya za kuzusha, lakini hii sio nafasi ya kulitafiti jambo hili.

### Mtihani Wa Ahmad Bin Hanbal:

Kwa kweli dosari inayojitokeza sana katika historia ya Ahmad bin Hanbal ni mtihani uliomkabili kwa sababu ya kusema kuwa Qur'ani haikuumbwa. Na taabu yake ilianza zama za Maamun ambaye alikuwa

anawatendea watu ukatili kwa kusema kwao kuwa Qur'ani imeumbwa. Na Maamun alikuwa mwanachuo wa theiolojia, alituma nyaraka zake kwa watendaji wake wote akiwapa amri ya kuwafanyia mtihani watu kuhusu kuumbwa kwa Qur'ani.

Imekuja katika waraka huo kuwa: "Khalifa wa waislam ni wajibu juu yake kuihifadhi dini na kuidumisha na kuwatendea raia haki. Amirul– Muuminina amejua kuwa kundi kubwa la watu na walio wengi toka raia wa kawaida na wa hali ya chini, ni watu wasio na maoni wala utambuzi, wala hawana dalili kwa dalili ya Mwenyezi Mungu na mwongozo Wake, wala mwanga kwa nuru ya elimu na uthibitisho wake, katika nchi na zoni zote.

Ni watu wasiomjua Mwenyezi Mungu na vipofu walio mbali naye, wapotevu wa ukweli wa dini yake na tawhidi yake na kumwamini, na wamekwenda kombo mbali na alama zake za wazi, na njia zake za wajibu. "Na wako na kiwango kidogo kumpa Mwenyezi Mungu uzito anaostahiki, na kumtambua utambuzi ulio sahihi, na wamtofautishe kati ya Yeye na viumbe wake, kwa sababu ya udhaifu wa rai zao na upungufu wa akili zao na ukavu wao kifikra na kikumbukumbu, na wamemfanya sawa Mwenyezi Mungu tabaraka wataala na alichoteremsha miongoni mwa Qur'ani, wakaafikiana kwa ujumla wao kuwa Qur'ani ni ya tangu na tangu, Mwenyezi Mungu hakuiumba na kuianzisha."56

Kutokea hapa ulianza mtihani wa kuumbwa Qur'ani, lakini Ibnu Hanbal bado hakuwa amenasa katika mtego wa mtihani na kuadhibiwa, mpaka katika zama za utawala wa Muutasim, kwa sababu ya kufa Maamun kabla hajatihaniwa. Na Muutasim alikuwa mkali katika kuwatahini watu na kuwatia adabu. Na ilipofika zamu ya Ahmad bin Hanbal, alikuwa ameapa kuwa hatomuua kwa upanga ila atampiga kipigo baada ya kipigo, na kumtupa mahali pa giza ambapo hatoona mwanga hapo.

Ahmad alibaki siku tatu kila siku analetwa kwa ajili ya mjadala, pengine atatii hukumu ya Sultani lakini yeye alishikilia kauli yake na alikataa. Na Muutasim alipokatishwa tamaa naye alitoa amri apigwe kwa mjeledi, na alipigwa mijeledi 38. Baada ya hivyo adhabu ya Ibnu Hanbal haikudumu, Muutasim alimuachia huru. Na hili ni miongoni mwa yanayostaajabisha na kushangaza, hivi hiyo yatosha kumfanyia Ahmad ubingwa wa kihistoria hali ikiwa historia imeshuhudia watu walioadhibiwa zaidi kuliko yeye?! Na wenye subira kuliko yeye?! Halafu kwa nini adhabu yake haikudumu?! Je alitii na kusema lisemwalo na Sultani?!

Na baadhi wamesema kuwa kundi la watu walijikusanya mlangoni kwenye nyumba ya Sultan, walikuwa wameazimia kuihujumu, Muutasim alitoa amri ya kuachiwa. Na hiyo haikubaliani na historia ya Muutasim ambaye alijulikana kuwa na nguvu na ugumu wa utashi na utukufu wa dola yake, hivyo ilikuwa haiathiriwi kwa kupingwa na watu wa kawaida.

Halafu hawa watu wa kawaida ni akina nani? Je ni wafuasi wa Ahmad?! Ahmad hakuwa mashuhuri kabla ya mtihani huu kiasi cha kuwa awe na watu wengi, na ikiwa walikuwa wafuasi wake basi jua Ahmad aliwapiga marufuku wasitoke dhidi ya Sultan. Hivyo sababu hii nayo haikinaishi.

Linalodhihiri ni kuwa sababu ya kuachwa huru ni kuwa Ahmad alimkubalia Khalifa na akasema usemi

wake, hivyo akamwachia kama alivyosema al-Jahidhu katika risala yake akiwasemesha Ahlul-Hadithi baada ya kuitaja taabu na mtihani, anasema:

"Alikuwa swahiba wenu huyu – yaani Ahmad bin Hanbal – anasema: 'Hapana *Taqiya* isipokuwa katika nyumba ya ushirkina. Lau ikiwa kukiri kwake kuwa Qur'ani imeumbwa, ilikuwa ni kwa njia ya *taqiya*, itakuwa ameitendea kazi *taqiya* ndani ya nyumba ya uislamu, na atakuwa amejikadhibisha mwenyewe. Na ikiwa kukiri alikokufanya ni sahihi na ni ukweli, basi ninyi si katika yeye na yeye si katika ninyi. Na yeye hakuona upanga uliochoomolewa, na wala hakupigwa mara nyingi, hakupigwa ila mijeledi thelathini iliochumwa matunda, yenye ncha zilizoshibishwa, mpaka alikiri bayana mara kadhaa.

"Wala hakuwa katika kikao cha dhiki wala hali yake haikuwa ya kukatisha tamaa, wala hakuwa amefungwa na chuma, wala kung'olewa roho yake kwa ukali wa kamio, kwa kweli alikuwa anazozwa kwa maneno laini mno na alikuwa akijibu kwa jibu zito, walikuwa wananyanyua sauti na yeye hurudisha chini, wanaongea naye kwa upole naye anahamaki, wanasema kwa upole naye hujibu upuuzi."57

Hilo latiliwa nguvu na alilolisema al-Yaqubiy katika kitabu chake cha historia miongoni mwa kauli ya al-Jahidhu juu ya Ahmad bin Hanbal kukiri kuwa Qur'ani ni kiumbe, akasema: "Muutasim alimtihani Ahmad bin Hanbal kuhusu kuumbwa kwa Qur'ani. Ahmad akasema: 'Mimi ni mtu nimejua elimu na sijajua katika elimu hiyo hili.' Alimletea wanachuoni, na Abdur Rahman bin Is'haqa na wengine walimhoji. Alijizuia kusema kuwa Qur'ani ni kiumbe, alipigwa mijeledi kadhaa, Is'haqa bin Ibrahim akasema: 'Niweke mimi ewe Amirul-Muuminina nimuhoji, akasema: 'Fanya naye mjadala.'

"Is'haqa akasema: 'Hii elimu ambayo umeijua aliteremsha kwako malaika au umejielimisha kutoka kwa watu?!' Ahmad akasema: 'Nilijielimisha kutoka kwa watu.' Is'haqa akasema: 'Kitu kimoja baada ya kingine au kwa mpigo?' Ahmad alisema: 'Nimejifunza kitu kimoja baada ya kingine.' Is'haqa akasema: 'Hivyo basi kumebaki kitu bado haujakijua.' Ahmad akasema: 'Kumebaki kwangu kitu sijajua.' Is'haqa akasema: 'Hiki ni miongoni mwa usichojua bado, na Amirul-Muuminiina amekujulisha.' Ahmad akasema: 'Mimi nasema usemi wa Amirul-Muuminina.' Is'haqa akasema: 'Kuhusu kuumbwa kwa Qur'ani?' Ahmad akasema: "Kuhusu kuumbwa kwa Qur'ani."58

Hivyo basi mayoe haya, sana yanakuwa ni ya kubuni kuliko ukweli hasa, mahanbali kutokana na kisa hiki wamebuni hadithi na visa ili iwe kujigamba na tangazo la kuutambulisha uimamu wa Ahmad bin Hanbal. Vinginevyo endapo mas'ala hii ikihukumiwa kwenye ardhi ya ukweli, Ibnu Hanbal hakuwa bingwa wake.

## Mabingwa Hawakulazimishwa Na Hali Ya Mambo:

1. Ahmad bin Nasru Al-Khuzaiy, aliyeuawa mwaka 231 A.H. Naye ni miongoni mwa wanafunzi wa Malik bin Anas. Na riwaya imeelezwa kutoka kwake na Ibnu Muin na Muhammad bin Yusuf, alikuwa miongoni mwa wenye elimu, al-Wathiq alimuuliza: "Wasema nini kuhusu Qur'ani?" Alisema: Maneno ya Mwenyezi Mungu si yenye kuumbwa." Alimlazimisha aseme yameumbwa lakini alikataa. Na alimuuliza

kuhusu kumuona Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama. Akasema: Ndio, na akasimulia Hadith kuhusu hilo.

Al-Wathiq akasema: "Ole wako, je ataonekana kama aonekanavyo aliye na mipaka, aliye na mwili na ambaye hubwebwa na mahali, na anazingirwa na mwonaji. Umemkufuru kabisa Mola ambaye umemsifu kwa sifa hizi."

Na Ahmad al-Khuzaiy aliposhikilia rai yake, Khalifa aliagiza aletewe upanga uitwao *as-Swamswamah,* na akasema: "Mimi nahesabia kosa langu kwa huyu kafiri ambaye anamwabudu Mola tusiyemwabudu, wala hatumtambui kwa sifa alizomsifu nazo."

Kisha yeye mwenyewe alimwendea na aliikata shingo yake. Alitoa amri kichwa chake kichukuliwe mpaka Baghdad, kilisimamishwa upande wa Mashariki siku kadhaa, kisha upande wa Magharibi siku kadhaa, na aliposulubiwa Al-Wathiq aliandika waraka na uliangikwa kichwani mwake: "Hiki ni kichwa cha Ahmad bin Nasr bin Malik, mja wa Mwenyezi Mungu Imam Harun alimwita - naye ni Al-Wathiq - alimlingania kuwa Qur'ani imeumbwa na akatae tashbihu, lakini alikataa na kukaidi, hivyo Mwenyezi Mungu alimharakisha kwenye moto wake."59

2. Yusuf bin Yahya al-Buwaytiy, kama ilivyotangulia ni miongoni mwa wanafunzi wa Shafii na mrithi wake wa duru ya darasa lake. Alibebeshwa uzito wa ratili arobaini za chuma kutoka Misri mpaka Baghdad. Alifanyiwa mtihani na alikataa kusema kuwa Qur'ani ni kiumbe. Na akasema: "Wallahi nitakufa nikiwa na chuma changu hiki ili baada yangu waje kaumu wajue kuwa wamekufa kaumu ya watu kwenye vyuma vyao kwa suala hili, na lau nitaingia kwake – amkusudia Al-Wathiq – nitakuwa mkweli." Na aliendelea kukataa mpaka alifia jela mwaka 232 .A.H.

Na wengine nafasi haitoshi kuwataja walikuwa wakakamavu mno na kung'ang'ania kuliko Ahmad, na ni miongoni mwa dhuluma kumfanya Ahmad bin Hanbal kuwa ni yeye peke yake aliyekabiliwa na taabu hii, na iwe ndio ubingwa wake mkubwa. Japokuwa yeye alikuwa kinyume na hali hiyo kabisa, kama ulivyokwishajua utii wake na kukiri kwake kwa Muutasim.

## Ahmad Katika Enzi Za Mutawakil:

Mutawakil alipokuja kwenye mlango wa hukumu, aliwaleta karibu Ahlul- Hadith na kuwatia adabu Muutazila, kinyume na hali ya mambo ilivyokuwa katika enzi ya Maamun, Muutasim na Al-Wathiq, aliwapa mtihani wa kuumbwa Qur'ani.

Mwenye kusema miongoni mwao kuwa Qur'ani imeumbwa huadhibiwa na kuuliwa, hivyo Ahlul-Hadith walipata walilokuwa wanalitaka, na kwa hilo sauti yao ikapanda, na walishikilia nafasi ya juu, na walilipiza kisasi kwa Muutazila vibaya mno.

Ahmad Amin amesema: "Khalifa Mutawakil alitaka aikumbatiye rai ya walio wengi, na ili avune uungwaji mkono, hivyo alibatilisha usemi wake wa kuumbwa Qur'ani, na kubatilisha mitihani na hukumu, na aliwanusuru wanahadith."60

Hisa kubwa mno ya kujikurubisha kwa Mutawakil ilikuwa ni ya Ahmad bin Hanbal. Kwa kuwa yeye ndiye aliyebaki kati ya waliotihaniwa na suala la Qur'ani, baada ya kuuliwa mashujaa wake. Na Mutawakil alikuwa anawausia maamiri wamheshimu Ahmad na kumthamini, na wawe wanampa kitu kizuri na waelemee kwake. Na alimuandalia kila mwezi mshahara Dirhamu elfu nne[61]

Nyota ya Ahmad ilipaa, watu walisongamana mlangoni kwake, na watu wa dola na wakuu wake walirundikana kwake. Na Ahmad kwa upande wake aliona ukhalifa na uimamu wa Mutawakil ni sahihi na ni lazima kumtii. Alikuwa anaiunga mkono dola na kuikazia mkanda wake. Na hili sio geni kwa Ahmad kwa kuwa yeye anaona yapasa kumtii mtawala yoyote awae, mwema au muovu.

Ahmad amesema katika moja ya risala zake: "Usikizi na utii ni wa maimamu na wa amiri wa waumini, wema na waovu, na ni wa mwenye kutawalia kiti cha ukhalifa, na watu wameafikiana na kumridhia. Na mwenye kuwashinda kwa upanga na akaitwa Amirul-Muuminiina.

Na kuhujumu kwaenda na watawala mpaka siku ya Kiyama, mwema na muovu. Na kutekeleza hadi za kisheria ni kwa maimamu, haimfalii yeyote awakebehi au kuwakinza, na kuwapa wao sadaka inafaa, ambaye ataitoa kwao itamtosheleza, mwema awe au muovu. Na swala ya Ijumaa nyuma yake na nyuma ya kila aliyetawala uimamu wake inafaa.

"Na mwenye kuiswali tena ni mfanya bidaa, na ni mwenye kuiacha athari, afanyaye kinyume na Sunna. Na mwenye kutoka dhidi ya imamu miongoni mwa maimamu wa waislam, ambaye watu waliafikiana na kumkiri awe khalifa kwa njia yeyote miongoni mwa njia, iwe kwa ridhaa au kwa ushindi, atakuwa amechana umoja wa waislamu na kukhalifu athari kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, akifa mwenye kutoka atakuwa amekufa kifo cha kijahiliya"[62]

Na Abu Zahra anasema ndani ya kitabu hikihiki Uk. 321: "Na Ahmad ana rai inayoafikiana na ya wanachuoni wengine, nayo ni kufaa uimamu wa kushinda kwa nguvu na watu wakaridhia, na akaweka hukumu njema kati yao. Bali yeye anaona zaidi ya hivyo, mwenye kushinnda japo awe muovu, utii kwake ni wajibu ili yasitokee machafuko."

Kwa minajili hiyo tunawakuta wafuasi wake miongoni mwa Salafiya na Mawahabi wanamhukumu Huseini bin Ali (a.s.) kuwa yeye ni mkosefu, na ilikuwa wajibu juu ya Yazid amuuwe kwa sababu ya kutoka kwake mbali na utii wa Imam wa zama zake. Nimelisikia hilo kwa sikio langu kutoka kwa mmoja wao naye alikuwa anajadiliana na mimi akilinda ulinzi wa kufa na kupona kumhami Yazid, akasema: "Husein alitoka na kuacha utii wa imamu wa zama zake, ni wajibu auawe."

Angalia kwa upeo gani mtu anachukua ufuasi wa waliopita kwa upofu?! Hivi Ahmad bin Hanbal ana thamani gani kwa kumlinganisha na Husein (a.s.), kiasi cha kuwa niwe ninasema asemayo na nifanye kulingana na fatwa zake, na nimvurumishie Husein kuwa ni dhalimu na aliyekiuka?!

Endapo tukijivua na kuwa mbali na kufuata huku kwa upofu, na tukazizingatia Aya za Qur'ani itakuwa bora na ni karibu mno na ukweli. Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amesema:

وَلَا تَرْكَنُوا إِلَى الَّذِينَ ظَلَمُوا فَتَمَسَّكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ أَوْلِيَاءَ ثُمَّ لَا تُنْصَرُونَ {113}

***"Wala msiwategemee wale waliodhulumu usije ukakuguseni moto. Na hamtakuwa na walinzi badala ya Mwenyezi Mungu, kisha hamtasaidiwa."*** (***Sura Hud: 113***)

Na amesema:

وَلَا تُطِعْ مَنْ أَغْفَلْنَا قَلْبَهُ عَنْ ذِكْرِنَا وَاتَّبَعَ هَوَاهُ وَكَانَ أَمْرُهُ فُرُطًا {28}

***"Wala usimtii ambaye tumeughafilisha moyo wake usitukumbuke, naye akafuata matamanio yake, na mambo yake yamepita kiasi."*** (***Sura Kahf: 28***)

Na amesema: ***"Basi usiwatii waliokadhibisha."*** (***Sura Qalam: 8***)
Na amesema: ***"Wala msitii amri za wale maasi."*** (***Sura Shu'ara: 151***)

Lakini wao wameiacha Qur'ani nyuma ya migongo yao, na walizitolea hoja riwaya zilizowekwa na wadhalimu miongoni mwa watawala wa Bani Umaiyya, ili watu watii utawala wao. Ahlul-Bayt wamezipinga Hadithi hizi kwa Hadithi za kweli na zinazoafikiana na Qur'ani na roho ya kiislam.

Imam as-Sadiq (a.s.) amesema: "Mwenye kupenda kubakia kwa wadhalimu atakuwa amependa Mwenyezi Mungu aasiwe." Hii zaidi ya kuwa ni Hadith nayo pia ni dalili ya kiakili makini.

Kwa kuwa aonaye yafaa kusalimu amri kwa dhalimu na kumtii na asimpinge, amependa kubaki kwa kufanyiwa Mwenyezi Mungu maasi. Mwenyezi Mungu (swt) amesema:

وَمَنْ لَمْ يَحْكُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ {44}

***"Na wasiohukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri."*** (***Sura Maidah: 44.***)

وَمَنْ لَمْ يَحْكُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ {45}

“Na wasiohukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu.” (Sura Maidah: 45.)

وَمَنْ لَمْ يَحْكُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ {47}

***“Na wasiohukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio waasi.” (Sura Maidah: 47.)***

Kuongezea juu ya hayo ni Aya na riwaya zinazojulisha wajibu wa kuamrisha mema na kukataza maovu. Ndio maana Huseni alipoazimia kutoka dhidi ya muovu wa zama zake Yazid alisema:

“Oh! Ninyi watu kwa hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) amesema: ‘Amuonaye sultani dhalimu anahalalisha aliyoharamisha Mwenyezi Mungu, mwenye kulitangua agizo la Mwenyezi Mungu, mwenye kwenda kinyume na Sunna ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), anawatendea waja wa Mwenyezi Mungu dhambi na uadui, na – muonaji – asibadilishe – aliyoyaona – kwa kitendo wala kwa kauli, itakuwa haki kwa Mwenyezi Mungu amuingize mahali pake.’ Tambua kwa kweli hawa wamejilazimisha utii wa Shetani na wameacha utii wa Rahmani na wamedhihirisha ufisadi na wameitelekeza mipaka, na wamejitwalia ngawira peke yao na wamehalalisha haramu ya Allah, na wameharamisha halali yake, na mimi ni mstahiki zaidi kuliko mwingine.”[63]

Lakini tutawaambia nini watu wakati wamewatelekeza maimamu wa Ahlul-Bayt na wamewabadilisha na maimamu waliotengenezwa, ambao Mwenyezi Mungu hajatoa amri ya kuwatii. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema:

وَقَالُوا رَبَّنَا إِنَّا أَطَعْنَا سَادَتَنَا وَكُبَرَاءَنَا فَأَضَلُّونَا السَّبِيلَا {67}

رَبَّنَا آتِهِمْ ضِعْفَيْنِ مِنَ الْعَذَابِ وَالْعَنْهُمْ لَعْنًا كَبِيرًا {68}

***“Na watasema: Mola wetu! Hakika tumewafuata mabwana wetu na wakubwa wetu, basi wao wametupoteza njia. Mola wetu! wape hawa adhabu maradufu na uwalaani laana kubwa.” (Sura Ahzab: 67- 68).***

Dhambi kubwa iliyoje hii, kwa umma wa kiislamu waliyoifanya watawala wa Bani Umaiyya, kwa kuziweka Hadithi hizi za uwongo kumzulia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), bali ukubwa ulioje wa

dhambi ya fatwa hii aliyoifutu Ahmad bin Hanbal.

Na kwa kiwango gani ni yenye kuharibu kizazi cha wanamageuzi wa kiislamu ambao wangeikana dhuluma na ukandamizwaji katika zama hizi zinazosifika kwa uelewa na mwamko enezi, ambao haiwezekani kwenye njia yake zikingame chombezo za wanachuo wa Ikulu na utawala. Ikiwa kuna dhambi imetendwa na kundi la vijana waliojiunga chini ya bendera za ujamaa na zisizo za kiislamu, basi dhambi ilio kubwa mno ni ile walioitenda wanachuo waovu.

## Fiqhi Kwa Ahmad Bin Hanbal:

Ni maarufu kuwa Ibnu Hanbal ni mtu wa Hadith, hakuwa mwanafiqhi. Wafuasi wake ndio waliokusanya baadhi ya rai zake mtawanyiko zilizonasibishwa kwake, na hatimaye kutokana nazo wamefanya madhehebu ya kifiqhi. Kwa minajili hiyo tunakuta mkusanyiko wa kifiq'hi ulionasibishwa kwa Ahmad ni wenye tofauti na wenye kupingana. Zaidi ya hapo ni kule kutofautiana kwao katika kuyapa tafsiri makusudio ya baadhi ya misamiati ambayo kutokana nayo, haifahamiki hukumu ya kisheria katika mas'ala hii. Kwa mfano ni kauli yake: 'Haipaswi.' je hilo tamko lichukuliwe kumaanisha haramu au makruhu. Hivyo hivyo kauli yake:
'Yanipendeza au Hainipendezi.' au 'Nachukia au Sipendi.'
Kama ambavyo Ahmad mwenyewe hajadai kuwa ni miongoni mwa wanafiqhi na mwanauelewa wa kifiqhi, bali alikuwa anajihadhari kutoa fatwa, na alikuwa anajiweka mbali nayo. Al-Khatib amesema kwa sanad yake: "Nilikuwa kwa Ahmad bin Hanbal, na mtu mmoja alimuuliza kuhusu mas'ala ya halali na haramu. Ahmad alimwambia: 'Muulize mtu mwingine Mwenyezi Mungu akusamehe.' Yule mtu alisema: 'Tutakalo ni jibu lako ewe baba Abdullah.' Alisema: 'Muulize mtu mwingine sio mimi, Mwenyezi Mungu akusamehe. Waulize wanafiqhi, muulize Abu Thaur.'64

Kwa mantik hiyo alikuwa binafsi kwa hilo hajihesabu miongoni mwa wanafiqhi. Amesema al-Maruziy: "Nilimsikia Ahmad akisema: 'Ama kuhusu Hadith tumekuwa na raha nayo, ama kuhusu mas'ala nimeazimia mtu akiniuliza kitu nisijibu."65

Al-Khatib amesema kwa sanad yake kuwa "Ahmad bin Harbi alikuja (mtawa wa Nisaburiy) kutoka Makka, Ahmad bin Hanbal aliniuliza: 'Huyu Mkhurasani aliyekuja ni nani?' Nilisema: 'Miongoni mwa zuhudi yake ni kadha na kadha.' Akasema: 'Haimpasi anayedai analodai – anakusudia zuhdi – ajiingize binafsi kutoa fatwa."66

Huu ndio mwendo wake, hajiingizi katika kutoa fatwa, alikuwa anauona utoaji fatwa haulingani na zuhudi, basi itakuwaje mtu mfano wa huyu awe na fiqhi au madhehebu kiasi afanyiwe ufuasi katika mambo ya kiibada?!

Abu Bakr al-Ashrum ambaye ni mwanafunzi wa Ahmad bin Hanbal amesema: "Nilikuwa ninahifadhi fiq'hi na tofauti zilizopo, na nilipomfuata Ahmad niliacha yote hayo."

Alisema Ahmad bin Hanbali: "Ole wako uongee kuhusu mas'ala ikiwa hauna Imam katika mas'ala

hiyo."[67]

Yaani kwa ibara iliyo safi: Usitowe fatwa japo unazo Hadith mkononi mwako, ila ukiwa una Imam wamtegemea katika fatwa hii.

Kama ambavyo alikuwa haoni kuwa yafaa kutilia uzito moja wapo kati ya kauli za Swahaba iwapo wakihitilafiana katika mas'ala, bali alikuwa anaona umfuate umtakaye. Na hilo lilikuwa ni jibu lake kwa Abdur- Rahman Swairafiy alipomuuliza: Je inawezekana kutilia uzito kati ya kauli za Swahaba.

Ambaye anakataza kutilia uzito na kuchukua kauli iliyo bora zaidi miongoni mwa kauli, yuko mbali mno na ijitihadi. Na miongoni mwa dalili ijulishayo kuwa Ahmad bin Hanbali hakuwa na madhehebu ya kifiqhi, ni kuwa wengi miongoni mwa swahaba wake wenye kumpendelea mno wametofautiana katika madhehebu yao kifiqhi.

Je wao ni mahanafi au mashafi? Mfano wa Abul-Hasan al-Ash'ariy, alipoacha madhehebu ya Muutazila na kuwa muhanbali, hakujulikana kuwa afuata dini ya Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa fiqhi ya Hanbali, kadhalika Kadhi al-Baqlaniy alikuwa mmaliki, hivyo hivyo Abdullah al- Answariy al-Harawiy, aliyefariki mwaka 481 A.H. Aliesema: "Mimi ni muhanbali niwapo hai na nifapo. Usia wangu kwa watu ni wawe mahanbali." Japokuwa alikuwa na upendeleo wa Ahmad, lakini upande wa fiqhi alikuwa katika njia ya Ibnu Al-Mubaraka. Na hilo ndilo lilikuwa linajulikana kwa waliokuwa katika zama zake na walio karibu na wakati wake. Hivyo wanaonasibika naye wananasibika naye kiitikadi sio kifiqhi.

Zaidi ya hapo ni kuwa Ibnu Hanbal katika risala zake anakataza: Rai, kukisia, na mapendekezo ya kifiqhi, na alikuwa anawafanya wasemao ukisiaji ni katika wafuasi wa al-Jahmiyah, al-Qadiriyah na Rawafidhu, na akimshambulia Abu Hanifa mwenyewe.
Pamoja na hayo yote lakini tunaona usemi wa ukisiaji umeingizwa katika fiqhi ya Hanbali, na hili ni miongoni mwa ambayo yanatufanya tuwe na shaka kuwa Ahmad bin Muhammad bin Harun (Abu Bakr al-Khallal) aliyefariki mwaka 311A.H. naye ndiye mpokezi na mwenye kunakili fiq'hi ya Hanbali, hakuwa mwaminifu katika kunakili kwake, au ni kuwa mambo yalimchanganya, khususan ni kuwa yeye hajakuwa katika zama za Ahmad bin Hanbal, amekusanya mas'ala mtawanyiko ya kifiqhi, yaliyonasibishwa kwa Ahmad. Na hilo linatiliwa nguvu na kule kuhitilafiana kwa riwaya kuhusu kauli za Ahmad, hitilafu kubwa mno kiasi kwamba inakuwa vigumu kwa akili kuzinasibisha zote kwake.

Abu Zahra anasema: "Kwa hakika fiqhi iliyonakiliwa kutoka kwa Ahmad bin Hanbal, kauli zake zimepingana humo, upinganaji ambao inakuwa vigumu kwa akili kuzinasibisha kauli hizi zote kwake. Fungua kitabu chochote miongoni mwa vitabu vya mahanbali, na mlango wowote miongoni mwa milango yake, utakuta haikosi kuwa na mas'ala kadhaa ambazo riwaya zake humo zimehitilafiana kati ya la na naam."[68]

Hivyo hapakuwa na madhehebu ya fiqhi yaliyo wazi ya Ibnu Hanbal kwa watu wa zama zake, na ambayo yapo ni madhehebu iliyofanywa iliyoenezwa na mahanbali kwa nguvu na ukali, kama ilivyokuwa huko Baghdad, ambako madhehebu ya Shia ndiyo yalikuwa aghlabia. Ama nje ya Baghdad hayakuwa

maarufu, walikuwa wanaitakidi watu kwa idadi maalumu huko Misri, na hiyo ni katika karne ya saba. Lakini alipotwaa ukadhi Muwafiqudin Abdullahi bin Muhammad bin Abdul-Malik al- Hijaziy, aliyefariki 769 A.H. madhehebu ya Ahmad yalisambaa kupitia yeye, hivyo aliwaweka karibu wanachuoni wa kihanbali na kuinua daraja zao.

Ama nchi zingine hawakutajika. Ibnu Khaldun ametoa sababu ya hilo kwa kauli yake: "Ama Ahmad wafuasi wake ni wachache kwa sababu madhhebu yake yako mbali na ijtihadi" Kama ilivyo katika kitabu *Al-Muqadimah*. Mahanbali hawakupata njia ya kusambaza madhhebu yao ila kwa vurugu na kuwapiga watu mitaani na njiani, hadi waliisumbua nidhamu huko Baghdad.

Hivyo Khalifa Radhiy ikatoa saini akikemea matendo yao, na akiwalaumu juu ya kauli yao ya tashbihi, sehemu ya saini hiyo ni: "Mara ninyi mwadhania sura za nyuso zenu mbaya zisizopendeza ziko mfano wa Mola wa ulimwengu, na umbo lenu duni liko kama alivyo! Na mnataja viganja, vidole, miguu miwili, ndara mbili za dhahabu, na kupaa mbinguni na kuteremka duniani. Mwenyezi Mungu ametukuka yumbali na wasemayo madhalimu na wapinzani juu utukufu mkubwa..."69

Yakawa madhehebu ya Hanbali katika usawa huo, hayakuwa na wafuasi wengi, kama ambavyo nafsi zilikuwa zayakimbia kwa ajili ya itikadi yao kuhusu Mwenyezi Mungu na kumshabihisha kwao Mola, na kumwelezea sifa zisizolingana Naye. Hayakupata fursa ya kutosha ya kusambaa, mpaka yalipokuja madhehebu ya Uwahabi yakiwa chini ya uongozi wa Muhammad bin Abdul-Wahabi, ambaye alijijengea mwenendo wa kihanbali, akasaidiwa na utawala wa Aali Suudi kueneza madhehebu kwa makali ya upanga, hapo mwanzo wake, na kwa nguvu ya Riyali huku mwishoni.

Na yasikitisha kuwa watu wengi wanashikamana na fiqhi ya Hanbali wakiwa hawana dalili juu ya hilo, ila kwa kutumia mlango:

قَالَ مُتْرَفُوهَا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ آثَارِهِمْ مُقْتَدُونَ {23}

***"Bali wanasema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu juu ya desturi na tunafuata nyayo zao."*** (***Sura Zukhruf: 23***)

Na ikiwa si hivyo basi hapana budi kuthibitisha dalili zao sehemu hizi tatu: Kwanza: Ahmad bin Hanbal ni mjuzi wa fiqihi. Pili: Fiqhi iliyonasibishwa kwake sio ya kubuni. Na baada ya kuthibiti yote hayo hapana budi kuthibitisha kwa hoja ya wazi kuwa ni wajibu kumfuata Ahmad bin Hanbal kwa dhati kabisa. Na kama si hivyo itakuwa ni kufuata dhana tu. Na dhana haitoshi kitu kwenye ukweli.
Hii ni ukiongeza kuwa wenye upendeleo kwa Ahmad mfano wa Ibnu Qutayba hawakumtaja katika jumla ya wanafiqhi, lau angekuwa mwanafiqhi mujtahid basi Ibnu Qutayba hangempunguzia haki yake, hivyo hivyo Ibnu Abdil-Bar alipowataja wanafiqhi katika kitabu chake *al-Intiqau* hakumtaja. Wala Ibnu Jarir Tabariy mwandishi wa tafsiri na historia, hakumtaja katika kitabu chake *Ikhtilaful-Fuqahau*. Aliulizwa hilo

akasema: “Ahmad hakuwa mwanafiqhi, bali alikuwa mwanahadithi, wala sikuona yeye kuwa na maswahiba wanaotegemewa.” Hilo likawachukiza mahanbali, wakasema kuwa yeye (Tabariy) ni Rafidhu.

Na walimuuliza (Tabariy) kuhusu Hadithi ya kukaa juu ya Arshi. Akasema: Ni muhali. Na alisoma beti:

**“Subhana Ambaye hana mliwazi. Wala mwenzi katika Arshi Yake.”**

Wakawazuwia watu wasikae naye (Tabariy) na wasiingie kwake, na wal- imshambulia kwa kalamu zao, na alipojibakisha nyumbani kwake walimshambulia kwa mawe hadi yakawa fungu.”70**70**

Na hii yajulisha upendeleo wa mahanbali na upekee wao katika kusambaza madhehebu yao ambayo wanachuoni bado hawajayatambua. Sheikh Abu Zahra amesema: “Kwa kweli wengi miongoni mwa watu wa mwanzo hawakumhesabu Ahmad kuwa ni miongoni mwa wanafiqhi, kama Ibnu Qutayba ambaye alikuwa karibu sana na zama za Ahmad, na Ibnu Jarir Tabariy na wengine wasiokuwa hawa wawili.”

## Hitimisho:

Na baada ya onyesho hili la madrasa za kifiqhi kwa Ahlu Sunna imetuwia wazi kuwa madhehebu haya hayana kipambanuzi cha kuyaweka mbali na mengine, ili yawe na haki pekee ya kusambaa na kuenea ulimwengu wote wa kiislamu, lau kama si ile siasa iliyofanya maimamu wa madhehebu wawe wanne, na ndio chimbuko la fiqhi.

Hivyo ni kwa sababu siasa inayotawala haiwezi kuipiga vita dini, bali ni kinyume chake, yenyewe inawanusuru wanachuoni na kuwakurubisha lakini kwa sharti mafunzo yao yasiguse maslahi ya dola. Kwa kuwa ukuu wa Sultani ni zaidi kuliko kingine chochote kile.

Kwa minajili hiyo tunaona madhehebu haya manne yamechaguliwa kati ya mamia ya madhehebu, na yakazingirwa na msamaha wa kifalme na ridhaa ya Sultani. Hivyo basi wanafunzi wao wakashikilia madaraka ya ukadhi, na mambo ya dini yakawekwa mkononi mwao. Wakasambaza kwa mujibu huo madhehebu ya masheikh wao, yale wayapendayo, kama ambavyo ufafanuzi wake ulivyotangulia.

Ilitoka amri wakati wa enzi ya Mansur, naye ni miongoni mwa watawala wa Bani Abbas, inayoamua kujiambatanisha na kauli za masheikh wa huko nyuma, kuwa kusitajwe kauli yoyote pamwe na kauli zao. Na wanavyuoni wa majimbo walitoa fatwa kuwa ni wajibu kufuata madhehebu manne, na kuharamisha madhehebu mengine yasizokuwa hayo manne, na kufunga mlango wa ijtihadi. Ahmad Amin anasema: “Serikali zilikuwa na uwezo mkubwa wa kujiingiza kuzinusuru madhehebu za Ahlu Sunna. Na kwa kawaida serekali inapokuwa yenye nguvu na ikaiunga mkono madhehebu miongoni mwa madhehebu, watu huyafuata kwa kuyafanyia taklidi, na yatabakia yametawala mpaka itoweke dola.”71

Je baada ya haya anaweza kutoa hoja mtoa hoja kuwa kufuata madhehebu manne haya ni wajibu?! Bali

je kimsingi, kuna dalili yoyote imekuja ya kuyawekea madhehebu uwigo wa kuwa ni manne tu?! Ikiwa hakuna dalili iwajibishayo kuwafuata wao, je, Mwenyezi Mungu na Mtume wake walighafilika na amri hii, ikawa hawakubainisha kwao kwa nani wachukue dini na sheria ya hukumu zao?! Na kwa nani wasichukue?!

Mwenyezi Mungu ni Mtukufu mno, si kiasi cha kuwaacha viumbe bila ya kuwabainishia hukumu zao na njia ambayo kwayo kuna uokovu wao. Kwa kweli amebainisha kupitia ulimi wa Mtume wake (s.a.w.w) na amesi- mamisha hoja na uthibitisho kuwa, ni wajibu kufuata kizazi cha Mtume (s.a.w.w), ambao ni watu mahsusi Kwake na mahali pa hekima Zake.

Lakini kilipokuwa kizazi kilicho tohara kinakinza watawala na madhalimu wa zama zao na mabeberu wao, na waliopokonya haki yao, utawala uliwaweka watu kando nao, na kuwa wasishikamane nao. Na aghlabu watu ni wapuuzi, wafuasi wa kila anayeguta, wanageuka na kila upepo, hawafaidiki na nuru ya elimu, wala kurejea kwenye kishiko thabiti.

Na kinyume chake waweza kuangalia kambi ya Ahlul-Bayt ambayo haikuhitajia utawala ili kung'arisha wanachuo wake, bali walishikamana na aliyoyasema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w): ''Kwa hakika mimi nimeacha katika ninyi Vizito Viwili: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu, Ahlul-Bayt wangu, kwa kuwa Mjuzi Mwenye hekima amenipa habari kuwa, viwili hivi havifarikiani mpaka vitakaponijia kwenye hodhi.''

Walijilazimisha kuwa pamoja na kizazi waliinywesha dini yao na fikra zao kutoka humo, hawakwenda kinyume na Ahlul-Bayt (a.s), wala hawakuwatangulia na wala hawakuwahitajia watu wengine ili wawatake kutoa fatwa, bali walichukua kutoka kwa ambao Hadithi yao ni Hadithi ya babu yake, na Hadithi ya babu yake ni Hadithi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), na Hadithi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ni Hadithi ya Jibril, na Hadithi ya Jibril ni Hadithi ya Allah.

Mshairi amesema: "Ukitaka madhehebu kwa ajili yako ikuokoe mbali na muale wa moto siku ya kufufuka, achana na kauli ya Shafii, Malik na Ahmad na Hanafi, iliyoelezwa na Kaabul-Akhbar. Wafanye mawalii watu ambao kauli yao na Hadithi yao ameieleza babu yetu kutoka Jibrail kutoka kwa Muumba."

## Fiqhi Kwa Shia:

Hali hii ya kuchukua moja kwa moja, kutoka kwa Maimamu wa Ahlul- Bayt (a.s.) iliendelea hadi alipokuja Imamu wa kumi na mbili Muhammad bin al-Hasan al-Mahdi (a.s.), aliwachorea Shia njia yao ambayo watakayoipita katika kuchukua hukumu za kifiqhi pindi atakapokuwa ghaibu, akasema: "Ama awae miongoni mwa mafaqihi mwenye kujilinda nafsi yake, mwenye kuihifadhi dini yake, yupo kinyume na matamanio yake, mtii wa amri ya Mola Wake, hivyo watu wa kawaida wamfuate.''72

Kwa ajili hiyo uliwafungukia mlango wa ijtihadi na uhakiki na istinbati. Hivyo ikajitokeza fikra ya marjaiyah ya kifiq'hi. Kuwa Shia atachagua miongoni mwa wanachuoni aliye na elimu zaidi na taqwa na uchamungu, amfuate katika hukumu za kifiqhi na mambo yajitokezayo, na wanafiqhi wamechambua

katika mlango huu.

Baadhi ya uchambanuzi wakujia kutoka katika kitabu *al-Masailu al-Islamiya* cha Samahatu Ayatullahi al-Udhma Sayyid al-Husainiy as-Shiraziy Uk. 90:

"**Mas'ala 1**: Ni wajibu itikadi ya mwislamu katika mizizi ya dini iwe inatokana na dalili na uthibitisho, wala haimfalii mwislamu kufuata, kwa maana ya awe anakubali maneno ya mtu yeyote kuihusu mizizi ya dini bila ya dalili.

"Amma katika hukumu za dini na matawi yake, ni wajibu aidha awe mujtahid anao uwezo wa kuziopoa hukumu kwa dalili zake, au awe anafuata, kwa maana awe anatenda matendo kwa mujibu wa rai ya mujtahid mwenye kutimiza masharti. Au awe anatekeleza majukumu yake kwa njia ya tahad- hari, kwa namna inayompatia yakini kuwa ametekeleza wajibu ipasavyo.

Kwa mfano endapo kundi la mujtahidina litatoa fatwa kuwa amali fulani ni haramu, na wengine wakatoa fatwa kuwa sio haramu, ni mustahabu kwamba atafanya tahadhari ya kutoitenda amali ile.
Na ambaye si mujtahid wala hawezi kufanya tahadhari ni wajibu juu yake amfuate mujtahid na atende kwa mujibu wa rai yake.

"**Mas'ala 4**: Kulingana na wajibu wa kumfuata aliye mjuzi zaidi, endapo kutakuwa na ugumu wa kumwainisha aliye mjuzi zaidi, itakuwa wajibu kumfuata anayemdhania kuwa ni mjuzi zaidi, bali ni wajibu kumfuata anayezingatiwa kuwa huenda akawa mjuzi kwa zingatio dhaifu la kuzidi kwake kielimu, huku ikiwa anajua kutokuwepo kwa aliye mjuzi zaidi ya yeye. Ama ikiwa kundi la watu linalingana kielimu – kwa mtazamo wake– atamfuata mmoja wao, lakini ikiwa mmoja kati yao ni mchamungu zaidi itakuwa wajibu kumfuata yeye kwa tahadhari, wala si mwingine.

"**Mas'ala 5**: Kuipata fatwa ya mujtahid na rai yake yawezekana kwa mojawapo kati ya njia nne zifuatazo:

Kusikia moja kwa moja kutoka kwa mujtahid.

Kusikia kutoka kwa waadilifu wawili wakinakili fatwa ya mujtahid.

Kusikia kutoka kwa anayeiamini kauli yake na anaitegemea nukuu yake. Kuwepo kwa fatwa kwenye risala yake ya kimatendo, kwa sura yenye matumaini ya usahihi wa yaliyopo kwenye risala, na usalama wake mbali na makosa."

Fiqhi imepiga hatua na kuwa na maendeleo kwa Shia, madrasa zimefun- guliwa na taasisi za elimu za kidini ambazo zinatoa wanachuo wataalamu wa fiqhi na mamufti, hivyo kati yao wamejitokeza wanachuo wa pekee muda wote wa historia mpaka zama hizi zilizopo. Na ambaye azifanyia rejea maktaba za kifiqhi za kishia, atasimama ameshikwa na butwaa kwenye juhudi kubwa hizo. Ninakunakilia hapa kiasi kidogo cha vitabu vya kifiqhi vya kishia.

Hivyo katika mlango wa riwaya ya kifiqhi kuna vitabu vingi vilivyo mashuhuri, miongoni mwavyo ni:

i. *Wasailus-Shia.* Jalada 20 kubwa kubwa, cha al-Huri al-Amiliy.

ii. *Mustadrakul-Wasa'ili*. Jalada 18 cha Nuriy Tabrasiy.

Na miongoni mwa vitabu vya dalili za kifiqhi ni:
i. *Jawahirul-Kalam*, cha Muhammad Hasan Najafiy, kina Jalada 43.

ii. *Hadaiqun-Nadhrah*, cha Sheikh Yusuf Al-Bahrayniy, kina Jalada 25.

iii. Mustamsikul-*Urwatul-Wuthqa*, cha Sayyid Muhsin Tabatabaiy al- Hakiim, kina Jalada 14.

iv. *Mausuatul-Fiqhiyah*, cha Sayyid Muhammad al-Husainiy as-Shiraziy, naye ni miongoni mwa wanachuoni wa wakati huu uliopo. Na enklopedia hii imepigwa chapa Jalada 110, kimechukua milango yote ya kifiq'hi, kati ya hiyo ni: Fiqhi kuhusu Qur'ani tukufu, fiqhi kuhusu haki, fiqhi kuhusu dola ya kiislam, fiqhi kuhusu idara, fiqhi kuhusu siasa, fiqhi kuhusu uchumi, na fiqhi kuhusu mambo ya kijamii.

v. Na miongoni mwa enklopedia za kisasa ni kitabu *Fiqhis-Swadiq*, cha Sayyid Muhammad Swadiq Ruhaniy, kina Jalada 26. Na *Silsilatu Yanabiul-Mawadah* cha Ali Asghari Mururidiy, kina Jalada 30.

## Mjadala Wa Yohana Na Wanazuoni Wa Madhehebu Manne:

Na tunahitimisha mlango huu kwa mjadala wa Yohana na wanavyuoni wa madhehebu manne. Nao ni miongoni mwa mijadala mizuri mno katika mlango huu. Na ni juu ya msomaji kuzingatia yaliyomo miongoni mwa hoja za hekima na madhubuti. Na tumeunakili mjadala huu kutoka katika kitabu Munadhwaratu *Fil-Imamah cha* mwandishi wake Abdullah al- Hasan.

"Yohana akasema: Nilipoona tofauti hizi kwa maswahaba wakubwa ambao hutajwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) juu ya mimbari, suala likaniwia kubwa na niligubikwa na hali ya mambo, nilikaribia kupatwa na mtihani katika dini yangu. Nikafanya safari kuelekea Baghdad, nayo ikiwa kuba ya kiislamu ili nikafanye mazungumzo ya kuhusiana na niliyoyaona, ikiwa ni tofauti za wanavyuoni wa kiislamu, ili niione haki na niifuate. Na nilipokutana na wanachuoni wa haya madhehebu manne, niliwaambia: Mimi ni mtu dhimmi, Mwenyezi Mungu ameniongoza kwenye uislamu nimesilimu na nimekujieni ili ninakili kutoka kwenu maalumati ya dini na sheria za kiislamu na Hadithi, ili nipate kuzidisha uelewa katika dini.

"Mkubwa wao ambaye alikuwa mhanafii aliniambia: 'Ewe Yohana madhehebu ya kiislamu ni manne, hivyo chagua moja kati ya hayo halafu anza kusoma utakacho.' Nilisema: Kwa hakika mimi nimeona tofauti, kwa hiyo nikajua kuwa ya haki katika hizo ni moja, hivyo basi nichagulieni muionayo kuwa ndiyo iliyo ya haki, ambayo Nabii wenu alikuwamo.

"Mhanafi akasema: 'Sisi hatujui kwa yakini hasa alivyokuwa Nabii wetu, bali tunajua kuwa njia yake haikuwa nje ya njia ya vikundi vilivyo mfarakano vya kiislamu, na sote sisi wanne kila mmoja anasema kuwa yeye ndiye aliye wa haki, lakini yawezekana akawa ndiye aliye batili, na anasema kuwa mwezake

ndiye aliye batili, lakini yawezekana akawa ndiye wa haki.

Na kwa jumla madhhebu ya Abu Hanifa ndio madhehebu yaliyo sawa, na ni yenye kutenda kwa mujibu wa Sunna, na yenye kuafikiana mno na akili, na ni ya hali ya juu mno kwa watu, kwa kweli madhhebu yake ndio chaguo la umma mwingi bali ni chaguo la masultani wa umma. Hivyo basi shikamana nayo utaokoka.'

"Yohana akasema: Imam wa kishafii alipiga mayowe, ninadhani kulikuwa na mzozo kati ya mshafii na mhanafii, akamwambia: 'Nyamaza usitamke, umesema uwongo na umezua. Wewe una haki gani ya kupambanua kati ya madhehebu, na kuwapa uzito mamujtahid? Ole wako mama yako akuhuzunikie, wapi wewe na kufahamu aliyosema na aliyokisia kwa rai yake. Kwa kweli yeye ni yule aliyeitwa mzee wa rai, anajitahidi kuikabili *Nasu,* anapendekeza katika dini ya Mwenyezi Mungu na kuyatendea kazi mapendekezo, mpaka rai yake dhaifu ilimfanya aseme:

"'Lau mtu afunge ndoa ya kisheria na mwanamke, naye akiwa katika nchi ya India na mwanamke yuko Roma – Italia – halafu akamwendea mke baada ya miaka, na amkute na mimba na mbele yake kuna watoto wanaotembea, halafu amwambie mke wake: Ni akina nani hao? Aseme: Ni wanao.

Hapo kwa hilo mume amfikishe mke mbele ya Kadhi wa Kihanafii. Yule Kadhi atoe hukumu kuwa watoto ni kutoka mgongoni mwake, na hapo wanaungana na yeye katika hali ya dhahiri na ya batini, atawarithi na watamrithi. Yule mtu aseme: Itakuwaje hivi na sikupata kumkurubia katu? Kadhi atasema: Inawezekana kuwa ulipatwa na janaba au iwe ulitokwa na manii hivyo manii yako yaliruka katika kipande na kuingia kwenye utupu wa huyu mwanamke.'73 Ewe mhanafii! Hivi maamuzi haya ndio yanalingana na Kitabu na Sunna?

"Mhanafii akasema: Ndio huambatanishwa naye kwa sababu yeye ni tandiko lake, na tandiko huambatanishwa na hukutanishwa na ndoa, wala katika hilo hakuna sharti la kumwingilia. Nabii (s.a.w.w) amesema: "Mtoto ni wa tandiko na mzinzi lake ni jiwe." Shafii alizuia liwe tandiko bila ya kuingilia. Hapo mshafii alimshinda mhanafii kwa hoja na akazuia kupatikana tandiko bila kujamiana.

"Halafu mshafii akasema: Na Abu Hanifa akasema: 'Lau mwanamke amepelekwa kwa mumewe, mtu mwingine akamuashki na kufikisha malalamiko kwa Kadhi wa kihanafii kuwa, yeye alifunga ndoa naye kabla ya mtu ambaye mke amepelekwa kwake, na mlalamikaji akatoa rushwa kwa mafasiki wawili, na wao mafasiki wakatoa ushahidi kuthibitisha madai yake ya uwongo, na Kadhi akapitisha hukumu kuwa mke ni wake, basi hapo mwanamke anakuwa haramu kwa mume wake wa kwanza katika hali ya dhahiri na batini. Na ndoa inathibiti kwa huyu wa pili, na kuwa mwanamke anakuwa halali kwake dhahiri na batini, na anakuwa halali kwa mashahidi ambao walifanya makusudi kutoa ushahidi wa uwongo.'74 Hebu angalieni ee ninyi watu! hivi hii ni madhehebu ya mwenye kujua sheria za kiislam?

"Mhanafii akasema: 'Hapana upinzani na wewe, kwetu sisi ni kuwa hukumu ya Kadhi inapita dhahiri na batini, na hili ni tawi latokana na hiyo.'

“Mshafii alikuwa hasimu na alikataa kupita kwa hukumu ya Kadhi dhahiri na batini, kwa kauli yake (s.w.t.): **“Na wahukumuni baina yao kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu.**” (***Sura Maidah*****: 49)**, na Mwenyezi Mungu hajateremsha hilo.

“Kisha mshafii akasema: Na Abu Hanifa amesema: ‘Lau itokee mume wa mwanamke ameghibu habari zake zikosekane, mtu mwingine akaja na kumwambia: Mumeo amekufa kaa eda, akakaa eda, halafu baada ya eda mtu mwingine akafunga ndoa naye na akamwingilia, na watoto wazaliwe, halafu yule mtu wa pili aghibu na kudhihiri uhai wa mtu wa kwanza na kufika kwake, watoto wote wa mtu wa pili ni watoto wa mtu wa kwanza, atawarithi na watamrithi.’75 Enyi wenye akili, aseme kauli hii mwenye uelewa na utambuzi?

“Mhanafii akasema: Kwa kweli amechukua kauli hii kutokana kwenye kauli ya Nabii (s.a.w.w.): “Mtoto ni wa tandiko na mzinzi lake ni jiwe.” Hapo mshafii alimtolea hoja kuwa tandiko ni kwa sharti ya kuingilia, na hatimaye akamshinda.

“Halafu mshafii akasema: Imam wako amesema: ‘Mwanaume yeyote akimwona mwanamke mwislamu akadai kwa Kadhi kuwa mumewe alimtaliki, na akaja na mashahidi wawili, wakashuhudia kwa ajili yake kwa uwongo, Kadhi akahukumu kuwa amepewa talaka, atakuwa haramu kwa mumewe, na itakuwa ruhusa kwa mdai amuowe, pia hata wale mashahidi.’76 Na alidai kuwa hukumu ya Kadhi inapita dhahiri na batini.

“Kisha mshafii akasema: Amesema Imam wako: ‘Wakitoa ushahidi watu wanne kuwa mtu fulani amezini, akiwakubali kuwa wamesema kweli, hadi itaporomoka haitothibiti juu yake, haitolazimu afanyiwe hadi ya kisheria, na akisema kuwa ni waongo, na endapo atawakadhibisha itamlazimu, na hadi itathibiti.’77 Basi zingatieni wenye uoni.

“Kisha mshafii akasema: Na Abu Hanifa amesema: ‘Lau mtu akimlawiti mvulana mdogo na kumwingiza, haitokuwa hadi juu yake, bali huadhibiwa.’78 Hali Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) amesema:

‘Mwenye kutenda tendo la kaumu ya Lut muuweni mtenda na mtendewa.’79

“Abu Hanifa amesema: ‘Endapo mtu akipora ngano na akaisaga atakuwa ameimiliki kwa kuisaga. Endapo mwenye ngano akitaka kuuchukua unga wake na ampe ujira aliyeipora, si wajibu juu ya mporaji kuitika, na anaweza kukutaa. Na iwapo mwenye ngano akiuliwa basi damu yake ni bure (haina fidia), na lau mwenye ngano atamuuwa mporaji, basi naye atauliwa kwa kumuua.’80

“Na amesema Abu Hanifa: ‘Lau mwizi akiiba Dinari elfu moja, na akaiba elfu zingine kutoka kwa mtu mwingine, na akazichanganya atakuwa amezimiliki zote, na itamlazimu badali yake.’

“Abu Hanifa amesema: ‘Lau mwislamu mcha-mungu mwanachuoni akimuuwa kafiri jahili, basi mwislamu atauliwa kwa ajili yake. na Mwenyezi Mungu anasema:

وَلَنْ يَجْعَلَ اللَّهُ لِلْكَافِرِينَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ سَبِيلًا {141}

***"Mwenyezi Mungu hatowajaalia makafiri njia ya kuwashinda waumini."*** (***Sura Nisaa: 141***)*.'*

"Na amesema Abu Hanifa: 'Lau mtu akimnunua mama yake au dada yake na akawaingilia, haitokuwa juu yake Hadi japokuwa alikuwa anajua na akafanya hivyo makusudi.'[81]

"Abu Hanifa anasema: 'Endapo mtu akifunga ndoa na mama yake au dada yake akiwa anamjua kuwa ni mama yake au ni dada yake, na akamwingilia haitokuwa Hadi dhidi yake, kwa sababu ni ndoa ya *shubha.*'[82]

"Abu Hanifa amesema: 'Lau mtu alale ukingoni mwa bwawa la kileo akapinduka akiwa usingizi, na kutumbukia ndani ya bwawa, janaba yake itatoweka na atakuwa tohara.'

"Amesema Abu Hanifa: 'Nia si wajibu katika wudhu,[83] wala katika kuoga.'[84] Hali imekuja katika Hadithi Sahihi: 'Amali haiwi ila kwa nia tu.'[85]

"Abu Hanifa amesema: 'Bismillahi sio wajibu katika Sura Al-Fatiha.'[86]

Na ameiondoa kutoka katika Sura Al-Fatiha japokuwa makhalifa waliiandika katika misahafu baada ya Qur'ani kuhaririwa.

"Abu Hanifa amesema: 'Lau ngozi ya mbwa aliyekufa ikichunwa na kudibaghiwa itatoharika, anaweza mtu kunywa humo na kuivaa wakati wa kuswali.'[87] Na hii ni kinyume na agizo la wazi, lisemalo kuwa mbwa dhati yake ni najisi, ambalo linaharamisha kunufaika naye kwa njia zote.

"Halafu akasema: 'Ewe Hanafii, katika madhehebu yako inamfalia mwislamu akitaka kuswali atawaze kwa mvinyo, na aanze kuosha miguu yake, na amalizie mikono yake,[88] na avae ngozi ya mzoga wa mbwa iliyosindikwa,[89]na asujudu juu ya kinyesi kikavu, na afanye takbira kwa Kihindi, na asome Sura Al-Fatiha kwa Kiebrania,[90] na aseme baada ya Sura Al-Fatiha: *'Dou bargh sabzi*.' yaani ikimaanisha: *Mudhamatani.* Halafu arukuu na wala asiinue kichwa chake, kisha asujudu na atenganishe kati ya sijda mbili kwa kiasi cha ukali wa upanga, na kabla ya salamu ajambe makusudi.

Hapo Swala yake ni sahihi, na endapo atajamba kwa kusahau, swala yake itabatilika.'[91]

"Kisha akasema: Ndio inafaa hivi, zingatieni ee wenye uoni. Je yafaa kuabudu kwa ibada kama hii? Au inafaa Nabii auamrishe umma wake ibada kama hii, huku ni kumzulia Mwenyezi Mungu na Mtume Wake!

"Mwanachuoni wa kihanafii akakwama bila jibu, hivyo alighadhibika na akasema: 'Ewe mshafii fupisha Mwenyezi Mungu aupasue mdomo wako. Wewe una upeo gani wa kumkosoa Abu Hanifa? Umbali ulioje kati ya madhehebu yako na yake! Madhehebu yako yanalingana mno na madhehebu ya Majusi, kwa

kuwa katika madhehebu yako mtu anaweza kumuoa binti yake aliyezaliwa kwa njia ya zinaa na pia dada yake.

Na anaweza kuwaoa madada wawili waliotokana na zinaa. Na anaweza kumuoa mama yake aliyezaliwa kwa zinaa.92 Pia shangazi yake na mama yake mdogo waliozaliwa kwa zinaa. Hali Mwenyezi Mungu anasema:

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أُمَّهَاتُكُمْ وَبَنَاتُكُمْ وَأَخَوَاتُكُمْ وَعَمَّاتُكُمْ{23}

***"Mmeharamishiwa mama zenu na mabinti zenu na dada zenu na shangazi zenu na dada wa mama zenu"*** (***Sura Nisai: 23***).

"Na hizi ni sifa za dhati hazibadiliki kwa kubadilika sheria na dini, wala usidhanie ewe mshafii, ewe mpumbavu kuwa kuzuilika kwao kurithi kunawatoa nje ya sifa hizi za dhati za ukweli, na kwa ajili hiyo ndio maana huegemezwa nazo, husemwa: Binti yake na dada yake wa zinaa, na kuletwa sifa hii si kwa sababu ya umajazi wake, kama katika kauli yetu: Dada yake wa nasaba, bali hiyo ni kwa sababu ya kufafanua.

"Na uharamu unamuingiza yule ambaye haya matamko huwa ni kielelezo kwake kwa namna ya hakika na majazi, kwa ijmai. Kwa kuwa bibi anaingia chini ya mama kwa ijmai, hivyo hivyo binti wa binti, wala hapana tofauti kuwa wao ni haramu kwa mujibu wa Aya hii. Hivyo basi angalieni enyi wenye akili, haya si lolote ila ni madhehebu ya Majusi, ewe Kharijiy.

"Ewe mshafii! Imamu wako amewahalalishia watu kucheza Shatranji,93 hali ikiwa Nabii (s.a.w.w) amesema: 'Haipendi Shatranji ila mwabudia sanamu.' Ewe mshafii! Imamu wako amewahalalishia watu kucheza ngoma na kupiga dufu na kupiga firimbi ya matete94**,** Mwenyezi Mungu ameifanya mbaya madhehebu yako, mtu anamuoa humo mama yake, dada yake, na anacheza Shatranji, na anacheza ngoma na anapiga dufu.

Hili si jambo lingine ila ni kumzulia Mwenyezi Mungu na Mtume Wake uongo. Hajiambatanishi na madhehebu hii ila kipofu wa moyo na aliye kipofu wa haki.'

"Yohana akasema: Mjadala kati yao ulikuwa mrefu mhanbali alijihami dhidi ya mshafii na mmaliki alijihami dhidi ya mhanafii. Mzozo uliibuka kati ya mmaliki na mhanbali. Na ilikuwa lililoibuka kati yao ni kuwa mhanbali akasema: 'Kwa kweli Malik amefanya bidaa katika dini, bidaa ambayo Mwenyezi Mungu amezihilikisha kwa ajili yake umma kadhaa, na yeye ameihalalisha. Na yenyewe ni kuhalalisha kumlawiti mvulana, kumlawiti mtwana. Hali ikiwa imethibiti habari sahihi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) amesema: 'Mwenye kumlawiti mvulana wauweni mtenda na mtendwa.'95

"Na mimi nimemuona mwana madhehebu ya Malik akimlalamikia mtu kwa Kadhi kuwa alimuuzia mtwana ambaye hawezi kumwingilia. Kwa hiyo Kadhi alithibitisha kuwa ni aibu ya mtwana na

anaruhusiwa kumrudisha.

Je humuonei haya Mwenyezi Mungu ewe mfuasi wa Maliki kuwa uko katika madhehebu kama hii, na wewe wasema: Madhehebu yangu ni bora kuliko madhehebu yako? Na imamu wako amehalalisha nyama ya mbwa, hivyo Mwenyezi Mungu ameifanya madhehebu yako na itikadi yako kuwa mbaya mno.'

"Mfuasi wa Malik naye akamrudia na kumkaripia: 'Nyamaza ewe unayeamini kuwa Mwenyezi Mungu ana mwili, ewe unayeamini kuwa Mwenyezi Mungu huingia katika mwili wa kiumbe mfano wa binadamu, ewe fasiki, madhehebu yako ni mbaya mno na inafaa kukimbiwa.

Kwa kuwa imamu wako Ahmad bin Hanbali anaamini kuwa Mwenyezi Mungu ni mwili unaoketi juu ya Arshi na inamzidi sawa na vidole vinne.

Na kuwa yeye kila usiku wa Ijumaa huteremka kutoka mbingu ya dunia na anakuwa juu ya paa za misikiti akiwa katika sura ya kijana asiye kuwa na ndevu, mwenye nywele fupi, akiwa na ndara mbili, kanda zake ni za lulu zenye ubichi, akiwa amepanda punda mwenye kishungi juu ya paji.'96

"Yohana akasema: Uliibuka mzozo kati ya mhanbali na mmaliki, mshafii na mhanafi. Sauti zao zilipanda, walidhihirisha maovu na aibu zao kiasi kwamba wote waliohudhuria maneno yao waliona vibaya yaliyojitokeza kwao, na walio wengi waliwaaibisha.

"Niliwaambia: Polepole, na ninaapa wallahi kwa kweli mimi nimezichukia itikadi zenu, ikiwa huu ndio uislamu basi ole wake, ubaya ulioje! Lakini mimi namuapa Mwenyezi Mungu kwenu ambaye hapana Mungu isipokuwa ni Yeye, kateni mjadala huu na muondoke, kwa kuwa walio wengi katika watu wamewachukieni.

"Yohana akasema: Walisimama na kutawanyika na walibaki kimya wiki hawatoki nje ya nyumba zao, watokapo hawakubaliki kwa watu.

Kisha baada ya siku kadhaa walifanya suluhu na walikutana pale Mustanswiria, na niliwaendea asubuhi na kuketi nao, na miongoni mwa yaliyojiri niliwaambia: Nilikuwa namtaka mwanachuo miongoni mwa wanavyuoni wa Rafidhu, tumjadili kuhusu madhehebu yake. Je mtatuletea mmoja kati yao tujadiliane naye?

"Wanazuoni wakasema: Oh! Yohana, Rafidhu ni kikundi cha watu wachache hawawezi kujitokeza kati ya waislamu kwa uchache wao, na kukithiri kwa walio kinyume nao, wala hawajidhihirishi sembuse kuweza kuhojiana na sisi juu ya madhehebu yao, wao ni wapotovu wachache hali walio hitilafu nao ni wengi.

"Yohana akasema: Hiyo ni sifa njema kwao, kwa kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amewasifu wachache kwa sifa njema, na amewalaumu wengi kwa kauli yake:

وَقَلِيلٌ مِنْ عِبَادِيَ الشَّكُورُ {13}

***"Na ni wachache wanaoshukuru katika waja wangu."*** (***Sura Saba'a: 13***)

وَمَا آمَنَ مَعَهُ إِلَّا قَلِيلٌ {40}

***"Na hawakuamini pamoja naye ila wachache."*** (***Sura Hud: 40***).

وَإِنْ تُطِعْ أَكْثَرَ مَنْ فِي الْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ ۚ{116}

***"Na kama ukiwatii wengi katika waliomo ulimwenguni watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu."*** (***Surat An'aam: 116***)

وَلَا تَجِدُ أَكْثَرَهُمْ شَاكِرِينَ {17}

***"Wengi katika wao hutawakuta ni wenye kushukuru."*** (***Sura A'arafu: 17***)

وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَشْكُرُونَ {243}

***"Lakini watu wengi hawashukuru."*** (***Surat Al-Baqara: 243***)

وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ {37}

***"Lakini wengi wao hawajui."***(***Surat An'aam: 37***)

وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يُؤْمِنُونَ {1}

***"Lakini watu wengi hawaamini"*** (***Sura Raadu: 1***).

Na zisizo kuwa hizo miongoni mwa Aya.

“Wanavyuoni wakasema: Oh! Yohana, hali yao ni kubwa mno si ya kuelezwa. Kwa kuwa sisi lau tungemjua mmoja wao tungemuwinda mpaka tumuue. Kwa kuwa wao kwetu ni makafiri, damu zao kwetu ni halali, na katika wanavyuoni wetu kuna anayetoa fatwa uhalali wa mali zao na wanawake wao.

“Yohana akasema: Allahu Akbar, hili ni jambo adhim, waona wanastahiki hivyo, je wao hawazitambui Shahada mbili?

Wakasema: Hapana.

Akasema: Hivi wao hawaelekei kibla ya waislamu?
Wakasema: Hapana.

Akasema: Hivi wao hawaitambui swala au swaumu au Hijja au Zaka au Jihadi?

Wakasema: Hapana, lakini wao wanaswali, wanafunga, wanatoa Zaka, wanahiji na wanapigana Jihadi.

Akasema: Hivi wao hawatambui kukusanywa siku ya Kiyama na kufufuka, swiratu, mizani, na uombezi?

Wakasema: Wanakiri hayo kwa sura muwafaka kabisa.

Alisema: Je wao wanahalalisha zinaa, ulawiti, kunywa pombe, riba, zumari na aina zingine za starehe?

Wakasema: Wanajiepusha na hayo na wanayaharamisha.

Yohana akasema: Oh! Mungu wangu, ajabu ilioje, kaumu ya watu wanashuhudia shahada mbili, na wanaswali kuelekea kibla, wanafunga mwezi wa Ramadhani na wanahiji nyumba tukufu, na wanasema kuwa kukusanywa na kufufuka vipo hivyo, na pia ufafanuzi wa hesabu, vipi mali zao, damu zao na wanawake wao wawe halali, hali Nabii wenu anasema:

‘Nimeamriwa kuwapiga vita watu mpaka washuhudie kuwa hapana Mola wa haki apasaye kuabudiwa ila Allah mmoja. Na kuwa hakika Muhammad ni Mtume wa Allah.

Wakisema watahifadhika na mimi, damu zao, mali zao na wanawake wao ila kwa haki na hesabu yao ni kwa Mwenyezi Mungu.’97

Wanazuoni wakasema: Ewe Yohana! kwa kweli wao wamefanya bidaa katika dini, miongoni mwazo ni kuwa, wao wanadai eti Ali (a.s.) ni mbora katika watu baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), na wanamboresha kuliko makhalifa watatu.

Hali ikiwa awamu ya kwanza waliafikiana kuwa mbora katika makhalifa ni mkubwa wa Taymu.

Yohana akasema: Mwaona mtu akisema kuwa Ali ni mbora kuliko Abu Bakr anafaa kukufurishwa?

Wakasema: Ndio, kwa kuwa yeye amekhalifu Ijmai.

Yohana akasema: Mwasema nini kumhusu msimulizi wenu wa Hadithi al- Hafidhu Abu Bakr Ahmad bin Musa bin Mardawayhi? Wanazuoni wakasema: Yeye ni mwaminifu, inakubalika riwaya yake, ni mfano sahihi.

Yohana akasema: Hiki hapa kitabu chake kiitwacho *Kitabul-Manaqib*, imeelezwa humo kutoka kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) kuwa amesema: "Ali ni mbora wa binadamu, na atakayekataa amekufuru." Pia katika kitabu chake kuna habari kuwa Hudhaifa alimuuliza Ali (a.s.). Akajibu: "Mimi ni mbora wa umma huu baada ya Nabii wake, wala hawi na shaka na hilo ila Mnafiki."

Pia katika kitabu chake kuna habari kutoka kwa Salman, kutoka kwa Nabii (s.a.w.w.) kuwa yeye alisema: "Ali bin Abu Talib ni mbora wa ninaowaacha baada yangu."

Pia katika kitabu chake kuna habari kutoka kwa Anas bin Malik kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: "Ndugu yangu, waziri wangu na aliye mbora ninayemwacha Khalifa baada yangu ni Ali bin Abu Talib."

Na kutoka kwa Imam wenu Ahmad bin Hanbal ameeleza katika *Musnad* yake kuwa Nabii (s.a.w.w.) alimwambia Fatima: "Je huridhiki kuwa mimi nimekuozesha kwa wa kwanza kusilimu katika umma wangu, na aliye na elimu nyingi zaidi yao, na mwenye saburi mno zaidi yao."[98]

Na pia imeelezwa katika *Musnad* ya Ahmad bin Hanbal kuwa Nabii (s.a.w.w) alisema: "Ewe Allah niletee kiumbe wako mpendwa mno kwako."[99]Akamjia Ali bin Abu Talibi, hiyo ni katika Hadithi ya ndege. Na Hadithi hii ameieleza Nasaiy na Tirmidhiy katika sahihi zao.[100] na hao wawili ni miongoni mwa wanachuoni wenu.

Na Akhtab Khawarzamiy ameeleza katika kitabu *al-Manaqib*, na yeye ni miongoni mwa wanavyuoni wenu, ameeleza kutoka kwa Muadhu bin Jabal, akasema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: "Ewe Ali nakugomba kwa unabii wala hapana unabii baada yangu, na unawagomba watu kwa mambo saba wala hatokuhoji yeyote miongoni mwa makuraishi: Wewe ni wa kwanza wao katika kumwamini Mwenyezi Mungu, na umtekelezaji mno wa amri za Mwenyezi Mungu na ahadi Zake kuliko wao, na mwenye kugawa kwa sawa zaidi kuliko wao, na ni mwadilifu mno kwa raia kuliko wao, na ni mtambuzi mno wa hukumu kuliko wao, na una adhama kubwa mno kwa Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama katika hitari kuliko wao."[101]

Na amesema mwandishi wa kitabu *Kifayatut-Talib* ambaye ni miongoni mwa wanazuoini wenu: "Hadithi hii ni nzuri ya hali ya juu. Na ameieleza al-Hafidh Abu Nua'im katika *Hilyatul-Awliyai*."[102]
Yohana akasema: Enyi maimamu wa kiislamu Hadithi hizi sahihi zimeelezwa na maimamu wenu, nazo zinaeleza kwa usafi kabisa utukufu wa Ali na ubora wake kuliko watu wote, Rafidhu dhambi yao ni nini?! Dhambi ni ya wanavyuoni wenu tu na ambao wanaoeleza riwaya zisizo za kweli na wanamzulia uwongo Mwenyezi Mungu (s.w.t.) na Mtume Wake!

Wakasema: Ewe Yohana, wao hawakueleza lisilo kweli, na wala hawakuzua Hadithi, lakini Hadithi zina taawili na maelezo.

Yohana akasema: Taawili gani itaafikiana na Hadithi hizi kwa kumhisisha binadamu. Kwa kuwa zimebainisha kuwa yeye ni bora kuliko Abu Bakr, ila ikiwa mtamtoa Abu Bakr katika jumla ya binadamu, hapo tutasalimu amri kuwa Hadithi hazijulishi maana hiyo, hebu nipeni habari ni yupi kati yao aliyepigana jihadi zaidi?

Wakasema: Ni Ali.
Yohana akasema: Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema:

وَفَضَّلَ اللَّهُ الْمُجَاهِدِينَ عَلَى الْقَاعِدِينَ أَجْرًا عَظِيمًا {95}

***"Lakini Mwenyezi Mungu amewatukuza kwa malipo makubwa wenye kupigana jihadi kuliko wenye kukaa."*** (***Sura Nisa'a: 95***)

Na hili ni tamko safi lisilokuwa na maana mchanganyiko.

Wakasema: Abu Bakr pia ni mpiganaji, hivyo basi hailazimu Ali awe bora kuliko yeye.

Yohana akasema: Jihadi chache inapolinganishwa na jihadi nyingi, huwa sawa na kukaa! Fanya kuwa wako sawa, basi mnakusudia nini mnaposema huyu ni mbora?

Wakasema: Ni yule ambaye sifa za ukamilifu na ubora wa kimaumbile na wa kuchuma vimekusanyika kwake, kama vile kuwa na utukufu wa asili, elimu, zuhdi, ushujaa, ukarimu na yanayotokana na hayo.

Yohana akasema: Fadhila hizi zote ni za Ali (a.s.), kwa namna bora kuliko kupatikana kwa mtu mwingine!

Yohana akasema: Ama kuhusu utukufu wa asili yake, yeye ni mwana wa ami yake Nabii (s.a.w.w.) na ni mume wa binti yake, na baba wa wajukuu zake wawili. Ama kuhusu elimu Nabii (s.a.w.w) amesema: "Mimi ni Jiji la elimu na Ali ni lango lake." Na imekubalika kiakili kuwa mtu hawezi kufaidika kitu na Jiji ila ikiwa atachukua kutokea langoni, hivyo basi njia ya kufaidika na Nabii (s.a.w.w) haiwi ila kupitia Ali (a.s.). Na hii ni daraja ya juu!

Na amesema (s.a.w.w): "Kadhi wenu hasa ni Ali." Hivyo mwenye kuhukumu kiadilifu zaidi kati yenu ni Ali, na kwake huchimbuka kila kadhia, na hutokomea kwake kila mfarakano, na huelemea kwake kila kundi.

Hivyo basi yeye ndio kilele cha kila fadhila na chemchemu yake, na ni mahali pa kujifunza, na mahali pa mkusanyiko wake, kila mwenye kuzidi uhodari humo basi ni kutoka kwake amechukua, na nyayo zake

amefuata, na mfano wake ameiga. Na mmetambua kuwa elimu iliyo na utukufu mno ni elimu ya Kiungu. Na kutoka katika maneno yake imedondolewa (elimu ya Kiungu), na kutoka kwake imenakiliwa na, kwake yeye ndio mwanzo.

Kwa kweli Muutazila ambao ndio watu wa mijadala, kutoka kwao watu wamejifunza fani hii, wao ni wanafunzi wake. Kwa kuwa mkuu wao Wasil bin Atwa ni mwanafunzi wa Abu Hashim Abdullah bin Muhammad Ibnu Al-Hanafiyah.[103]
Na Abu Hashim Abdullah ni mwanafunzi wa baba yake, na baba yake ni mwanafunzi wa Ali bin Abu Talib (a.s.).

Ama Ashairah kwa kweli wao wanaishia kwa Abul Hasan al-Ash'ariy, naye ni mwanafunzi wa Abu Ali al-Jubaiy, naye ni mwanafunzi wa Wasil bin Atwa.[104]

Ama Imamia na Zaydia kuishia kwao kwake ni jambo halina kificho. Ama kuhusu elimu ya fiqhi, yeye ndio asili yake na ndio msingi, na kila mwanafiqhi katika uislamu, kwake ndio ajipa utukufu.

Ama Malik amechukua fiqhi kutoka kwa Rabiatur-Raay, na yeye ameichukua kutoka kwa Ikrimah, na yeye ameichukua kutoka kwa Abdullah, naye ameichukua kutoka kwa Ali. Ama Abu Hanifa, yeye ameichukua kutoka kwa Sadiq (a.s.). Na Shafii ni mwanafunzi wa Malik. Na Hanbali ni mwanafunzi wa Shafii.[105]

Ama wanavyuoni wa kishia kurejea kwao kwake ni dhahiri. Ama wanafiqhi wa kiswahaba kurejea kwao kwake ni dhahiri pia, kama vile Ibnu Abbas na wengine. Acha kauli ya Umar si mara moja: "Mtu yeyote asitoe fatwa msikitini ikiwa Ali yupo." Na kauli yake: "Nisibakiye kwenye tatizo bila ya Abul Hasan kuwepo."[106] Na kauli yake: "Lau si Ali Umar angeangamia."[107]

Na Tirmidhiy amesema katika *Sahihi* yake na al-Baghawiy, kutoka kwa Abu Bakr, amesema: "Anayetaka kumtizama Adam katika elimu yake, na Nuhu katika fahamu yake na Yahya bin Zakariya katika utawa wake na Musa bin Imraan katika ushupavu wake, basi amtizame Ali bin Abu Talib."[108]

Na al-Bayhakiy amesema kwa sanad yake kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Atakaye kumtizama Adam katika elimu yake, Nuhu katika uchamungu wake, Ibrahim katika uvumilivu wake, Musa katika haiba yake na Isa katika ibada yake, basi amtizame Ali bin Abu Talib."[109]

Na yeye ndiye aliyebainisha hadi ya unywaji pombe.[110] Na ambaye ametoa fatwa kuhusu mwanamke aliyejifungua akiwa na mimba ya miezi sita.[111]

Na ugavi wa pesa kwa mwenye mikate.[112] Na ni mwenye kutoa amri ya kuchanwa mtoto nusu mbili.[113]

Na ni mwenye kuamuru akatwe shingo mtumwa. Na ndiye aliye hukumu kumhusu mwenye vichwa viwili.[114] Na aliyebainisha hukumu ya wazinzi.[115] Na yeye ndiye aliyetoa fatwa kumhusu mwenye mimba aliyezini.[116]

Na miongoni mwa elimu ni elimu ya tafsiri, watu wameijua hali ya Ibnu Abbas katika hilo, na yeye alikuwa mwanafunzi wa Ali (a.s.), aliulizwa na kuambiwa: "Ni kwa kiwango gani elimu yako kwa kuilinganisha na ya mwana wa ami yako?" Akasema: "Ni sawa na tone la mvua katika bahari kubwa."117

Na miongoni mwa elimu ni elimu ya Tariqa na ya hakika, na elimu ya Tasawwuf, na mnajua kuwa mabwana wa fani hii katika nchi zote za kiislam wanaishia kwake. Na kwake wanasimama, na hilo amelieleza wazi Shibliy na Hanbali na Sirriy as-Saqtiy na Abu Zayd al-Bastaamiy na Abu Mahfudh maarufu kwa jina la al-Karkhiy na wengine. Na itakutosheni kuwa dalili juu ya hilo ile al-Khirqa, kitambaa ambacho ni kauli mbiu yao, na kuwa wao huziegemeza kwa sanadi inayoashiria kutoka kwake, na kuwa yeye ndio mwanzilishi wake.118

Na miongoni mwa elimu ni elimu ya Nahau na ya Kiarabu, na watu wote wanajua kuwa yeye ndiye aliyeiasisi na kuianzisha, na alimfanyia imla Abul-Aswad Duwaliy, kwa kweli ni majumuu inayokaribia kuunganishwa na miujiza, kwa kuwa nguvu za kibinadamu hazitoshelezi udondozi kama huu.

Yuwapi mwenye sifa kama hizi kwa kumlinganisha na mtu wanayemuuliza nini maana ya 'Malisho', anasema: "Sisemi kuhusu Kitabu cha Mwenyezi Mungu kwa rai yangu." Na huyo huyo anapitisha amri ya mirathi ya babu, amri mia moja zinazopingana, na anasema: "Nikipotoka ninyoosheni na nikinyoka nifuateni."119

Je mwenye akili timamu anaweza kumlinganisha mfano wa mtu huyu na anayesema: "Niulizeni kabla hamjanikosa, niulizeni njia za mbinguni wallahi mimi ni mjuzi wa njia hizo kuliko njia za ardhini!" Na akasema: "Kwa kweli hapa pana elimu nyingi." Na alipiga kwa mkono wake kifua chake, na akasema: "Hata pazia iondolewe sitozidi yakini." Imedhihirisha kuwa ni mwanachuo.120

Ama kuhusu zuhdu, kwa kweli yeye ni bwana wa wanazuhdi wote. Yeye ni badala wa badala, na kuelekea kwake misafara hufanywa, na hupunguzwa nguo, na wala hakupata kushiba chakula katu, na alikuwa mvaaji wa magwanda zaidi kuliko watu na mlaji wa chakula cha kawaida.

Abdullah bin Ubay Rafiu amesema: "Niliingia kwa Ali (a.s.) siku ya Idi akaleta chakula jina lake Jirabu, akakuta humo muna mkate wa shairi, mkavu uliovunjwavunjwa, akaja na akaula.
Nilisema: 'Ewe Amirul- Muuminina, vipi unauona mzuri, nao ni mkate wa shairi?' Akasema: Niliwaogopa hawa watoto wawili wanauchanganya na mafuta au samli."'

Na nguo yake ilikuwa na viraka vya ngozi, mara nyingine na kumbi. Na ndara zake ni za kumbi. Na alikuwa anavaa nguo ya pamba nene, na endapo atakuta mikono ya shati lake imerefuka huikata kwa kitu chenye makali na huiacha bila kuishona, na hubakia kwenye dhiraa zake mpaka hubakia tupu bila ya nyama.

Na alikuwa anapotowea hutowea kwa siki na chumvi, na ikiwa atapanda kwa kitoweo cha hali ya juu zaidi ya hicho basi huwa ni kwa baadhi ya mboga mboga za mimea ya ardhi, na akipanda juu kidogo

huwa kwa maziwa ya ngamia kidogo, na alikuwa hali nyama ila kidogo na alikuwa akisema: “Musiyafanye matumbo yenu kuwa makaburi ya wanyama.” Pamoja na hayo yote alikuwa mtu mwenye nguvu mno na mkono mtukufu mno.121

Ama upande wa ibada, ni kutoka kwake watu wamejifunza swala za usiku, na kujilazimisha na nyiradi, na kiyamu ya swala za Sunna. Wamdhania nini mtu ambaye bapa la uso wake lilikuwa kama goti la ngamia, na kwa kudumisha kuhifadhi nyiradi zake alitandaza nguo ya ngozi kati ya swafu mbili usiku wa mapambano ya vita ya Swifiini, akawa anaswali juu yake na mishale inamdondokea na yapita kwenye masikio yake, kushoto kulia, wala hasimami mpaka alipomaliza wadhifa wake.

Na wewe endapo utazingatia dua zake na faragha zake na ukafahamu yaliyomo humo kati ya kumuadhimisha Mwenyezi Mungu (s.w.t.) na kumtukuza na yaliyokuwemo kati ya unyenyekevu wake mbele ya haiba Yake Mungu – na kuinyenyekea enzi Yake, ungejua ikhlaswi aliyokuwanayo.

Zaynul-Abidina (a.s.) alikuwa anaswali usiku mmoja rakaa elfu, na alikuwa anasema: “Wapi mimi na ibada ya Ali (a.s.).”122

Ama kuhusu ushujaa, yeye ni mwana mzoefu wa mambo, amewafanya watu katika ushujaa wasahau kuwakumbuka waliokuwa kabla yake, na amefuta jina la watakaokuja baada yake. Na nafasi yake, kwenye medani za vita ni mashuhuri hupigiwa mfano mpaka siku ya Kiyama. Yeye ni shujaa ambaye katu hajapata kukimbia, wala kufadhaishwa na kikosi, wala hakukabiliana na yeyote ila humuua, wala hajampiga pigo adui katu na ikawa lahitajika la pili.

Imekuja katika Hadithi: Akipiga na kushinda hukata, na akipiga na kupata upinzani humega.

Katika Hadithi: Mapigo yake yalikuwa witri123 – yaani moja moja, na ilikuwa washirikina wakimuona vitani wanausiana wao kwa wao, na kwa upanga wake limeimarika jengo la dini na nguzo zake zimekuwa imara.

Malaika walistaajabishwa na ukali wa mapigo na mashambulizi yake.

Na katika vita vya Badr ambavyo ni msiba mkubwa kwa waislamu, aliwaua katika vita hivi mabingwa wa kikuraishi, mfano wa Walid bin Utbah na al-Aswi bin Said, Nawfal bin Khuwailid ambaye aliwakuta Abu Bakr na Talha kabla ya hijra na kuwaadhibu. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) akasema: “Sifa njema ni zake Allah ambaye ameitika ombi langu kumhusu huyu.”124Aliendelea katika hilo anampiga bingwa mmoja baada ya mwingine mpaka aliwauwa nusu ya waliouawa, na idadi yao walikuwa sabini. Na waislamu wote pamwe na malaika elfu tatu washambulizi waliwaua nusu ya waliobaki, na katika hilo Jibril alinadi:

**“Hapana upanga isipokua *Dhul-Fiqar* wala kijana ila Ali. “**

Na siku ya Uhud walipomkimbia waislamu Nabii (s.a.w.w) na Mtume wa Mwenyezi Mungu kutupwa chini, washirikina walimpiga kwa panga na mikuki, Ali (a.s.) akiwa amechomoa upanga wake mbele

yake, Nabii (s.a.w.w) aliangalia baada ya kuzindukana kutokana na kuzimia, akasema: “Ewe Ali waislamu wamefanya nini?” Akasema: “Wametangua ahadi na wamekimbia.” Akasema: “Nitosheleze hao.” Akawatimua mbali na yeye, na alikuwa aendelea kupambana na kikosi baada ya kikosi huku akinadi waislamu mpaka walijikusanya.

Jibril akasema: “Malaika wamestaajabishwa na uzuri wa *muwasatu* 125 wa Ali nafsi yake kwako.” Hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: “Nini kimzuie kufanya hivyo hali ikiwa yeye atokana na mimi na mimi natokana na yeye.”126

Na kwa ajili ya kubaki imara kwa Ali (a.s.), baadhi ya waislamu walirudi kwenye medani ya vita, na Uthman alirudi baada ya siku tatu. Nabii (s.a.w.w) alimwambia: “Umekwenda......”127

Katika vita vya Handaki walipoizingira washirikina Madina kama Mwenyezi Mungu (s.w.t.) alivyosema:

إِذْ جَاءُوكُمْ مِنْ فَوْقِكُمْ وَمِنْ أَسْفَلَ مِنْكُمْ وَإِذْ زَاغَتِ الْأَبْصَارُ وَبَلَغَتِ الْقُلُوبُ الْحَنَاجِرَ وَتَظُنُّونَ بِاللَّهِ الظُّنُونَا {10}

***“Walipowajia kutoka juu yenu na kutoka chini yenu, na macho yaliponywea na nyoyo zikapanda kooni, nanyi mkaanza kumdhania Mwenyezi Mungu dhana mbalimbali.”* (*Surat Ahzab: 10*),**

Umar bin Abduwudd alipoingia handaki ili kuwavamia waislamu, alinadi kutaka makabilano, waislamu walinywea, Ali (a.s.) alijitokeza akiwa amejifunga kilemba cha Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) mkononi mwake, akiwa na upanga, akampiga pigo moja lililokuwa linalingana na uzito wa amali za viumbe vya aina mbili (majini na watu) mpaka Siku ya Kiyama.128 Abu Bakr, Umar na Uthman walikuwa wapi?

Mwenye kuangalia kitabu *Ghazawatil-Waqidiy* na *Tarikhul-Baladhuriy* atajua nafasi yake kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu katika jihadi na mtihani wake siku ya Handaki, na siku ya Banil-Mustalaq, na siku ya kuung’oa mlango wa Khaybar, na katika ghazwa ya Khaybar. Na mlango huu hautoshi kurefusha maneno kwa kuwa ni mashuhuri.

Na Abu Bakr al-Anbariy ameeleza katika kitabu chake *al-Amal* kuwa Ali (a.s.) alikuwa ameketi kwa Umar msikitini hali akiwa na watu, Ali alipoinuka na kuanza kuondoka, mtu mmoja alimtaja na kumnasibishia upotovu na kujiona.

Umar akasema: “Mtu mfano wake apotoke! lau si upanga wake nguzo ya dini isingesimama, na yeye ni Kadhi mwadilifu mno wa umma na wa mwanzo katika umma kusilimu, na mwenye hadhi katika umma.” Yule msemaji alimwambia Umar: “Basi ni kitu gani kimekuzuieni mbali na yeye ewe Amiirul-Muuminina?” Akasema: “Hatukumchukia ila kwa sababu ya udogo wa umri wake, na upendo wake kwa Bani Abdil-Mutalib, na kuifikisha kwake Sura ya Baraa Makka.”

Na Ali (a.s.) alipomuita Muawiyah wapambane ili watu wapumzike mbali na vita endapo mmoja wao atauwawa, Amru alimwambia Muawiya: "Kwa kweli huyu mtu amekufanyia insafu." Muawiyah akamwambia Amru: "Haujanighushi kila uliponipa nasaha ila ni leo.
Unaniamuru nipambane na Abul Hasan hali ukiwa wajua kuwa yeye ni shujaa mwenye kuzingira? Nakuona una tamaa ya uamiri wa Sham baada yangu."[129]

Waarabu walikuwa wanajionea fahari kuwa kwao vitani na kukabiliana na yeye. Ama waliouawa na yeye jamaa zao walijionea fahari kuwa yeye (a.s.) ndiye aliyewauwa.

Na kauli zao katika hilo ni dhahiri na ni nyingi kiasi hazihesabiki. Ummu Kulthum[130] akasema kumhusu Umar bin Abdil- Wud:

**"Lau angekuwa muuwaji wa Amr sio yeye. Ningelia abadan muda wote wa kuishi kwangu. Lakini muuaji wake ni asiye na kifani, alikuwa baba yake aitwa Baydwatul Baladi."**[131]

Na suala kwa jumla ni kwamba kila shujaa duniani ananasibika na yeye, na kwa jina lake Mashariki ya nchi na Magharibi yake.

Ama kuhusu ukarimu wake na upaji wake, ni yule aliyekuwa anabakia na njaa katika swaumu yake kiasi kwamba alifikia kufunga akiwa na njaa siku tatu - yaani hakula usiku wa kuamkia funga - anampa kipaumbele mwombaji kila usiku kwa chakula chake, mpaka Mwenyezi Mungu (s.w.t.) akateremsha Sura kuhusiana na jambo hili:

هَلْ أَتَىٰ عَلَى الْإِنْسَانِ حِينٌ مِنَ الدَّهْرِ لَمْ يَكُنْ شَيْئًا مَذْكُورًا {1}

***"Hakika ulimfika mtu wakati fulani wa zama ambapo hakuwa kitu kinachotajwa."***
**(*Sura Dahri: 1*)**

Alitoa sadaka pete yake akiwa katika hali ya rukuu Aya ilishuka:

إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ رَاكِعُونَ {55}

***"Hakika kiongozi wenu hasa ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walioamini ambao husimamisha swala na hutoa zaka na hali ya kuwa wamerukuu."*** **(*Sura Maidah: 55*)**

Alitoa sadaka dirhamu nne Mwenyezi Mungu (s.w.t.) akateremsha kuhusiana na tukio hilo Aya: **"Wale watoao mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhahiri"** (***Surat al-Baqarah*: 274**) Na alitoa dirham

kumi siku ya kusema siri na Mtume (s.a.w.w.). Mwenyezi Mungu aliufanyia wepesi umma kwa ajili ya sadaka hiyo.

Naye ni yule ambaye alikuwa anamwagia maji mitende kwa mkono wake na kwa ujira wa kazi hiyo alikuwa anatoa sadaka. Na kuhusiana na hilo adui yake Muawiya bin Abu Sufyan alimwambia Mahjinu Dhwabiy alipomwambia: "Nimekujia kutoka kwa mtu bakhili mno."

Akasema: "Ole wako, umesemaje? Wasema yeye ni mtu bakhili mno katika watu! Lau angekuwa anamiliki nyumba ya dhahabu na nyumba ya majani angetoa dhahabu yake kabla ya majani yake."132

Na yeye ndiye yule asemaye: "Ewe njano (dhahabu) ewe nyeupe (fedha) mghuri mwingine, ni kwa ajili yangu umejitokeza au ni kwa ajili yangu umekuwa na shauku, haiwi, haiwi, nimekwisha kutaliki talaka tatu isiyo na rejea."133

Naye ni yule ambaye alipambana na nafsi yake usiku wa kulala juu ya kitanda cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w), na alijitoa mhanga kwa ajili ya Nabii (s.a.w.w) mpaka iliteremka kumhusu:

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَشْرِي نَفْسَهُ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ رَءُوفٌ بِالْعِبَادِ {207}

***"Na miongoni mwa watu kuna ambaye huiuza nafsi yake kwa ajili ya kutaka radhi za Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni Mwenye huruma juu ya waja.***)
(***Surat Al-Baqarah: 207***)

Yohana akasema: Waliposikia maneno haya hakuna yoyote aliyeyakana kati yao, na wakasema: Sahihi umesema kwa kweli haya uliyoyasema tumeyasoma kutoka katika vitabu vyetu na tumeyanakili kutoka kwa maimamu wetu, lakini mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kuwatilia maanani ni jambo liko nyuma ya haya yote, na huenda Mwenyezi Mungu akawa anamtilia maanani Abu Bakr zaidi kuliko Ali, kwa hiyo anamboresha zaidi yake.

Yohana akasema: Kwa kweli sisi hatujui ghaibu, na wala hajui ghaibu ila ni Allah (s.w.t.). Na hili mlilosema ni singizio, na Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema "**Wazushi wameangamizwa.**" (***Surat al-Dhaariyatu*: 10**) Na sisi twahukumu kwa ushahidi tu alionao Ali (a.s.) kuhusu ubora wake na tumeutaja.

Ama utiliaji maanani wa Mwenyezi Mungu kumhusu Ali, upatikanao kutoka kwenye maneno haya ni dalili ya katashauri kwa maneno hayo, hivi ni utiliaji manani gani ulio bora kuliko Mwenyezi Mungu kumjaalia Ali baada ya Nabii wake kuwa ni mtu bora zaidi katika watu wa nasaba, na mvumilivu mno kati yao, shujaa mno wa roho, mwenye vita vingi, mwenye zuhdi sana, mfanya ibada kwa wingi, ukarimu, uchamungu, na mengine miongoni mwa makamilifu ya tangu, huu ndio utiliaji maanani.

Ama kuhusu upendo wake wa kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Mtume wa Mwenyezi

Mungu (s.a.w.w) ametoa ushahidi katika maeneo, miongoni mwayo ni kwenye ule msimamo usioweza kukanushika, ule wa siku ya Khaybar, pindi Nabii (s.a.w.w) aliposema:

"Kesho nitampa bendera mtu anayempenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na anapendwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake."[134]

Na mwanachuoni wenu Akhtab Khawarzami ameeleza katika kitabu *al- Manaqib* kuwa Nabii (s.a.w.w) alisema: "Ewe Ali lau mtu amwabudu Mwenyezi Mungu kwa muda mfano wa aliobaki Nuhu katika kaumu yake, na awe na dhahabu kama mlima wa Uhud na aitumie katika njia ya Mwenyezi Mungu, na arefushwe umri wake ili ahiji hija elfu moja ya kutembea kwa miguu yake, halafu auwawe kati ya Swafa na Marwa kwa dhuluma, halafu awe hajakufanya wewe kuwa walii wake, ewe Ali hatoipata harufu ya Janna na wala hatoiingia."[135]

Na katika kitabu kilichotajwa kuna habari kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) amesema: "Lau watu wangeafikiana kumpenda Ali bin Abu Talibu (a.s.), basi Mwenyezi Mungu asingeumba moto."[136] Na katika kitabu *al-Firdawsu* kuna habari kuwa: "Kumpenda Ali ni wema ambao haudhuriki na ovu lolote, na kumchukia ni uovu ambao hauathiriwi na jema lolote."[137]

Na katika kitabu cha Ibnu Khalawiyah imepokewa kutoka kwa Hudhaifa bin Alyamani, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) amesema: 'Mwenye kutaka atoe kito cha pete yake cha yakuti ambacho Mwenyezi Mungu alikiumba kwa mkono wake halafu alikiambia: Kuwa na kikawa, basi na amfanye Ali bin Abu Talib walii wake baada yangu."

Na katika *Musnad* ya Ahmad bin Hanbal katika jalada la kwanza: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alishika mkono wa Hasan na Husein na akasema: "Mwenye kunipenda mimi na akawapenda hawa wawili na akampenda baba wa wawili hawa, atakuwa pamwe na mimi katika daraja yangu Siku ya Kiyama."[138]

Yohana akasema: Ee ninyi maimamu wa kiislamu je baada ya maneno haya yaliyo katika kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume wake, kuhusu kumpenda yeye na kumboresha juu ya yule ambaye hana fadhila hizi, kuna maneno?

Maimamu wakasema: Ewe Yohana! Marafidhu wanadhani kuwa Nabii (s.a.w.w) aliusia ukhalifa kwa Ali (a.s.), na kuwa ameagiza hilo wazi wazi ukhalifa uwe kwa Ali. Na kwetu sisi ni kuwa Nabii (s.a.w.w) hakumusia ukhalifa mtu yoyote.

Yohana akasema: Hiki hapa Kitabu chenu ndani yake mna:

كُتِبَ عَلَيْكُمْ إِذَا حَضَرَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ إِنْ تَرَكَ خَيْرًا الْوَصِيَّةُ لِلْوَالِدَيْنِ وَالْأَقْرَبِينَ بِالْمَعْرُوفِ ۖ حَقًّا عَلَى الْمُتَّقِينَ {180}

***“Mmelazimishwa, mmoja wenu anapofikiwa na mauti kama akiacha mali, kuwausia wazazi wawili na jamaa kwa uadilifu, ni wajibu kwa wamchao Mungu.”* (*Surat Al-Baqarah: 180*).**

Na katika Bukhari yenu anasema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) amesema: “Si haki kwa mtu mwislamu alale ila usia wake uwe chini ya kichwa chake.”139 Je mnasadiki kuwa Nabii wenu anaamuru asiyoyatenda, hali ikiwa katika Kitabu chenu kuna lawama kwa ambaye anaamuru asiyoyatenda, miongoni mwa kauli zake Mtukufu:

أَتَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبِرِّ وَتَنْسَوْنَ أَنْفُسَكُمْ وَأَنْتُمْ تَتْلُونَ الْكِتَابَ ۚ أَفَلَا تَعْقِلُونَ {44}

***“Je mnawaamuru watu kutenda mema na mnajisahau wenyewe na hali mnasoma Kitabu? Basi hamfahamu.”* (*Sura Al-Baqrah: 44*).**

Wallahi ikiwa Nabii wenu amekufa bila ya usia itakuwa amekhalifu amri ya Mola wake, na amelitangua neno lake mwenyewe, na wala hakuwafuata manabii waliopita kwa kuusia kwao atakayesimamia mambo baada yao. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

فَبِهُدَاهُمُ اقْتَدِهْ ۗ{90}

***“Basi fuata mwongozo wao.”* (*Surat An’aam: 90*).**

Lakini yeye yuaepukana na hayo, ninyi mwasema haya kwa kuwa hamna elimu na kwa sababu ya ukaidi. Kwa kuwa imamu wenu Ahmad bin Hanbal ameeleza ndani ya *Musnad* yake kuwa: “Salman akasema: ‘Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) hivi ni nani wasii wako?’
Akasema (s.a.w.w.): ‘Ewe Salman nani alikuwa wasii wa ndugu wa Musa (a.s.)?’ Akasema: ‘Yushau bin Noun!’ Akasema (s.a.w.w.): ‘Kwa kweli wasii wangu na mrithi wangu ni Ali bin Abi Talib.’”

Na katika kitabu cha Ibnu al-Maghaziliy as-Shaafiiy kuna habari kwa isnadi yake kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), akasema: “Kila nabii ana wasii na mrithi. Na mimi wasii wangu na mrithi wangu ni Ali bin Abu Talib.”140

Na huyu imamu al-Baghawiy mwenye kuhuisha Sunna ya dini, naye ni miongoni mwa wanahadithi wenu wakubwa na wafasiri wenu. Ameeleza katika tafsiri yake iitwayo Maalimut-*Tanzili kwenye* kauli yake (s.w.t.):

**“Na waonye jamaa zako wa karibu.” (*Sura Shuarau*: 214).** Amenukuu kutoka kwa Ali (a.s.) kuwa amesema: “Iliposhuka Aya hii Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) aliniamuru nimkusanyie Bani Abdil-Muttalibi, nikawakusanya nao wakati huo wakiwa watu arobaini wanazidi mtu mmoja au

wanapungua. Aliwakaribisha mguu wa kondoo na bakuli la maziwa, walishiba na walikunywa na kukoza kiu japokuwa mmoja wao angeweza kula wote na kunywa maziwa yote, kisha akawaambia:

“Ee ninyi wana wa Abdul-Muttalib, kwa kweli mimi nimekujieni na jambo lenye kheri ya dunia na akhera. Na Mola wangu ameniamuru nikuiteni muingie kwenye jambo hili, hivyo basi ni nani miongoni mwenu atan- iongezea nguvu kwenye jambo hili, naye atakuwa ndugu yangu na wasii wangu na khalifa wangu baada yangu?’ Hakuitika mmoja yoyote.

“Ali akasema: Nilisimama kwa ajili yake, na nilisema: Mimi naitika ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w). Akaniambia: Wewe ni ndugu yangu na wasii wangu baada yangu hivyo basi msikilizeni na mumtii. Walisimama huku wakicheka na wanamwambia Abu Talib: Ama kwa haki- ka amekuamuru umsikilize mwanao na umtii.”141

Riwaya hii pia ameielezea imamu wenu Ahmad bin Hanbal katika *Musnad* yake.142 Na Muhammad bin Is’haaqa Tabariy katika *Tariikh* yake.143 Na Kharkashiy pia ameieleza.

Ikiwa ni ya uongo itakuwa mmetoa ushahidi dhidi ya maimamu wenu kuwa wao wanaelezea uwongo kumhusu Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: **“Sikilizeni! Laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya madhalimu.”** (***Sura Huud*: 18**).
Na anase- ma: **“Waambie: Wale wanaomzulia Mwenyezi Mungu uongo hawatafaulu.”**
(***Sura Yunus*: 69**). Na amesema:

ثُمَّ نَبْتَهِلْ فَنَجْعَلْ لَعْنَتَ اللَّهِ عَلَى الْكَاذِبِينَ {61}

***“Na tuiweke laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie wenye kusema uwongo.”***
**(*Surat Aali Imran: 61*).**

Na ikiwa hawakudanganya na suala likiwa kama lilivyo, nini dhambi ya Rafidhu? Mwogopeni Mwenyezi Mungu enyi maimamu wa waislamu. Billahi mwasema nini kuhusu habari ya Ghadiri ambayo Shia wanadai?

Maimamu wakasema: Wanazuoni wetu wameafikiana kuwa ni uongo uliozuliwa.

Yohana akasema: Allahu Akbar! Huyu hapa imamu wenu na mwanahadithi wenu Ahmad bin Hanbal ameeleza katika M*usnad* yake kuwa al-Barau bin Aazib amesema: “Tulikuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) tukafika Ghadir Khum, palinadiwa katika sisi: Swalatu jamia.

Na alifagiliwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) chini kati ya miti miwili, aliswali dhuhuri, na aliushika mkono wa Ali (a.s.) na akasema: “‘Si mwajua kuwa mimi ni bora kuliko kila muumini?’ Wakasema: Ndio. Akaushika mkono wa Ali (a.s.) na aliunyanyua hadi weupe wa kwapa zao ulionekana

bayana, na aliwaambia:

‘Ambaye mimi ni walii wake, na huyu Ali ni walii wake. Ewe Allah mpende ampendaye na mfanye adui amfanyaye adui, na umnusuru atakayemnusuru na umtelekeze atakayemtelekeza.’ Umar bin al-Khattab alimwambia Ali: “Hongera ewe mwana wa Abu Talib! Asubuhi hii umekuwa walii wangu na walii wa kila muumini wa kiume na muumini mwanamke.”

Na ameieleza katika *Musnad* yake kwa njia nyingine na ameifanyia sanad kwa Abu Tufa’il. Na ameielezea kwa njia nyingine na akaifanyia sanad kwa Zaid bin Arqam.144 Na aliieleza Ibnu Abdu Rabi katika kitabu *Al- Aqdu Al-Farid*.145 Na Said bin Wahab ameieleza na pia Thualibiy katika tafsiri yake.146

Na alitilia mkazo khabari hizi zile tafsiri zilizoeleza suala la kushuka kwa *Sura Maarij*. Nalo ni kuwa Harith bin Nu’man al-Fahriy alimjia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) akiwa katika kundi la swahaba zake na akasema: “Ewe Muhammad umetuamuru tushuhudie hapana Mola wa haki ila Allah, na kuwa wewe Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, tukakubali. Na ulituamuru tuswali Swala tano, tukakukubalia.

Na ulituamuru tufunge mwezi wa Ramadhan, tukakubali. Na ulituamuru tuhiji nyumba, tukakubali. Halafu hukuridhika mpaka umenyanyua mabega ya mtoto wa ami yako na umemfadhilisha zaidi yetu na umesema: “Ambaye mimi ni walii wake basi huyu Ali ni walii wake.” Je kitu hiki ni kutoka kwako au ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu?

Mtume alisema: “Namuapa Mwenyezi Mungu ambaye hapana Mungu ila ni Yeye, kwa kweli ni amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.” Hapo Harith bin Nu’man aligeuka huku akisema: “Ewe Mola! Ikiwa asemayo Muhammad (s.a.w.w) ni ya kweli tunyeshee mvua ya mawe kutoka mbin- guni.” Hakufika kwenye kipandwa chake Mwenyezi Mungu alimtupia jiwe likaangukia juu ya kichwa chake na likatoka chini yake eneo la haja kubwa, akaanguka mwereka, ikateremka: “**Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea**.” (**Surat Ma’arij: 1**) Inakuwaje jaizu kwenu maimamu wenu watowe maelezo ya riwaya na nyinyi mseme uongo sio sahihi?!

Maimamu wakasema: Ewe Yohana maimamu wetu wameeleza hayo lakini ukirejea kwenye akili zako na fikra zako utajua kuwa ni miongoni mwa mambo yaliyo muhali, eti Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) amuusiye Ali bin Abu Talib, ambaye yeye ni kama mlivyomsifu, halafu waafikiane maswahaba wote kuuficha usia huu na wasiutelekeze, na waafikiane kuuficha, na wageukie kwa Abu Bakr Mtaymiy, aliye dhaifu mchache wa ndugu wa karibu, hali ikiwa maswahaba walikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu anapowaamuru wajiuwe binafsi hufanya hivyo. Vipi mwenye akili aisadiki hali hii ya muhali?

Yohana akasema: Msione ajabu hilo, umma wa Musa (a.s.) ulikuwa zaidi ya mara sita ya umma wa Muhammad (s.a.w.w), alimwacha nduguye Harun kwao naye pia alikuwa Nabii wao pia, na walikuwa wanampenda sana kuliko Musa, na walimtelekeza na kumuelekea Saamiriy, na walibaki wakiuabudia mwili wa ndama wenye sauti.

Hivyo basi haiwi mbali umma wa Muhammad kumtelekeza wasii wake baada ya umauti wake na kumwelekea Sheikh ambaye Mtume (s.a.w.w) alimuoa binti yake. Na huenda lau Qur'ani haingekileta kisa cha ibada ya ndama msingekiamini. Maimamu wakasema: Ewe Yohana basi ni kwa nini hakuwagomba bali alinyamaza na kuwafanyia baia?
Yohana akasema: Hapana shaka kuwa alipokufa Mtume wa Mungu (s.a.w.w), waislamu walikuwa wachache, na huko Yamama kuna Musaylama Al-Kadhabu akiwa amefuatwa na watu thamanini elfu, na waislamu walio Madina wamezungukwa na wanafiki. Lau angeonyesha ugomvi kwa upanga angekuwa kila ambaye Ali bin Abu Talib amemuua mwanawe au nduguye angekuwa dhidi yake, na ilikuwa siku hizo ni wachache miongoni mwa watu kuwepo mtu ambaye Ali hakuua mtu kutoka kabila lake na swahibu zake, na anaonasibiana nao, lazima kutakuwa na mmoja aliyeuawa au zaidi.

Na walikuwa wawe dhidi yake, kwa ajili hiyo alivuta subira na alishindana nao kwa njia ya hoja miezi sita bila tofauti kati ya Ahlu sunna.

Kisha lilipomfikia ombi la baia kutoka kwao, upande wa Sunni wanasema kuwa alifanya baia na kwa Rafidhu wanasema hakufanya baia. Na *Tariikhut-Tabariy* yajulisha kuwa yeye hakufaya baia, ila tu Ibnu Abbas alipoona fitna alipiga kelele: "Fanya baia ewe mwana wa ndugu yangu!"

Na ninyi mnajua kuwa ukhalifa lau usingekuwa wa Ali asingeudai, lau angeudai bila ya haki angekuwa mtu wa batili, na ninyi mnaleta riwaya kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) kuwa amesema: "Ali yu pamoja na haki na haki ipo pamoja na Ali." Sasa itakuwa vipi adai lisilo la haki, kwa hivyo amkadhibishe Nabii wenu siku zile?!

Ama kustaajabishwa kwenu na Bani Israili kumkhalifu nabii wao kuhusu khalifa wake na kurejea kwao kwenye ibada ya ndama na kumfuata Samiriy, ndani yake kuna siri ya ajabu. Ninyi mmeleta riwaya kuwa nabii wenu alisema: "Mtaiga mwendo wa Bani Israeli kiatu kwa kiatu ....... hadi lau wangeingia shimo la kenge mngeingia."147 Na imethibiti katika kitabu chenu kuwa wana wa Israili walimkhalifu Nabii wao kuhusu khalifa wake, na walimgeuka na kuelekea kusikofaa.

Wanachuoni wakasema: Yohana wewe unatambua kuwa Abu Bakr hafai kuwa khalifa?

Yohana akasema: Ama mimi wallahi sioni kuwa Abu Bakr anafaa kwa ukhalifa, wala mimi siwapendelei Rafidhu. Lakini mimi nimeangalia vitabu vya kiislamu nikaona kuwa maimamu wenu wametufundisha sisi kuwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake wametoa habari kuwa Abu Bakr hafai kwa ukhalifa.

Maimamu wakasema: Iko wapi hiyo?

Yohana akasema: Nimeona katika *Bukhari* yenu148 na katika *al-Jam'u Baynas-Swihahi Sita*, katika *Sahih Abi Daudi*, *Sahih Tirmidhiy*149 na *Musnad Ahmad bin Hanbal*, kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alituma Sura Baraa ipelekwe kwa watu wa Makka na Abu Bakr, alipofika Dhul'hulaifah alimwita Ali (a.s.) na akamwambia: "Hebu muwahi Abu Bakr na chukua kile kitabu kutoka kwake na wasomee." Alimkuta sehemu iitwayo al-Johfa akachukua kitabu kutoka kwake na Abu Bakr alirejea kwa

Nabii (s.a.w.w) na akasema: “Je kimeteremshwa kitu kunihusu?” Alisema (s.a.w.w.): “Hapana ila Jibril (a.s.) alinijia na akasema: ‘Hatekelezi mtu badala yako ila wewe au mtu atokanaye na wewe.’”

Ikiwa hali ni kama hii, Abu Bakr hafai kuzifikisha Aya chache badala ya Nabii (s.a.w.w.) katika uhai wake, basi vipi atafaa awe khalifa baada ya kufa kwake na atekeleze badala yake! Kutokana na hilo tumejua kuwa Ali (a.s.) anafaa kutekeleza badala ya Nabii (s.a.w.w). Oh! Enyi Waislam vipi mnaufumbia macho ukweli ulio bayana? Na kwa nini mnawatumainia hao jamaa na kwa kiwango gani mnahofia mambo ya kutisha?

Mhanafi aliinamisha kichwa chini halafu alikiinua na akasema: Ewe Yohana wallahi wewe waangalia kwa jicho la insafu, na kwa kweli haki ni yenu, na ninakuzidishia maana ya Hadithi hii, ni kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu alitaka kuwabainishia watu kuwa Abu Bakr hafai kuwa khalifa, kwa minajili hiyo alimwamuru Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amtoe Ali nyuma yake na amuengue mbali na daraja hii tukufu, ili awajulishe watu kuwa Abu Bakr hafai kwa ukhalifa. Na kuwa anayefaa kwa ukhalifa ni Ali (a.s.), hivyo alimwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.): “Hafikishi mtu badala yako ila wewe mwenyewe au mtu kutokana na wewe.”150 Wewe wasemaje ewe mmaliki?

Maliky akasema: Wallahi yangali mawazo yananijia akilini kuwa Ali alimgomba Abu Bakr katika ukhalifa wake muda wa miezi sita, na wawili wagombanao kuhusu jambo hapana budi mmoja wao atakuwa ndio mwenye haki, hivyo basi tukisema kuwa Abu Bakr alikuwa na haki tutakuwa tumekhalifu lijulishwalo na kauli ya Nabii (s.a.w.w): ‘’Ali yuko pamwe na haki na haki ipamwe na Ali.’’ Na hii ni Hadithi sahihi hakuna tofauti kuihusu. Na hapo alimwangalia mhanbali ili aone rai yake.

Mhanbali akasema: Jamani kwa kiwango gani tutaufumbia macho ukweli! Wallahi kwa yakini Abu Bakr na Umar wamepora haki ya Ali (a.s.).

Yohana akasema: Jamaa walibabaika, na mzozo kati yao ukazidi, lakini tija ya usemi wao ni kuwa ukweli uko upande wa Rafidhu, basi aliyekuwa karibu mno na ukweli kati yao ni Imam wa mashafi. Aliwaambia: Nawaona mnashuku kuwa Nabii (s.a.w.w) amesema: ‘’Mwenye kufa hali akiwa hamjui imamu wa zama zake, na afe akipenda akiwa Yahudi na akipenda akiwa Mnaswara.’’

Nini makusudio ya imamu wa zama? Na ni nani?
Wakasema: Imam wa zama zetu ni Qur’ani kwa kuwa sisi kwayo twaongoka.

Mshafii akasema: Mmekosea kwa kuwa Nabii (s.a.w.w) amesema: “Maimamu watakuwa kutoka kwa makuraishi.” Wala Qur’ani haisemi mkuraishi.

Wakasema: Nabii ni imamu wetu.

Mshafii akasema: Mmekosea, kwa kuwa wanavyuoni wetu walipohojiwa kuwa vipi inafaa kwa Abu Bakr na Umar wamwache Mtume wa Mwenyezi Mungu akiwa kitandani bila kufanyiwa josho la maiti na waende kugombania ukhalifa. Na hii ni dalili ya pupa ya ukhalifa waliyokuwa nayo, na hiyo ni dosari ya

kusihi ukhalifa wa wawili hawa. Wanazuoni wetu walijibu: Kwa kweli wao waliona kauli za Nabii (s.a.w.w.) “Atakayekufa akiwa hamjui imamu wa zama zake atakuwa amekufa kifo cha kijahiliya.” Hawakuona jaizi wafe kabla ya kuainishwa imamu, ndio maana waliharakia kumwainisha kulikimbia kemeo hili. Hapo tumejua kuwa mradi wa imamu sio Nabii.

Walimwambia Mshafii: Nani imamu wako ewe mfuasi wa Shafii? Alisema: Nikiwa katika kabila yenu sina imamu, na nikiwa katika kabila ya Ithna’ashara Imam wangu ni Muhammad bin Hasan (a.s.).

Wanazuoni wakasema: Hili wallahi ni jambo liko mbali kabisa, vipi itajuzu awe imamu wako ni mmoja kwa muda ambao hawezi kuishi yeyote mfano wa muda huo, wala yoyote hawezi kumwona? Hilo ni mbali kabisa.

Mshafii akasema: Dajjal ni miongoni mwa makafiri, na mnasema kuwa: Yeye ni hai na yupo. Na yeye ni wa kabla ya Mahdi, na Samiriy kadhalika. Na hamkanushi kuwepo kwa Ibilisi, na huyu Khidhru na huyu Isa, mnasema kuwa hawa wawili wapo hai. Na limekuja kwenu ambalo lijulishalo kupewa umri mrefu watu wa kheri na mabazazi. Na hii Qur’ani inasema kuwa vijana wa pangoni walilala miaka mia tatu na miaka tisa, hawali hawanywi. Hivi inakuwa vigumu mmoja katika dhuria wa Muhammad (s.a.w.w) aishi muda mrefu, anakula na anakunywa, ila tu yoyote hatuambii kuwa yeye alimuona?! Hivyo basi kuona kwenu ugumu kuko mbali mno na ukweli.
Yohana akasema: Nabii wenu amesema: “Umma wangu utafarakana baada yangu na kufikia vikundi sabini na tatu, kikundi kimoja ndio kiokovu, na sabini na mbili motoni.” Je wajua ni kipi hicho?

Wakasema: Ni Ahlus Sunna Wal’jamaa kwa mujibu wa kauli ya Nabii (s.a.w.w), alipoulizwa kikundi kiokovu kuwa ni kipi hicho? Alisema: “Ni wale walivyo nilivyo mimi na sahaba zangu.”[151]

Yohana akasema: Mwathibitisha vipi kuwa ninyi hii leo mko kama alivyokuwa Nabii (s.a.w.w)? Wakasema: Hivyo wananakili waliopita kutoka kwa waliotangulia. Yohana akasema: Nani ambaye anayeamini nukuu yenu? Wakasema: Inakuwaje hivyo?

Akasema: Kwa sababu mbili: Ya kwanza: Kwa kweli wanachuoni wenu wamenakili Hadithi nyingi ambazo zinajulisha uimamu ni wa Ali (a.s.) na ubora ni wake. Na ninyi mnasema kuwa nukuu hizo ni za uongo.

Na kwa kudai hivyo mnakuwa mmetoa ushahidi dhidi ya wanachuoni wenu kuwa wao wananakili uongo, huenda na hii ikawa nukuu ya uongo pia, kwa hiyo hamna rejea.

Pili: Nabii (s.a.w.w.) alikuwa anaswali kila siku swala tano msikitini, lakini haikudhibitiwa kuwa je yeye alikuwa anasoma Bismillahi asomapo al- Hamdu au hapana? Na je alikuwa anaamini kuwa ni wajibu au hapana? Na je alikuwa ananyosha mikono yake au hapana? Na ikiwa alikuwa anaikunja alikuwa anaikunja chini ya kitovu au juu yake? Na je alikuwa anapaka wudhu nywele tatu au robo ya kichwa? Au baadhi yake au chote. Na ikiwa hao salafu wenu hawakudhibiti kitu ambacho Mtume (s.a.w.w) alikuwa anafanya usiku na mchana mara nyingi, vipi wanadhibiti kitu ambacho hajapata kukifanya katika umri

wake ila mara moja au mara mbili? Liko mbali hili!

Vipi mnasema Ahlusunna wako kama vile alivyokuwa Nabii (s.a.w.w) hali ikiwa Ahlu Sunna sio kundi moja, na wanapingana wao kwa wao katika itikadi zao, na mawili yanayopingana kuwa pamoja ni muhali. Mfano, maji ndani ya kikombe kimoja yawepo ya baridi sana na ya moto sana wakati huo huo, hilo ni muhali!

Yohana akasema: Waliinama wote, na kukajiri maneno kati yao, sauti zilipanda kati yao na wakasema: Ambalo ni sahihi ni kuwa sisi hatujui kikundi kiokovu ni akina nani. Kila mmoja wetu anadhani kuwa yeye ndiye mwokovu. Na kuwa wasiokuwa wao ndio wa kuhiliki. Na yawezekana ikawa yeye ambaye anadhania kuokoka ndiye mwenye kuhiliki, na wengine ni wenye kuokoka.

Yohana akasema: Hiki kikundi cha Rafidhu ambao mnawadhania kuwa wapotovu wanakata shauri kuwa ndio watakaookoka, na wataangamia wasiokuwa wao, na hilo wanalitolea dalili kuwa itikadi yao iko na ukweli mno na iko mbali mno na shaka.

Wanachuoni wakasema: Ewe Yohana, sema, sisi wallahi hatukutuhumu kwa kuwa tunajua wewe unajadiliana na sisi ili kuidhihirisha haki.

Yohana akasema: Mimi nasema itikadi ya Shia ni kuwa Mwenyezi Mungu ni wa milele na milele, wala hakuna wa milele ila ni Yeye. Na kuwa Yeye yupo, na kuwa Yeye sio mwili, wala hayuko mahali, na Yeye anaepukana na itikadi ya *hululu*. Na itikadi yenu mnathibitisha kuwa pamoja na Yeye kuna vya milele vinane, navyo ni sifa imefikia kiasi Imam wenu al-Fakhru Raziy amekuaibisheni, na amesema: “Kwa kweli Manaswara na Mayahudi wamekufuru walipofanya miungu miwili pamoja na Mungu kuwa ni wa milele, na swahiba zetu wamethibitisha wa milele tisa.” Na Ibnu Hanbal ni mmojawapo miongoni mwa maimamu wenu amesema: Mwenyezi Mungu ni mwili, na kuwa Yeye yupo juu ya Arshi. Na kuwa Yeye huteremka akiwa katika sura ya mvulana asiye na ndevu. Ewe Mwenyezi Mungu, je hali si kama nilivyosema?
Wakasema: Ndio.

Yohana akasema: Hivyo basi itikadi yao ni bora kuliko itikadi yenu. Itikadi ya Shia ni kuwa Allah Subhanahu wa Taala hafanyi baya, wala haachi wajibu, wala hakuna dhuluma katika utendaji wake. Na wanaridhia maamuzi ya Mwenyezi Mungu kwa kuwa Yeye haamui ila la kheri, na wanaamini kuwa tendo lake huwa kwa lengo si kwa mchezo.

Na kuwa Yeye haifanyii nafsi takilifu ila kadiri ya uwezo wake, wala hampotoshi yeyote katika waja wake, wala hazuii kati yao na ibada Yake, na kuwa Yeye ameutaka utii na amekataza maasi. Na kuwa wao wana hiyari katika matendo yao binafsi.

Na itikadi yenu ninyi ni kuwa maovu yote ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na kuwa kila linalotokea katika uwaji wa kitu kama vile ukafiri, ufasiki, maasi, kuuwa, kwiba na zinaa, Mwenyezi Mungu ameviumba kwa watendaji wake na amevitaka kwao na amewaamulia na ameondoa hiyari zao. Kisha

atawaadhibu kwavyo.

Na ninyi hamridhiki na maamuzi ya Mwenyezi Mungu bali Mwenyezi Mungu Mtukufu haridhiki na maamuzi Yake binafsi. Na kuwa Yeye ndiye aliyewapoteza waja na amezuia kati yao na ibada na imani, hali Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

إِنْ تَكْفُرُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنْكُمْ ۖ وَلَا يَرْضَىٰ لِعِبَادِهِ الْكُفْرَ ۖ وَإِنْ تَشْكُرُوا يَرْضَهُ لَكُمْ ۗ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۗ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ مَرْجِعُكُمْ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ۚ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ {7}

***"Mkikufuru, basi Mwenyezi Mungu hana haja nanyi, wala haridhii kufru kwa waja wake. Na kama mkishukuru, hayo atawaridhieni, wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine, kisha marudio yenu ni kwa Mola wenu, basi atakuambieni yale mliyokuwa mkifanya. Bila shaka Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani."*** (***Sura Zumar: 7***)

Zingatieni, je itikadi zenu ni bora kuliko itikadi zao au itikadi zao ndio bora kuliko itikadi zenu! Na ninyi mwasoma Kitabu, je hamtii akilini?!

Shia wanasema: Manabii wa Mwenyezi Mungu wamehifadhika mbali na dhambi, ndogo na kubwa, kuhusiana na wahyi na mengine, kusudi na kukosea, tokea mwanzo wa umri wao mpaka mwisho wake. Na itikadi yenu ni kuwa inajuzu kwao wao kukosea na kusahau. Na mmemnasibisha (s.a.w.w.) kuwa alisahau Qur'ani, na hilo ni jambo ambalo liwajibishalo kufru.

Mmesema: Aliswali swala ya asubuhi na alisoma Sura Najmu: **"Je mmewaona Lata na Uzza? Na Manata, mwingine wa tatu?"** (***Sura Najmu*: 19-20**) Na hii ni kufru na ushirikina wa dhahiri. Hata kuna baadhi ya wanavyuoni wenu kuna aliyetunga kitabu ndani yake kuna idadi ya dhambi alizozinasibisha kwa manabii (a.s.). Shia wakakijibu kitabu hicho kwa kitabu wamekiita *Tanziihul-Anbiyai*. Mnasemaje, ni itikadi gani iliyo karibu mno na usahihi, na karibu mno na ufanisi?

Na itikadi ya Shia ni kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) hakufishwa mpaka alipousia mtu atakaeshika amri baada yake, na kuwa yeye hakuuacha umma wake umetelekezwa na wala hakukhalifu kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w.t). Na itikadi yenu ni kuwa yeye ameuacha umma wake umetelekezwa, na hakumuusia atakayeshika amri baada yake.

Na Kitabu chenu ambacho kimeteremshwa kwenu ndani yake kuna wajibu wa kuusia, na katika Hadithi ya Nabii wenu ni wajibu kuusia. Hivyo imelazimu kulingana na itikadi yenu Nabii (s.a.w.w) awe amewaamuru watu asiyoyafanya! Basi ni itikadi ipi kati ya hizi mbili iliyo bora kuokoka?

Itikadi ya Shia ni kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) hakutoka duniani mpaka alipobainisha

kuwa ukhalifa ni wa Ali bin Abu Talib (a.s.), wala hakuuacha umma wake umetelekezwa, akamwambia siku ya kikao cha ndugu wa karibu: "Wewe ni ndugu yangu, wasii wangu na khalifa wangu baada yangu. Msikilizeni na mtii amri yake." Na ninyi mmeinakili na ameinakili imamu wa wasoma Qur'ani, na Tabariy, Kharkushiy na Ibnu Is'haqa.

Na akasema katika jambo hili siku ya Ghadir Khum: "Ambaye mimi ni walii wake, hivyo basi huyu Ali ni walii wake." mpaka Umar alimwambia Ali: "Hongera hongera ewe Ali, umekuwa walii wangu na walii wa kila muumini." Imam wenu Ahmad bin Hanbal amenakili hilo katika *Musnadi* yake.152 Na alimwambia Salman katika hili: "Hakika wasii wangu na mrithi wangu ni Ali bin Abu Talibi." Ameipokea hiyo imamu wenu Ahmad bin Hanbal.153

Na amesema kumsuhu: "Manabii usiku wa miiraji waliniambia: Tulitumwa tukiri unabii wako, na uwalii wa Ali bin Abu Talib."

Na mmeeleza riwaya katika *at-Thaalabiy* na *al-Bayan,* amesema humo: "Hakika anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake." Mmeleta riwaya katika *Bukhari* na *Muslim*.154Amesema Mtume (s.a.w.w.) kumhusu: "Hatekelezi kwa niaba yangu ila mimi au mtu kutokana na mimi." Na alimkusudia kwa hilo Ali bin Abu Talib.

Na mmeeleza katika *al-Jam'u Baynas-Swahihayni*, humo amesema: "Wewe kwangu uko na daraja ya Harun kwa Musa, isipokuwa hapana unabii baada yangu." Na mmeeleza kumhusu katika *Bukhari*.155

Mwenyezi Mungu ameteremsha kumhusu: **"Hakika ulimfika mtu wakati fulani wa zama ambapo hakuwa kitu kinachotajwa." (*Sura Dahr*:1)** Na imeteremshwa kumhusu: **"Hakika kiongozi wenu hasa ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walioamini ambao husimamisha swala na hutoa zaka na hali ya kuwa wamerukuu." (*Sura Maidah*: 55)** Na kuwa yeye ni mwenye Aya ya sadaka.156

Na kipigo alichompiga Amru bin Wud al-Amiriy ni bora kuliko amali za umma mpaka siku ya Kiyama.157 Naye ni ndugu wa Mtume wa Mwenyezi

Mungu (s.a.w.w) na mume wa binti yake. Na ni mlango wa Jiji la elimu. Na Imamu wa wachamungu, na ni raisi wa dini. Na yeye ni kiongozi wa pekee.158 Mtatuaji wa matatizo na mfumbuzi wa yaliyo magumu. Yeye ni Imam kwa tamko la kiungu. Halafu baada yake ni Hasan na Husein ambao Nabii (s.a.w.w) akasema kuwahusu:

"Hawa ni maimamu, wawe wameketi au wamesimama, na baba yao ni mbora kuliko wao."159Na Nabii (s.a.w.w.) akasema: "Hasan na Husein ni mabwana wa vijana wa peponi."160

Halafu ni Ali Zaynul-Abidina. Halafu watoto wake maasumina ambao hitimisho lao ni al-Hujja al-Mahdi Imamu wa zama hizi (a.s.) ambaye atakayekufa na asimtambue atakuwa amekufa kifo cha kijahili.

Na ninyi mmeeleza riwaya katika vitabu vyenu sahihi kutoka kwa Jabir bin Samrah kuwa amesema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) akisema: 'Baada yangu ni makhalifa kumi na wawili.'

Na akasema neno ambalo sikulisia vizuri."161 Na katika Bukhari *yenu*162

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) amesema: "Jambo la watu litaendelea mpaka wawatawale wanaume kumi na wawili." Halafu akasema neno kwa sauti hafifu sikulisikia."

Na katika *Sahih Muslim*: "Dini itaendelea kusimama mpaka Kiama kisimame, na watawaliwe na makhalifa kumi na wawili, wote kutoka kwa kuraishi."163 Na katika kitabu *Al-Jam'u Baynas-Swahihayni* na katika *Swihahu Sita* ni kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: "Hakika jambo hili halitotoweka mpaka wapite makhalifa kumi na wawili, wote kutoka kurayshi."164

Mwanachuoni wenu na msimulizi wenu wa hadithi na aliye mwaminifu kwenu, mwandishi wa kitabu *Kifayatut-Talibi* ameeleza kutoka kwa Anas bin Malik, akasema: "Mimi nilikuwa na Abu Dharr na Salman na Zayd bin Thabit na Zayd bin Arqam kwa Nabii (s.a.w.w), punde Hasan na Husein (a.s.) waliingia, Mtume wa Mwenyezi Mungu aliwabusu, na Abu Dharr alisimama akawainamia - kuonesha heshima - na alibusu mikono yao, na akarejea na kukaa pamoja na sisi. Kwa siri tulimwambia: 'Ewe Abu Dharr umemwona mzee miongoni mwa swahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) anasimama kwa heshima ya watoto wawili wa kibani Hashim na anawainamia na kuwabusu na kuibusu mikono yao!'

"Alisema: 'Naam, lau mngesikia niliyosikia mngewafanyia zaidi ya niliyofanya.' Tulisema: Umesikia nini kuwahusu wawili hao kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) ewe Abu Dharr? Akasema: Nilisikia anamwambia Ali na wao - Hasan na Husein: 'Wallahi lau mja aswali, afunge mpaka awe kama ngozi iliyochakaa, hivyo Swala yake wala saumu yake hazitomnufaisha ila kwa kuwapendeni nyinyi na kujiepusha na adui yenu. Ewe Ali, mwenye kuwafanyeni wasila kwa Mwenyezi Mungu kwa haki yenu itakuwa haki kwa Mwenyezi Mungu asimrudishe tupu. Ewe Ali, mwenye kuwapenda ninyi na kushikamana na nyinyi atakuwa ameshikamana na kishiko thabiti.'

"Akasema: Halafu Abu Dharr alisimama na alitoka, tulikwenda mbele kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na tukasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Abu Dharr alitupa habari ya kadha na kadha. Akasema: 'Abu Dharr amesema kweli, Wallahi ardhi haijapata kuwa na mwenye usemi wa kweli mno kuliko Abu Dharr."165

"Halafu (s.a.w.w) akasema: 'Mwenyezi Mungu Mtukufu ameniumba mimi na Ahlul-Bayt wangu kutoka nuru moja kabla Mwenyezi Mungu hajaumuumba Adam kwa miaka elfu saba, halafu tulihamishwa kutoka mgongoni mwake katika migongo ya watoharifu na kwenda kwenye miji ya uzazi ya walio tohara.' Nilisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) mlikuwa wapi? Na katika hali gani mlikuwa? Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akasema: 'Tulikuwa vivuli chini ya Arshi tunamsabihi Mwenyezi Mungu na tunamtakasa.'

"Halafu akasema (s.a.w.w.): 'Aliponipandisha mbinguni na nikafika Sidratul'muntaha Jibril aliniaga. Nikasema: Ewe mpenzi wangu Jibril mahali kama hapa wajitenga mbali na mimi? Akasema: 'Ewe Muhammad mimi sivuki mahali hapa mbawa zangu zitaungua.' Halafu nuru ilinitupa kutoka nuru hadi nuru kiasi Mwenyezi Mungu Mtukufu alivyopenda.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alinipa ufunuo: 'Ewe Muhammad! Hakika mimi nimeangalia ardhini mara moja kutoka humo – ardhini – nikakuchagua wewe na nikakufanya Nabii. Halafu niliangalia mara ya pili kutoka humo nimemchagua Ali na nimemfanya wasii wako na mrithi wa elimu yako na imamu baada yako. Na nitatoa migongoni mwenu dhuria iliyo tohara na maimamu walio na umaasumu, wahifadhi wa elimu yangu, lau si wao nisingeumba dunia wala akhera, wala Janna wala moto. Je ungependa uwaone? '

"'Nilisema: Ndio ewe Mola wangu, niliitwa: 'Ewe Muhammad inua kichwa chako.' Nilikiinua kichwa changu ghafla niliona nuru za Ali, Hasan na Husein, Ali bin Husein, Muhammad bin Ali, Ja'far bin Muhammad, Musa bin Ja'far, Ali bin Musa, Muhammad bin Ali na Ali bin Muhammad, Hasan bin Ali, na al-Hujja bin al-Hasan, ambayo inang'ara kwao kama nyota, juu yao rehema na amani iwashukie.

Nilisema: Ewe Mola wangu ni nani hao na huyu ni nani? (swt) Akasema: 'Hao ni maimamu baada yako waliotoharishwa kutoka mgongoni kwako, na huyu ndio al-Hujja ambaye ataijaza ardhi usawa na uadilifu kama ambavyo imejazwa giza na uonevu na ataviponya vifua vya kaumu ya waumini.'

"Tulisema baba zetu na mama zetu wawe fidia kwa ajili yako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa kweli umesema la ajabu. Akasema (s.a.w.w):

'Na la ajabu zaidi kuliko hilo ni kuwa kaumu wanasikia hili kutoka kwangu halafu wanarejea nyuma kwa visigino vyao baada ya kuwa Mwenyezi Mungu amewaongoza, na wananiudhi kuhusu wao, Mwenyezi Mungu asiwafikishie uombezi wangu."166

Yohana akasema: Na itikadi yenu ninyi ni kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alipotawafu alitawafu bila usia na wala hakutoa agizo kuhusu khalifa wake, na kuwa Umar bin al-Khattab alimchagua Abu Bakr na alimfanyia baiya na umma ulimfuata, na kuwa yeye alijiita binafsi kuwa ni khalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).

Na nyinyi nyote mnajua kuwa Abu Bakr na Umar alipotawafu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) walimtelekeza bila ya kumuosha wala kumkafini na walikwenda kwenye Saqifa ya Bani Saaida wakazozana na Answari kuhusu ukhalifa. Abu Bakr alitawalia ukhalifa na hali Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) akiwa kitandani. Na hapana shaka kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) hakumfanya khalifa. Na kuwa yeye alikuwa anaabudia sanamu miaka arobaini kabla hajasilimu. Na Mwenyezi Mungu (s.w.t.) anasema: **"Ahadi yangu haiwafikii madhalimu."** **(*Surat Al-Baqarah*: 124)**

Na alimzuia Fatima urithi wa baba yake Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) kwa habari (alizozieleza). Fatima akasema: "Ewe Abu Bakr wewe wamrithi baba yako na mimi nisimrithi baba yangu. Kwa kweli umeleta kitu cha uzushi." Na alimpinga kwa kauli Yake Mwenyezi Mungu (s.w.t.): **"Atakayenirithi na awarithi ukoo wa Yaakub" (*Sura Maryam*: 6)**. Na kauli Yake: **"Na Sulaiman alimrithi Daud." (*Sura Namli*: 16)**. Na kauli Yake: **"Mwenyezi Mungu anawausia kwa watoto wenu" (*Sura Nisaa*: 11)**

Lau Hadithi ya Abubakr ingekuwa sahihi basi Ali bin Abu Talib (a.s.) hangeushikilia upanga wa Mtume

wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), nyumbu wake na kilemba chake. Abbas alimgomba Ali baada ya kifo cha Fatima (a.s.) kuhusu hilo. Lau Hadithi hii ingekuwa maarufu haingewafalia hilo.

Na Abubakr alimzuia Fatima (a.s.) Fadak kwa kuwa yeye aliidai. Na alikumbusha kuwa Nabii (s.a.w.w) alimpa – kama zawadi. Na Abubakr hakumsadiki japokuwa yeye Fatima ni miongoni mwa watu wa peponi, na kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amemwondolea kila chafu ikiwemo itikadi na matendo, yakiwemo uongo na mengine. Na alimfanya Ali (a.s.) kuwa shahidi wake na Ummu Ayman pamwe, achia mbali ushuhuda wa Nabii (s.a.w.w) kuwa Fatima ni miongoni mwa watu wa Janna. Abu Bakr akasema: 'Mwanaume na mwanaume na mwanamke.'

Lakini akasadiki maneno ya wake walipodai chumba, hivyo hakukifanya chumba kuwa ni sadaka. Ndipo Fatima alimuusia Ali na alitilia mkazo kabisa usia huo, kuwa amzike usiku ili asije akaswaliwa na Abubakr.[167]

Kwa ajili ya matukio hayo Abu Bakr akasema: "Niuzuluni mimi sio mbora kwenu na Ali akiwa kati yenu."[168] Ikiwa ni mkweli haitokuwa sahihi amtanguliye Ali bin Abu Talibi (a.s.). Na ikiwa ni mwongo si vyema awe imamu. Usemi wake huu hauchukuliwi kuwa amefanya unyenyekevu, yaani usemi wa kuonyesha adabu, kwa kuwa ni jambo linalolazimu kuutangua uimamu na linalomshambulia yeye mwenyewe.

Na Abu Bakr alipata kusema kuwa "Kwa kweli mimi hupagawa na Shetani, nikipotoka ninyoosheni."[169] Na ambaye hupagawa na Shetani si vyema awe imamu!! Na Umar akasema kumhusu Abu Bakr: "Kwa kweli bai'a ya Abu Bakr ilikuwa ni tendo la fujo isiotarajiwa, Mwenyezi Mungu amewalinda waislamu mbali na shari yake, hivyo basi mwenye kurejea kufanya mfano wake muuweni." Kwa hiyo imebainika kuwa bai'a ya Abu Bakr ilikuwa ya mpango usio sawa, na kuwa ni wajibu kuuwana juu ya mfano wa tendo kama hilo.

Na Abu Bakr alikwepa kwenda na jeshi la Usamah ambalo Mtume (s.a.w.w.) alimfanya amiri jeshi wake (yaani Amiri-jeshi wa Abu Bakr). Na katu Mtume hakuwahi kumfanya mtu yeyote kuwa amirijeshi wa Ali (a.s.).[170]

Pia ikumbukwe kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) hakuwahi kumtawaza Abu Bakr kwa kazi yoyote katika zama zake katu, ila kuifikisha Sura ya Bara'a.

Na alipotoka Mwenyezi Mungu (s.w.t.) alimuamuru Mtume wake amuengue na akamkabidhi wadhifa wa kuifikisha Sura hiyo Ali (a.s).

Pia izingatiwe kuwa Abu Bakr hakuwa na ujuzi wa kutosha wa hukumu za kisharia, kuthibitisha hilo katika utekelezaji wake wa hadi za kisheria aliukata mkono wa kushoto wa mwizi, na alimuunguza kwa moto al-Fajaata al-Salmiy at-Taymiy.[171] Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alikwishasema: "Asiadhibu kwa moto ila Mola wa moto."[172]

Na alipoulizwa kuhusu msamiati *al-Kalalatu*173 hakujuwa la kusema na akasema: “Nasema kwa rai yangu ikiwa sawa ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu na ikiwa kosa ni kutoka kwa Shetani.” Na bibi alimuuliza kuhusu mirathi yake, yaani mirathi yake kwa mjukuu, akasema: “Sikuti kitu kwa ajili yako ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu wala katika Sunna ya Muhammad, rejea mpaka niulize. Mughira bin Shuuba alimpa khabari kuwa: Nabii (s.a.w.w.) alikuwa amempa sudusi, yaani moja katika sita. Na ukweli ni kuwa Abu Bakr alikuwa anawauliza maswahaba kuhusu hukumu nyingi.

Na Abu Bakr hakumkanusha Khalid bin al-Walidi kwa kumuuwa Malik bin Nuwayra, wala kwa kumuoa mkewe usiku ule ule aliouawa bila ya eda.

Na Abu Bakr alituma watu waende kwenye nyumba ya Amiril-Muuminiina (a.s.), alipojizuia kufanya bai'a, wakawasha moto174 kwenye nyumba yake ndani mkiwemo Fatima (a.s.) na jamaa katika Bani Hashim na watu wengine. Na walimkanusha kwa tendo hilo.

Na Abu Bakr alipopanda mimbari ya Mtukufu Mtume punde alikuja Hasan na Husein na jamaa miongoni mwa Bani Hashim na wengine wal- imkanusha, na Hasan na Husein wakasema: “Hii nafasi ya babu yetu na wewe haustahiki.”175

Na Abu Bakr alipokabiliwa na hali ya umauti, akasema: “Ni afadhali ningeiacha nyumba ya Fatima bila kuikashifu, na ni bora ningemuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) je Answar wana haki kwenye jambo hili?” Na akasema laiti nilipokuwa katika kibanda cha Bani Saida ningepiga juu ya mkono wa mmoja wapo kati ya watu wawili, yeye angekuwa amiri na mimi ningekuwa waziri.”176

Na kulingana na itikadi yenu nyinyi, Abu Bakr alifanya kinyume na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) kwa kumwainisha khalifa, kwa kuwa yeye, Abu Bakr, alimfanya Umar bin al-Khattab khalifa, na Nabii (s.a.w.w) hakumfanya walii kwa kazi yeyote ile isipokuwa vita vya Khaybari, na alirejea akiwa ameshindwa.

Na alimfanya walii wa kusimamia sadaka, na Abbas alipolalamika dhidi yake Nabii (s.a.w.w) alimuuzulu. Na Swahaba walimpinga Abu Bakr kitendo chake cha kumtawaza Umar ukhalifa, kiasi kwamba hata Talha akasema: “Umemtawaza Umar mkali mwenye tabia ngumu.”

Amma kumhusu Umar, yeye aliletewa mwanamke aliyezini akiwa na mimba. Aliamuru apigwe mawe mpaka afe. Ali akasema: Ikiwa una sababu kwa mwanamke hauna sababu kuhusu mimba yake. Alijizuia, na akasema: “Lau si Ali Umar angehiliki.”

Umar alishuku kufa kwa Nabii (s.a.w.w.) na akasema: Muhammad hakufa wala hafi, mpaka Abu Bakr alipomsomea Aya hii: **“Kwa hakika wewe utakufa, na hakika wao watakufa.”** (***Sura Zumar*: 30**). Akasema: “Sadakta.” Na akasema: “Kana kwamba mimi sijaisikia Aya hiyo.”177

Na walimletea Umar mwanamke kichaa aliyezini. Aliamuru arujumiwe. Ali (a.s.) alimwambia: “Kalamu haifanyi kazi dhidi ya kichaa mpaka azindukiwe na akili.” Akaacha. Akasema: “Lau si Ali Umar

angeangamia.”

Na akasema katika moja ya hotuba zake: “Mwenye kuifanya mahari ya mkewe ghali nitaitia katika hazina kuu ya waislamu. Mwanamke mmoja akamwambia: “Unatuzuia ambalo Mwenyezi Mungu ametuhalalishia aliposema:

وَإِنْ أَرَدْتُمُ اسْتِبْدَالَ زَوْجٍ مَكَانَ زَوْجٍ وَآتَيْتُمْ إِحْدَاهُنَّ قِنْطَارًا فَلَا تَأْخُذُوا مِنْهُ شَيْئًا ۚ أَتَأْخُذُونَهُ بُهْتَانًا وَإِثْمًا مُبِينًا {20}

***“Na kama mkitaka kubadilisha mke mahala pa mke, na hali mmoja wao mmempa mali chungu nzima, basi msichukue chochote katika hicho. Je, mtachukua kwa dhulma na kosa lililo wazi?” (Sura Nisai: 20).***

Akasema: “Watu wote wanajua fiqhi kuliko Umari hata watawa wa kike waliopo majumbani.”178

Na alikuwa anampa Hafsa na Aisha kila mmoja Dirhamu mia mbili elfu. Na alichukua kutoka Baytul’mali Dirham mia mbili elfu. Waislamu walilipinga hilo. Yeye akasema: “Nimezichukuwa kwa mkopo.”179 Na aliwanyima Hasan na Husain (a.s.) mirathi yao kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na aliwazuia khumsi.180

Na Umar alipitisha hukumu za hadi sabini, na alizidisha katika kuwapa na katika mgao, na alizuia Muta mbili na akasema: “Muta mbili zilikuwa halali zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na mimi ni mwenye kuziharamisha, na ni mwenye kumwadhibu mwenye kuzifanya.”181

Na alifanya kinyume na Nabii (s.a.w.w.) na Abu Bakr katika *Nassu* na bila ya *Nassu.* Kwa kuwa yeye aliujaalia ukhalifa katika watu sita, na kisha alijipinga binafsi akaujaalia katika watu wanne, kisha katika watatu, kisha katika mmoja.

Na alijaalia haki ya kuchagua kwa Abdur Rahman bin Aufi baada ya kuwa alikwishamuelezea kuwa ni dhaifu na mzembe. Kisha akasema: “Akijumuika Ali na Uthman kauli ni waliyoisema wao. Na wakiwa watatu watatu kauli ni ya wale ambao Abdur Rahman bin Aufi yuko pamoja nao.”

Kwa sababu alijua kuwa Ali na Uthman hawatokuwa kwenye jambo moja, na kuwa kuwa Abdur Rahman bin Aufi hatoliweka jambo mbali na mwana wa dada yake ambaye ni Uthman. Kisha aliamuru kukatwa shingo ya mwenye kuchelewa kufanya bai’a baada ya siku tatu.182

Pia Umar alichana barua ya Bibi Fatma (a.s.) na hilo lilikuwa pale mzozo ulipokuwa mrefu kati ya Fatima (a.s.) na Abu Bakr, Abu Bakr alimrudishia Fadak na posho, na alimwandikia barua, basi alitoka na ile barua ikiwa mkononi mwake, hapo alikutana na Umar alimuuliza shida yake. Fatima alimueleza kisa chake, na Umar alichukua kutoka mkononi mwake ile barua na akaichana.183

Fatima alimwacha, na Umar aliingia kwa Abu Bakr na alimlaumu kwa kumrudishia Fatima Fadak. Wawili hao Abu Bakr na Umar waliafikiana kumnyima Fatima.

Ama kuhusu Uthman bin Affan alijaalia ugavana wa majimbo kati ya ndugu zake wa karibu, al-Walid nduguye upande wa mama yake alimfanya gavana wa Kufa, akanywa pombe, na aliwaswalisha watu akiwa amelewa.[184] Watu wa Kufa walimfukuza likajitokeza kutokana na yeye lililojitokeza.

Na aliwapa mali nyingi waume wa mabinti wake wanne, akampa kila mmoja gramu laki moja za dhahabu kutoka Baytul'mali ya waislamu, na alimpa Marwan Dirham milioni moja kutoka katika khumsi ya Afrika.[185]

Na Uthman alijihami binafsi mbali na waislamu na aliwazuia na walibaki kando na yeye, na kwake vilitokea vitendo viovu kuwahusu swahaba. Alimpiga Ibnu Mas'udi[186] mpaka alikufa na msahafu wake aliuunguza. Ibnu Mas'udi alikuwa akimkebehi Uthman na kumkufurisha.

Na alimpiga Ammar bin Yasir swahiba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) mpaka aliteguka.[187]

Alimleta Abu Dharr kutoka Sham kwa utashi wa Muawiya, alipofika alimpiga na kumhamishia Rabdhwa.[188] Hali ilikuwa Nabii (s.a.w.w.) alikuwa anawaweka karibu hawa watatu.

Na Uthman alimwondolea adhabu ya kisasi Ibnu Umar kwa kumuuwa Nawar baada ya uislamu. Na alitaka kumuondolea adhabu ya kunywa pombe al-Walid bin Utbah fasiki mkubwa, Ali (a.s.) alimtekelezea adhabu.

Na swahaba walimtelekeza mpaka aliuawa na hakuzikwa ila baada ya siku tatu na walimzika mahali paitwapo *Hashukaukab.*

Na alitoweka mbali na waislamu siku ya Badri, na siku ya Uhud, na Baiy'atu ridhwan. Na yeye alikuwa sababu ya Muawiya kumpiga vita Ali (a.s.) kwa ajili ya ukhalifa. Hali ilifikia Bani Umayyah kumtukana Ali (a.s.) juu ya mimbari.

Na walimuuwa Hasan kwa sumu na kumuuwa Husein kikatili. Na waliwatangaza wana wa Nabii (s.a.w.w.) na dhuria zake katika miji wakizungushwa wakiwa juu ya wanyama.[189]

Suala likaishia kwa al-Hajjaj naye aliwauwa Aali Muhammad kumi na mbili elfu, na wengi miongoni mwao aliwajengea kwenye kuta wakiwa hai.Yote hayo yalitendeka sababu ni kuwa wao wameufanya uimamu kwa hiyari na utashi. Lau wao katika hilo wangefuata agizo la Mtume, na wala Umar lau asingekwenda kinyume na Nabii (s.a.w.w.) katika kauli yake: "Nileteeni kidau cha wino na mfupa wa bega nikuandikieni maandiko ambayo hamtopotea baada yake abadan." basi tofauti na upotovu kama huu havingetokea kabisa.

Yohana akasema: Oh! Nyie wanachuoni wa dini, hawa wanaoitwa Rafidhwa, hii tulioitaja ndio itikadi yao, na nyinyi hii tuliyoikiri ndio itikadi yenu, na dalili yao ni hii mliyoisikia, na dalili yenu ni hii mliyoinakili. Ni

kundi gani kati ya mawili haya wana haki katika jambo hili ikiwa mnajua?

Kwa kauli moja wakasema: Wallahi kwa kweli Rafidhu wako na haki, na wao ni wakweli katika kauli zao. Lakini suala hili limepita kama lilivyopita, kwani wangali wenye haki ni wenye kukandamizwa, tushuhudie ewe Yohana sisi ni wenye kuwapenda Aali Muhammad, na tunajiepusha mbali na maadui zao, isipokuwa tunakuomba tufichie suala letu hili kwa kuwa watu wapo katika dini ya wafalme wao.

Yohana akasema: Nilitoka kwao na mimi nikiwa najua dalili yangu, mwenye imani na itikadi yangu, kwa yakini Mwenyezi Mungu ndiye mwenye himidi na hisani, na ambaye Mungu humuongoza ndiye mwenye kuongoka.

Hivyo basi nimeandika risala hii ili iwe mwongozo kwa mwenye kuitafuta njia ya uokovu, kwa mwenye kuiangalia kwa jicho la insafu huongozwa kwenye usawa, na atakuwa na ujira kwa hilo, na mwenye kupigwa muhuri moyoni mwake na ulimini mwake hapana njia ya kumwongoza kama Mwenyezi Mungu (s.w.t.) alivyosema:

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ۚ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ {56}

***"Kwa hakika wewe humwongoi umpendaye, lakini Mwenyezi Mungu humwongoa amtakaye."* (*Sura Al-Qasas: 56*).**
Kwa kweli waliowengi miongoni mwa wenye chuki binafsi:

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ أَأَنْذَرْتَهُمْ أَمْ لَمْ تُنْذِرْهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ {6}

خَتَمَ اللَّهُ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ وَعَلَىٰ سَمْعِهِمْ ۖ وَعَلَىٰ أَبْصَارِهِمْ غِشَاوَةٌ ۖ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ {7}

***"Ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye, hawaamini. Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na juu ya masikio yao, na juu ya macho yao pana kifuniko. Basi watapata adhabu kubwa."* (*Surat Al-Baqarah: 6-7*)**

Oh! Allah hakika sisi tunakuhimidi kwa ajili ya neema zako kubwa mno, na tunamtakia rehma Muhammad na ahali wake waliotoharishwa miongoni mwa watu, siku zote mpaka siku ya Kiyama.

Mpaka hapa ndipo tulipopafahamu kutoka katika kitabu hiki kilichotajwa.[190] Na Mwenyezi Mungu (s.w.t.)

ni mstahiki wa sifa njema.

---

1. Mizanul-Ijtihad, Uk. 14.
2. Ni kodi ambayo hutozwa Kafiri anayeishi kwenye ardhi ya Waislamu.
3. Al-Bidaya Wan-Nihaya Juz. 4, Uk.76. al-Imam Sadiq Wal-Madhahibul-Arbaa Uk.190.
4. Ibnu Al-Athir Juz. 8, Uk. 229.
5. Tadhkiratul-Huffadh Juz. 3 Uk. 375.
6. Rejea kitabu Shadharatu dhahbi Juz.3. Uk. 252.
7. Tabaqatus-Shafiiyyah Juz. 4 Uk.184.
8. Al-Yaaqutu Fil-Waadhi, cha Abu Faraji Ali bin al-Jawziy Uk. 48.
9. Al-Yaaqutu Fil-Waadhi, cha Abu Faraji Ali bin al-Jawziy Uk. 48.
10. Mashariqul-Anwar cha Adwiy Uk. 88.
11. Ad-Diin Al-Khalisw Juz. 3, Uk. 355.
12. Tabaqatus-Shafiiyyah Juz. 3, Uk. 22.
13. Al-Kashafu cha Zamakhshariy Juz. 2, Uk. 498.
14. Imam Sadiq Wal-Madhahibul-Arbaa. Juz.1. Uk 285.
15. Al-Intiqaau cha Ibnu Abdil-Bar Uk. 5.
16. Tarikhut-Tashriiul-Islam cha Al-Khidhriy, Uk. 275.
17. Abu Hanifa cha Muhammad Abu Zahra.Uk.5
18. Abu Hanifa cha Muhammad Abu Zahra.Uk.5.
19. Al Khatib Juz.13. Uk.374.-
20. Al-Intiqaau cha Ibnu Abdil-Bar Uk. 148.
21. Al Khatib Juz.3. Uk.374.
22. Ta'awilu Mukhtalafil-Hadithi cha Abu Qutayba Uk.63.
23. Al-Intiqaau, cha Ibnu Abdil-Bar Uk. 150.
24. Al-Intiqaau, cha Ibnu Abdil-Bar Uk. 150.
25. Manaqibu Abihanifa cha Muwafiq Juz.1, Uk. 137. Tadhkiratul-Huffadhi cha Ad-Dhahabi Juz.1, Uk.157.
26. At-Tabaqaatul-Kubra cha Shaaraniy Juz.1, Uk. 28.
27. Ni aina ya meno manne ya mbele.
28. Wafayatul-Aayaan Juz. 1, Uk. 212. Shadharatu Dhahab. Juz.1, Uk. 220.
29. Al-Imam Sadiq, cha Abdilhaliim al-Jundiy. Kwenye pambizo Uk.180.
30. Al-Imam Sadiq, cha Abdilhaliim al-Jundiy. Kwenye pambizo Uk.162.
31. Al-Imam Sadiq, cha Abdilhaliim al-Jundiy. Kwenye pambizo Uk.163.
32. Twabaqatul-Fuqahaa cha Abu Is'haqa.
33. Imamah Wasiyasa. Juz. 2, Uk. 156.
34. Muujamul-Udabai Juz.11. Uk.275.
35. Imam Sadiq Mualimul-Insan.Uk.24, cha Ibn Shahri Ashwab.
36. Imam Sadiq Mualimul-Insan.Uk. 52, cha Ibn Shahri Ashwab.
37. Sharhul-Muwatau cha Zurqaniy Juz.1,Uk. 8.
38. Al-Imam Swadiq Wal-Madhahibil –Aabaa Juz. 1 Uk. 166.
39. Ibnu Khalkan, Juz. 2, Uk. 116.
40. Ni Kadhi wa madhehebu ya Malik, aliyeyaeneza huko Uhispania.
41. Manaqibu Malik cha az-Zaawiy. Uk. 17- 18.
42. Ar-Rahmatul-Ghaibiyah cha Ibnu Hajar Uk. 6.
43. Tarikhu Baghdad, Juz.10, Uk.164.
44. Jaamiu Fadhailul-Ilmi Juz. 2, Uk. 158.

45. Jaamiu Fadhailul-Ilmi Juz. 2, Uk. 158.
46. Al-Khatib al-Baghdadiy Juz. 2, Uk. 175.
47. Al-Imam Swadiq Wal-Madhahibil –Aabaa Juz. 1, Uk. 498.
48. Tadhkiratul-Huffadhi Jalada la 1. Uk.176.
49. Tahdhibut-Tahdhib
50. Al-Manaqib cha Al-Bazzazu.Jalada 1. 153.
51. Jamiu Bayanil-Ilmi Wafadhlihi.
52. Tawali At-Taasisi. Uk.86.
53. Al-Laaliy al-Masnunah cha Suyutiy, Juz. 1, Uk. 217.
54. Al-Intiqau, Uk. 70.
55. Ahmad bin Hanbal, cha Abu Zahrah. Uk.198.
56. al- Imam Sadiq Wal-Madhahibul-Arbaa Juz. 2, Uk. 453.
57. Utangulizi wa Ahmad bin Hanbal Wal-Mihnah, Uk. 14, nukuu kutoka katika pambizo ya al-Kamil, Juz. 3, Uk. 131-139.
58. Tarikhul-Yaaqubiy. Uk.198.
59. Tabaqatush-Shafiiyah Juz. 1, Uk. 270.
60. Dhuhrul-Islam Jalada. 4. Uk. 8.
61. Tarikhu Ibn Kathiir Juz.10.Uk.239.
62. Tarikhul-Madhahibil-Islamiya cha Abu Zahra, Juz. 2, Uk. 322.
63. Tarikhut-Tabariy. Jalada 4. Matukio ya mwaka 61. A.H.
64. Tarikh Baghdad. Jalada, Jz. 2, Uk. 66.
65. Manaqibu Ahmad, Uk. 75.
66. Tarikh Baghdad, Jalada la 4, Uk. 119.
67. Ahmad bin Hanbal, cha Abu Zahra, Uk. 196.
68. Ahmad bin Hanbal, cha Abu Zahra, Uk. 168
69. al- Imam Sadiq Wal-Madhahibul-Arbaa Juz.2. Uk.509.
70. Dhuhal-Islam Juz. 2, Uk. 235, cha Ahmad Amin.
71. Dhuhrul-Islam, Juz. 4, Uk. 96.
72. Wasailus-Shia Jalada la 18, Uk. 94.
73. Angalia: al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa Jalada, 4, Uk. 14 – 15.
74. Angalia al-Ummu cha Shafii Juz. 5, Uk. 22- 25.
75. al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa Jalada la 5. Uk, 119.
76. Na mfano wake ni kama alivyosema katika Juz. 13, ndani ya Tarikh Baghdad Uk. 370 kuwa: "al-Harithu bin Umayr amesema: 'Na nilimsikia anasema (Abu Hanifa): Endapo mashahidi wawili watashuhudia mbele ya Kadhi, kuwa fulani bin fulani amemtaliki aliyekuwa mke wake, na wote wakawa wanajua kuwa hawa wametoa ushaidi wa uwongo, na Kadhi akawatenganisha, halafu mmoja wa mashahidi wawili akakutana na yule mwanamke anaweza kumuoa."'
77. al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa, Jalada la 5, Uk. 129
78. al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa, Jalada la 5, Uk. 141.
79. Al-Mustadrak cha Hakim. Juz. 4, Uk. 355. Kanzul-Ummal Juz. 5,Uk. 340 Hadithi ya 13129.
80. Al-Fatawa Al-Khayriya, Juz. 2, Uk. 150.
81. al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa, Jalada la 5, Uk. 123.
82. al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa Jalada la 5, Uk. 124.
83. al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa Jalada 1. Uk. 63.
84. al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa Jalada 1. Uk. 117.
85. Musnad Ahmad Juz. 1, Uk. 25, Hilyatul-Awliyai, Juz.6, Uk. 242. as-Sunanl- Kubra cha Bayhaqiy Juz.1, Uk. 41
86. al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa Jalada 1, Uk. 242.
87. al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa Jalada 1, Uk. 26.
88. al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa Jalada 1, Uk. 68. al -Fiqhi Alal-Madhahibil- Khamsah Uk. 37.
89. al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa Jalada 1, Uk. 26.

90. al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa Jalada 1, Uk. 230.
91. al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa Jalada 1, Uk. 307.
92. al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa Jalada 5. Uk. 134.
93. Angalia al-Ummu cha Shafii Jalada 6, Uk. 208, al-Fiqhul-Islamiy Waadilatuhu Juz. 5, Uk. 566.
94. al-Fiqhul-Islamiy Waadilatuhu Juz. 7, Uk. 128.
95. al -Fiqhi Alal-Madhahibil-Arbaa Jalada 5, Uk. 140.
96. al-Imam Swaadiq Wal-Madhaahibul-Arbaa Juz. 2, Uk. 509. Na miongoni mwa walioeleza kuwa Yeye Taala huteremka mpaka mbingu ya dunia ni Bukhari katika mlango wa ibada za usiku. Na Musnad Amad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 120 na Uk. 446. Na at-Tirmidhiy Juz. 1, Uk. 142.
97. Sahih Muslim, Juz. 1, Uk. 51 – 53.
98. Musanad Ahmad Juz. 5, Uk. 25; al-Muujam al-Kabiir cha Tabraniy Juz. 20, Uk. 229-230 Hadithi ya 538. Majmauz-Zawaidi Juz. 9,Uk. 102. Kanzul-Ummal. Juz. 11, Uk. 605 Hadithi ya 32924.
99. al-Muujamu al-Kabiir cha Tabraniy Juz. 1, Uk. 226, Hadithi ya 730; Taarikh Baghdad Juz. 9, Uk. 369; Kanzul-Ummal Juz.13, Uk. 167. Hadithi ya 36507. Na Hadithi hii imefanyiwa vitabu vya peke yake. Mfano kitabu Qisatut-Tayr cha Haakim an-Nisaburiy aliyetawafu mwaka 305 A.H. Na baadhi ya rejea za Hadith hii zimetangulia. Rejea huko.
100. Sahih Tirmidhiy, Jalada la 5, Uk. 595, Hadithi ya 3721. Majmauz-Zawaidi. Juz. 9, Uk. 126. al-Mustadrak. Juz. 3, Uk. 130-131. Mishkatul-Maswabiih cha Al- Khatib at-Tabriziy Juz. 3, Uk. 1721. Hadithi ya 6085. Khaswaisu Amiril- Muuminina cha Nasaiy Uk. 34. Hadithi ya 12.
101. Manaqibul-Khawarzamiy Uk.110 Hadithi ya 18. Faraidus-Samtaini. Jalada.1, Uk. 223 Hadith ya 174.
102. Kifayatut-Talibi.Uk. 270. Hilyatul-Awliyai. Juz. 1, Uk. 65 – 66.
103. Yeye ni Abdullah bin Muhammad. Lakabu yake ni al-Akbar. Na kuniya yake ni Abu Hashim, ni Imam wa Kaysania. Amefariki mwaka 98 au 99. Angalia Tanqihul-Maqaal cha al-Mamaqaniy Juz. 2, Uk. 212.
104. Sharh Nahjul-Balagha cha Ibnu Abul-Hadid Juz. 1, Uk. 17.
105. Sharh Nahjul-Balagha cha Ibnu Abul-Hadid Juz. 1, Uk. 17-18.
106. Manaqibul-Khuwarzamiy Uk. 26, Uk. 96- 97. Hadithi ya 97 na 98. Faraidus- Samtini. Jalada la 1, Uk. 344-345, Hadithi ya 266 na 267.
107. Faydhul-Qadir Juz. 4, Uk. 357. Fadhailul-Khamsa Minaswihahi Sita, Jalada la 2, Uk. 309. Manaqib Ibnu Shahri Ashub Juz. 2, Uk. 361. Aliyu Imamul- Muttaqiyna cha Abdur Rahman As-Sharqawiy Juz. 1, Uk. 100-101.
108. Al-Bidayatu Wan-Nihaya. Juz. 7, Uk. 356. Kifayatut-Talib, Uk. 121.
109. Kanzul-Ummal Uk. 226. Ar-Riyadh An-Nadhrah Juz. 2, Uk. 218. Kifayatut- Talib Uk. 122. Al-Ghadir Juz. 3, Uk. 353.
110. Al-Muwatau cha Malik.Jalada 2. Uk. 842. Hadithi ya 2. al-Mustadrak. Juz.Uk.375. Fadhailul-Khamsa.Juz.2. Uk.310.
111. al-Istiiabu Juz. 3, Uk.1106. Sharhu Nahjul-Balagha cha Ibnu Abi Hadid Juz.1, Uk. 19. Na Al-Qurtubi ameitaja ndani ya tafsiri yake Juz. 16, Uk. 390, anapozungumzia kauli ya Mwenyezi Mungu: “Na kumbeba na kumwachisha ziwa ni miezi thelathini.” (Sura Ahqaf: 15), amesema kuwa: Uthman aliletewa mwanamke ambaye alijifungua baada ya miezi sita, akataka kumpiga hadi, ndipo Ali akamwambia hastahili kufanyiwa hivyo, Mwenyezi Mungu amesema: “Na kumbeba na kumwachisha ziwa ni miezi thelathini.” (Sura Ahqaf: 15).
112. Al-Istiab Juz. 3, Uk. 1105-1106. Fadhailul-Khamsa Minaswihahi-Sita Juz. 2, Uk. 302. Dhakhairul-Uqba Uk. 84. as-Swawaiqul-Muhriqa, Uk. 77.
113. Manaqibu Ibnu Shahri Ashub Juz. 2, Uk. 367. al-Fusulul-Mia Juz. 5,Uk. 366. Hadihti ya 15. Kanzul-Ummal, Juz. 3, Uk. 379. Biharul-Anwar Juz. 40, Uk. 252. Al-Ghadir Juz. 6 Uk. 174.
114. Kanzul-Ummal, Juz. 3, Uk. 179. Biharul-Anwar Juz. 40, Uk. 257.
115. Sharhu Nahjul-Balagha cha Ibnu Abi Hadid Juz. 9, Uk. 231. Kitabul-Ummi Juz. 4, Uk. 233, Shafii amesema: “Tuliijua hukumu ya wazinzi toka kwa Ali (a.s.).”
116. Imeelezwa kuwa Umar bin al-Khattab aliletewa mwanamke mja mzito aliyekiri kuwa amefanya zinaa, akatoa amri arujumiwe. Punde si punde Ali (a.s.) alifika kabla hukumu haijatekelezwa, ndipo akasema: “Ana nini huyu mwanamke?” Wakasema: “Umar ameamuru arujumiwe.” Ali (a.s.) alimwita Umar na akasema: “Huyu una mamlaka naye hivi, lakini una mamlaka gani na kilichokuwa tumboni mwake? Huenda wewe umemkemea au umemtisha.” Akasema: “Hilo lilikuwa.” Ali akasema: “Je haukumsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) akisema: Hapana hadi kwa aliyekubali baada ya balaa,

kwa kuwa mwenye kufungwa kamba au kutiwa mahabusi au kutishwa hana kukiri." Hapo Umar alimwacha huru, halafu akasema: "Wanawake wameshindwa kumzaa mfano wa Ali bin Abu Talib. Lau si Ali Umar angeangamia." Rejea Riyadhu An-Nadhrah Juz. 3, Uk. 163. Dhakhairul-Uqbah, Uk. 81. Matalibus-Suul, Uk. 13. Manaqibul- Khawarzamiy Uk. 48. Al-Arbaiin cha Fakhru Raziy, Uk. 466. Al-Ghadir Juz. 6, Uk. 110.
117. Nahjul-Haqi Wakashfus-Swidqi, Uk. 228. Sharh Nahjul-Balagha cha Ibnu Abil Hadid.Juz.1, Uk. 119.
118. Sharh Nahjul-Balagha cha Ibnu Abul-Hadid Juz. 7, Uk. 253.
119. Tari'kh Tabari, Jz. 1 uk. 245; Tabaqaat ibn Sa'ad, Jz. 3, Uk. 103; al-Imama was-Siyasa cha Ibn Qutaybah, uk. 6; Maj'maul-Zawa'id, Jz.5 uk. 183 na vinginevyo.
120. Sharh Nahjul-Balagha cha Ibnu Abul-Hadid Juz. 7, Uk. 253.
121. Sharh Nahjul-Balagha, cha Ibnu Abul-Hadid Juz. 1, Uk. 26.
122. Irshadu cha Sheikh Mufiidu Uk.256. Iilamul-Wara Uk.255. Biharul-Anwar Juz.46. Uk.74.Hadithi ya 62.Uk.314.
123. Sharh Nahjul-Balagha cha Ibnu Abul-Hadid Juz.1.Uk. 20.
124. al-Maghaaziy cha Al-Waaqidiy Juz.1. Uk.92.
125. Muwasatu: Ni kumsaidia mtu, ila ukweli wa maana yake ni zaidi ya kusaidia, bali ni kumtendea mtu kama unavyopaswa kujitendea.
126. Dhakhairul-Uqba Uk. 68. Fadhwailus-Swahaba cha Ahmad Juz. 2, Uk. 594. Hadithi ya 1010. Majmauz-Zawaidi Juz. 6, Uk. 114. Nahjul-Haqi Wakashfus-idqi. Uk. 249.
127. Taarikhut-Tabariy Juz. 2, Uk. 203. al-Kamil cha Ibnul-Athiir, Juz. 2, Uk. 110. Syra al-Halabiya Juz. 2, Uk. 227. al-Bidaya Wan-Nihaya, Juz. 4, Uk. 28. Syra Nabawiyah cha Ibnu Kathiir, Juz. 3, Uk. 55. Sharhu Nahjul-Balagha cha Ibnu Abil-Hadid Juz.15, Uk. 21. Durul-Manthur Juz. 2, Uk. 89.
128. Al-Maghaziy cha al-Waqidiy Juz. 2, Uk. 470 – 471. Habari ya kuuliwa kwa Umar bin Abdil-Wud imetangulia.
129. Sharhu Nahjul-Balagha cha Ibnu Abil-Hadid Juz. 1, Uk. 20 na Juz. 8, Uk. 53.
130. Naye ni dada yake Amru Abil-Wuud, jina lake ni Amratu, na kunia yake ni Ummu Kulthum.
131. Al-Mustadrak Alas-Swahihayni Juz. 3, Uk. 33. al-Fusulul-Muhimah cha Ibnu Swabaghiy al-Maliky. Uk. 62. al-Irshaadu cha Sheikh Mufiid Juz. 1, Uk. 108 . Lisanul-Arabi cha Ibnu Mandhuur, Juz. 7,Uk. 127.
132. Sharhu Nahjul-Balagha cha Ibnu Abil-Hadid Juz.1, Uk. 22.
133. Nahjul-Balagha cha Subhi Swalih.Uk. 480-481, hekima fupifupi 77.
134. Tarjumatul-Imam Ali bin Abi Talib, kutoka katika Tarikh Dimishqi cha Ibnu Asakir. Juz.1, Uk.,205 Hadithi ya 269, na Uk. 157 Hadithi ya 219 – 231. Sunan Tirmidhiy, Juz. 5, Uk. 596. Hadithi ya 3724. Faraidus-Simtaini Juz. 1, Uk. 259. Majmauz-Zawaidi, Juz. 6, Uk.151 . al-Mustadrak cha Haakim Juz. 3, Uk. 38 na Uk. 437. Uyunul-Athar, Juz. 2. Uk.132. Musnad Ahmad bin Hanbal Juz. 2. Uk. 384. Sahih Muslim Juz. 4. Uk. 1878. Hadithi ya 33 – ( 2405). Ansabul-Ashrafi cha Baladhuriy, Juz. 2, Uk. 93. Khaswaisun-Nisaiy Uk.34. Hadithi ya 11. Manaqibu Ali bin Abi Talib cha Ibnu Al-Maghaziliy, Uk. 181. Hadithi ya 216. Tabaqatu cha Ibnu Saad, Juz. 2, Uk. 110. Yanabiul-Mawaddah, Uk. 49. al-Muujamul-Swaghiir cha Tabaraniy Juz. 2, Uk. 100. Musnad Abidaudi at-Tayalisiy. Uk. 320. Tadhkiratul-Khawasi cha Sibtu Ibnu Al-Jawziy Uk. 24. Sunanul-Kubra cha Al- Bayhaqiy Juz. 9, Uk. 106 na Uk. 131. Hilyatul-Awliyai Juz. 1, Uk. 62. Asnal- Matalibi cha Sakhriy. Uk. 62. Sahih Bukhari, Juz. 5, Uk. 22. Usudul-Ghabah. Juz.4, Uk. 21. al-Bidaya Wan-Nihaya Juz. 4, Uk. 182. Tariikhut-Tabariy, Juz. 3, Uk. 12. Dhakhairul-Uqba, Uk. 87. Tarikhul-Islam cha Dhahabiy, Juz. 2, Uk. 194. Iqdul-Fariidi, Juz. Uk. 194. al-Kamilu Fii Tariikh. Juz. 2, Uk. 149. Murujudhahabi Juz. 3, Uk. 14. Ihqaqul-Haqi. Juz. 5, Uk. 400. Fadhailul-Khamsa Juz. 2, Uk. 161.
135. Lisanul-Mizan Juz. 5, Uk. 219. Mizanul-Iitidal. Juz. 2, Uk. 597.
136. Manaqibul-Khawarzamiy, Uk. 67. Hadithi ya 39. al-Firdawsu, Juz. 3, Uk. 373. Hadithi ya 5135.
137. Manaqibul-Khawarzamiy, Uk. 75, Hadithi ya 56. al-Firdawsu, Juz. 2, Uk. 142. Hadithi ya 2725.
138. Musnad Ahmad Juz.1, Uk. 77. Sunan Tirmidhiy Juz. 5, Uk. 599. Hadithi ya 3733. Tarikh Baghdad Juz. 13, Uk. 288. Kanzul-Ummal Juz. 13, Uk. 639. Hadith ya 37613.
139. Sahih Bukhari. Jalada la 4, Uk. 2, Sahih Muslim, Juz. 3, Uk. 1249, Hadithi ya 1; Sunan Ibnu Majah Juz. 2, Uk. 901, Hadithi ya 2699.
140. Manaqib Ibnu al-Maghaziliy, Uk. 200-201, Hadithi ya 238. Dhakhairul- Uqba, Uk. 71.
141. Maalimut-Tanzili cha Baghwiy, Juz. 3, Uk. 400.

142. Musnad Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 159.
143. Tarikhu Tabariy Juz. 2, Uk. 319- 321
144. Musnad Ahmad bin Hanbal, Juz. 2, Uk. 93, na Juz. 4, uk. 368 na Uk. 372; na Uk. 381.
145. Al-Iqdu al-Fariid. Juz. 5, Uk. 61.
146. Faraidus-Samtwayn Juz. 1, Uk. 82, hadithi ya 53. Nurul-Abswar cha Shablanjiy Uk. 71, chapa ya Saadiya na Uk. 71 chapa ya Uthmaniya. Yanabiul- Mawaddah Uk. 328, chapa ya Al-Haydariya na Uk. 374, chapa ya Istanbul, na Juz.2, Uk. 99, chapa ya Irfan Swayda.
147. Angalia Maalimut-Tanziil cha al-Baghawiy Juz. 4, Uk. 465; Majmaul-Bayan, Juz. 10, Uk. 462. Japo kuna tofauti kidogo.
148. Sahih Bukhariy Juz. 6. Uk.81.
149. Sunan Tirmidhiy Juz. 5.Uk.256 - 257. Hadithi ya 3090 – 3092 na Juz.3. Uk.222 Hadithi ya 871.
150. Musnad Ahmad Juz. 3, Uk. 212; al-Muswanifu cha Ibnu Abi Shayba Uk. 84- 85 Hadithi ya 12184. Kanzul-Ummal Juz. 2, Uk. 431 Hadithi ya 4421. al-Bidaya Wan-Nihaya Juz. 5, Uk. 37.
151. Al-Muujamus-Swaghir cha Tabaraniy Juz.1, Uk. 256; Kanzul-Ummal, Juz.1, Uk. 210, Hadithi ya 1057; Majmauz-Zawaidi Juz.1, Uk. 189.
152. Musnad Ahmad, Juz. 4, Uk. 281.
153. Fadhailus-Swahaba cha Ahmad bin Hanbal Juz. 2, Uk. 615, Hadithi ya 1052.
154. Sahih Muslim Juz. 4, Uk. 1871 – 1873, hadithi ya 32-35. Sahih Bukhari Juz. 5, Uk. 23.
155. Sahih Muslim Juz. 5, Uk. 1870, Hadith ya 32 – 35. Sahih Bukhari Juz. 5, Uk. 23.
156. Nayo ni kauli yake (s.w.t.): “Wale watoao mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhahiri” (Surat al-Baqarah: 274).
157. al- Mustadrak Juz.3.Uk.32. Tarikh Baghdad Juz.13.Uk19. Hadithi ya 6978. al-Firdawsu Bimaathuril-Khitwab Juz.3.Uk.455.Hadithi ya 4506.
158. Imekuja katika Faraidus-Samtiin Jalada. 1.143 hadithi ya 105, kutoka kwa Abdullah bin Akiim al-Jahniy. Amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): “Kwa hakika Mwenyezi Mungu alinifunulia wahyi usiku wa miraji, wa vitu vitatu kumhusu Ali (a.s.): Kuwa yeye ni Bwana wa waumini na Imam wa wachamungu na na kiongozi wa pekee.” Na pia mfano wa hayo yakiwa na tofauti kidogo, yamekuja katika Uk.145 Hadithi ya109. Na katika Biharul-Anwar Juz. 18.Uk.343. Na katika Safinatul-Bihar Juz.1.Uk.133.
159. Kifayatul-Athar.Uk.37. Biharul-Anwar Juz. 36.Uk.289.
160. Musnad Ahmad. Juz.3.Uk.3 na Uk.62. Sunan Tirmidhiy Juz.5. Uk.614. Hadithi ya 3768. Tarikh Baghdad.Juz.11.Uk.90. Kanzul-Ummal.Juz.12.Uk.112. Hadithi ya 34246.
161. Musnad Ahmad Juz. 5, Uk. 92, na Uk. 94; al-Muujamul-Kabiir, Juz. 2, Uk. 236, Hadithi ya 1875 na Uk. 248, Hadithi ya 1923.
162. Sahih Bukhari Juz. 4, Uk. 218.
163. Sahih Muslim Juz. 3, Uk. 1453, Hadithi ya 10.
164. Sahih Muslim Juz. 3, Uk. 1452, Hadithi ya 5; Musnad Ahmad, Juz. 4, Uk. 94 na Uk. 96.
165. Majmauz-Zawaidi Juz. 5, Uk.197, na Juz. 6, Uk. 442; Mushkilul-Athaar Juz.1, Uk. 224; Musnad Ahmad bin Hanbal Juz. 2, Uk. 175 na Uk. 223 chapa ya al- Maymaniyah; Al-Kamilu Fi Dhuafai cha Ibnu Udiy Juz. 5, Uk. 1816; Bidaya Wan-Nihayah Juz. 7,Uk.165; Sharh Nahjul-Balagha cha Ibnu Abul Hadidi Juz. 8, Uk. 259, Kukiwa na tofauti kidogo.
166. Kifayatul-Athar Uk. 79- 73.
167. Sharhu Nahjul-Balagha cha Ibnu Abil Hadid Jalada la 16, Uk. 280 – 281.
168. al-Imamah Was-Siyasah, Juz. 1, Uk. 22; Kanzul-Ummal. Juz. 5, Uk. 588, Hadithi ya 14046 na Hadithi ya 1405; Tarikhut-Tabariy Juz. 3, Uk. 210; Nahjul- Haqi Uk. 264; Sharhu Nahjul-Balagha cha Ibnu Abil Hadid Jalada.1 Uk. 169.
169. al-Imamah Was-Siyasah, Juz. 1, Uk. 22; Kanzul-Ummal, Juz. 5, Uk. 588, Hadithi ya 14046 na Hadithi ya 1405; Tarikhut-Tabariy Juz. 3, Uk. 210; Nahjul- Haqi Uk. 264; Sharhu Nahjul-Balagha cha Ibnu Abil Hadid Jalada.1, Uk. 169.
170. Angalia: Al-Milalu Wan-Nahlu cha Shahrustaniy Juz. 1, Uk. 144; Sharhu Nahjul-Balagha cha Ibnu Abil Hadid Jalada la 4, Uk. 96.
171. al-Imamah Was-Siyasah. Juz. 1, Uk. 14.
172. Sharhus-Sunna cha al-Baghawiy, Juz. 12, Uk. 108; Majmauz-Zawaidi, Juz. 6, Uk. 251; Kashful-Astar Juz. 2, Uk. 211

Hadithi ya 1538.

173. Naye ni mtu aliyekufa na hakuacha mtoto wala mzazi.

174. al-Imama Wasiyasah Juz.1, Uk. 191, Nahjul-Haq, Uk. 27; Na katika Sharhu Nahjul-Balagha cha Ibnu Abil Hadid Jalada la 2, Uk. 56 kuna: Umar aliwajia ili aiunguze nyumba wakiwemo ndani. Ndipo Zuberi alimtokea kwa upanga, na Fatima alitoka (a.s.) hali analia na kupiga kelele, akiwazuia watu. Hayo yameelezwa kutoka kwa Abu Bakr al-Jawhariy.

175. Nahjul-Haq, Uk. 272; Usudul-Ghabah, Juz. 2, Uk.14; Swawaiqul-Muhriqa Uk.175, chapa ya al-Muhammadiyah na Uk. 105. chapa ya al-Yamania, Misri.

176. al-Imamah Was-Siyasah Juz. 1, Uk. 14; Murujud-Dhahabi. Juz. 2, Uk. 301 –302; Nahjul-Haq Uk. 265.

177. Tarikhul-Khamisi Juz. 2, Uk. 167, Sahih Bukhari Juz. 6, Uk. 17.

178. Durul-Manthur Juz. 2, Uk. 466. Nahjul-Haqi Uk. 278; Sharhu Nahjul- Balagha cha Ibnu Abil Hadid Juz.1, Uk.182. na Juz. 12, Uk. 17.

179. Nahjul-Haqi Uk. 279.

180. Ahkamul-Qur'an cha al-Jaswaswi Juz. 3. Uk.61.

181. Nahjul-Haqi, Uk. 281; ad-Durul-Manthur, Juz. 2, Uk. 487.

182. Al- Imamah Wasiyasah Juz. 1,Uk. 28 – 29, Nahjul-Haq, Uk. 285, Hadithi imetangulia na toleo lake.

183. Sharhu Nahjul-Balagha cha Ibnu Abil Hadid Juz.16. Uk. 274.

184. Sharhu Nahjul-Balagha cha Ibnu Abil Hadid Juz.3, Uk. 18. Tarikhul-Khamisi, Juz. 2, Uk. 255 na Uk. 259; al-Kamilu Fii Taarikhi Juz. 3, Uk. 52; al-Imama Wasiyasa Juz.1, Uk. 32. Usudul-Ghaba Juz.5. Uk.90. Nahjul-Haqi. Uk. 290.

185. Tarikhul-Khamisi Juz. 1, Uk. 26, Tarikhut-Tabariy Juz. 5, Uk. 49; Tarikhu al- Yaaquubiy, Juz. 2, Uk. 155; al-Maarif cha Ibnu Qutaybah Uk. 84, Nahjul-Haq Uk. 293; Sharhu Nahjul-Balaghah cha Ibnu Abil Hadiid Juz.1, Uk. 198.

186. Nahjul-Haqi Uk. 294; Tarikhul-Khamisi, Juz. 2, Uk. 262; Sharhu Nahjul- Balaghah cha Ibnu Abil Hadiid Juz.1, Uk. 199; Tarikhul-Khulafai; Uk. 164.

187. Nahjul-Haqi Uk. 296; Tarikhul-Khamisi; Juz. 2, Uk. 271; Sharhu Nahjul- Balaghah cha Ibnu Abil Hadiid Juz.1, Uk. 238; al-Imama Wasiyasa Juz.1, Uk. 32.

188. Tarikhul-Yaaqubi Juz. 2, Uk. 162; al-Kamilu Fii Tarikhi Juz. 3, Uk. 56. Nahjul- Haq, Uk. 298. Ansabul-Ashrasf, Juz. 5, Uk. 52; Murujud-Dhahabi.Juz.2, Uk. 339.

189. Angalia: Yanabiul-Mawaddah, mlango wa 71 Uk. 350; Maqtalul-Husein (a.s.) cha Muqrim.

190. al-Kushkuul cha Al-Bahrainiy Juz. 2, Uk. 28.

# Orodha Ya Vitabu Vilivyo Chapishwa Na Al-Itrah Foundation:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora

9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)

48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliy onyooka
75. Shia asema haya, Sunni asema haya, Wewe wasemaje?
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali

87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqalain
102 Fatima al-Zahra
103. Tabaruku
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Idil Ghadiri
107. Mahdi katika sunna
108. Kusalia Nabii (s.a.w.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Nne
112. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
113. Shiya N'abasahaba
114. Iduwa ya Kumayili
115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Vikao vya Furaha
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
119. Ukweli uliopotea sehmu ya Tatu
120. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Historia na sera ya vijana wema
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi

126. Visa vya kweli sehemu ya kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaa ya kijamii
136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
137. Taqiyya
138. Mas-ala ya Kifiqhi
139. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili
141. Azadari
142. Wanawake katika Uislamu na mtazamo mpya

## Back Cover: Ukweli Uliopotea

Kitabu hiki ni utafiti uliofanywa na mwanachuoni wa Sudan, Sheikh M'utasim Sayyid Ahmad. Mwanachuoni huyo alikuwa ni wa madhehebu ya Sunni, aliamua kufanya utafiti juu ya madhehebu hizi mbili, yaani Sunni na Shia na utafiti wake huu ukazaa kitabu hiki ambacho amekiita, *Ukweli ukiopotea.*

Pia katika jitihada yake hii, amejaribu kuelezea kwa urahisi kabisa njia za kupunguza (kama si kuondoa kabisa) misuguano iliyopo baina ya Waislamu na baina ya madhehebu.

Nia kubwa ya mwandishi huyu ni kutafuta na kuugundua ukweli. Hata hivyo kusema ukweli na kuutafuta wakati mwingine huchukuliwa kama jinai isiyosameheka. Lakini msema kweli ni mpenzi wa Mwenyezi Mungu; na mafunzo ya Uislamu yamejaa msisitizo wa kusema kweli hata kama ni mchungu, na hata kama unamhusu mpenzi wako au juu yako wewe mwenyewe. Ukweli siku zote huelea juu - kamwe hauzami.

Kimetolewa na kuchapishwa na:
**Alitrah Foundation**
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640/ 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com [14]
Tovuti: www.ibn-tv.com [15]

**Source URL:** https://www.al-islam.org/node/25164

**Links**

[1] https://www.al-islam.org/user/login?destination=node/25164%23comment-form

[2] https://www.al-islam.org/user/register?destination=node/25164%23comment-form

[3] https://www.al-islam.org/person/sheikh-mu%E2%80%99tasim-sayyid-ahmad

[4] https://www.al-islam.org/organization/al-itrah-foundation-0

[5] https://www.al-islam.org/person/sheikh-harun-pingili

[6] https://www.al-islam.org/library/general-belief-creed

[7] https://www.al-islam.org/tags/historia

[8] https://www.al-islam.org/tags/dini

[9] https://www.al-islam.org/tags/madhehebu

[10] https://www.al-islam.org/person/imam-ahmad-bin-hanbal

[11] https://www.al-islam.org/person/imam-jaffar-sadiq

[12] https://www.al-islam.org/person/imam-malik-bin-anas

[13] https://www.al-islam.org/person/imam-abu-hanifa

[14] mailto:alitrah@raha.com

[15] http://www.ibn-tv.com